DIGNITY

www.dignityonline.org.uk

Misingi 2:

# Maisha Hukua

Kuandaliwa na Sarah Small, Jon Paul Witt, Alan Scantlebury na Jo Kimball



# Misingi 2
# Maisha Hukua

*'Wapate kuitwa miti ya haki,*
*iliyopandwa na BWANA, ili atukuzwe.'*

*Isaya 61:3*

**Misingi 2: Maisha Hukua, Toleo la Kwanza, Januari 2018**
Haki Miliki @ Dignity 2018. Haki zote zimehifadhiwa.

**Wasiliana na Dignity**

Kwa Posta: 6 Barlow Moor Road, Didsbury, Manchester, M20 6TR, UK

Kwa Tovuti: hello@dignityonline.org.uk

Kwa Simu: +44 (0)7340 573 937

**Shukrani**

Dignity inamshukuru Yesu kwa maisha anayotoa kugundua ndani ya kitabu hiki. Dignity inamshukuru kila mtu na kumwamini kila aliyetoa mchango kwa kazi hii.

**Kazi ya Dignity**

Washiriki wa Dignity pamoja na wale wa kiunga kwenye jamii wanavuvia mabadiliko ya maisha na jumuiya kuleta uhuru kutoka kwenye umaskini kupitia mahusiano na Yesu. Tunayafikia haya kimsingi kupitia Vikundi vya Uzima, vikundi visivyo rasmi inayoongoza jumuia za Kikristo inayowaandaa watu kutembea karibu na Yesu na kuonyesha upendo kwa hao wanaowazunguka. Kupitia kazi yetu tuanawaona watu wakiishi maisha ya kushangaza na kuwa sehemu ya muujiza wa kila siku. Tafuta zaidi kwa: **www.dignityonline.org.uk**

**Kikundi nyuma ya Misingi**

Waandishi na wahariri: Sarah Small, Paul Witt, Alan Scantlebury na Jo Kimball

Wasomi wa Kitamaduni: Cornelius Chalwe, Gervas Chalwe na Dorothy Jikubi

Wasomi Wahakiki: Rachel Warner, Mark Vermes, na Elisabeth Cartwright

Mkalimani: Christopher John Mollel

**Dondoo za Biblia**

Biblia Habari Njema kwa Watu Wote (Yenye Vitabu vya Deuterokanoni): Tafsiri ya Ushirikiano wa Makanisa (BHN): Hakimiliki - 1995, 2001: kwa Chama cha Biblia cha Tanzania na Chama cha Biblia cha Kenya. Haki zote zimehifadhiwa.

**Taswira za Alama Zinazoongoza**

Taswira za Alama Zinazoongoza zimechorwa na Studio ya Metro Icon 5 iliyochapishwa na SyncFusion. Alama zimetumika kwa ruhusa.

# Misingi

***Misingi*** ni mafundisho inayowasaidia watu kugundua na kukua ndani ya mahusiano yao na Mungu na kuwatia moyo kuhudumia jumuiya zao. Iliandikwa ili iweze kutoa vifaa vilivyo bora ambavyo vingeweza kutumika kwenye maeneo mengi ya kijiografia na kwenye vikundi vya kitamaduni duniani pote. ***Misingi*** ni mkusanyiko wa seti ya vitabu vine, na kila kimoja kinayo vipindi kumi na vitatu ya mafundisho kwenye vikundi.

***Misingi*** imeandikwa na waandishi wageni waliojitolea toka duniani kote na kukusanywa na kuandaliwa na Dignity.

***Misingi 1: Maisha Yameanza*** inawalenga wale walio wapya au wasio na imani. Kwa mwanzo rahisi inawaongoza watu kwenye hatua hatua za mwanzo za imani na kumjua Mungu.

***Misingi 2: Maisha Hukua*** na kujenga msingi itakayowezesha imani kukua na kutoa ufahamu kwa baadhi ya maandiko yanayotumika ya Biblia na maombi.

***Misingi 3: Maisha Huumba*** umakini namna mitume walivyoishi ndani ya jumia walivyoleta mabadiliko kwa kila kilchowazunguka wao. Mkristo mwenye afya kwa kawaida huumba maisha waliyopewa kwenye jumuia zao na kwa watu wengine.

***Misingi 4: Maisha Hukomaa*** huonyesha jinsi Mkristo aliyekomaa anavyopaswa kuonekana. Kitabu hiki kinabeba mawazo wa mtiririko uliyobaki, ikizamisha na kupanua.

# Uandishi

***Misingi 2: Maisha Hukua*** iliandikwa na waandishi waliyojitolea toka duniani pote. Waandishi waliyochangia kwenye kitabu hiki wameorodheshwa kwa utaratibu wa alfabeti.

**Pete Davies** amemwoa Cher na wanao watoto 4 na wajukuu 2. Walikutana London kwenye chuo cha Biblia, mahali ambapo wote walisoma Theolojia ya BA(Hons). Walianzisha chuo cha Kikristo cha Ushirika, mahali walibaki kama washirika. Pete anapenda mchezo wa Ragbi na Cher anapenda stoo ya Uffizi kule Florence!

*Kipindi cha 9*



**Andy Economides** yeye ni mzungumzaji wa kimataifa mwenye kuhudumia kule Ungereza, Ulaya na Afrika. Anawezesha na kuvuvia Wakristo kwenye uongozi, kufikia nje na kuwasaidia maskini na penye mahitaji.

*Kipindi cha 6 inayohusiana na Ukrasa 1 wa kitabu cha Andi Uhusiano*[1] *wa kweli na ruhusa ya utu wema*



**Kurt Francis** ni Mchungaji Msaidizi wa Kanisa la Kikristo la Ruthin  Fellowship pale Wales. Amemwoa Ann, na anao vijana 3 na sasa babu anayejisikia. Anafurahia kusoma na kutumia muda wake na marafiki na familia na hasa uvuvi wa samaki.

*Kipindi cha 5*



**Randall Hardy** aliletwa Yorkshire kule Uingereza kabla ya kuhamia Manchester. Akiwa na mkewe Mary, wakitoa elimu elimu kamili ya Kikristo kwa watoto tao 6 wakiwa na wito kamili kwenye maisha yao. Randall alianzisha huduma ya mafundisho ya Biblia (www.amen.org.uk) akifanya kazi kamą mtu aliyejiajiri mwenyewe fundi wa umeme kwa miaka 20.

*Kipindi cha 1 na 3*

---

[1] Economides, Andy, (2013) *True Relationships* Emsworth: Soteria Trust pages 9 -17



**Jo Kimball** amekuwa sehemu ya timu ya Dignity kuanzia 2008, akitembea mbali Zambia kufanya kazi na Vikundi vya Uzima na Kuvuvia Timu. Yeye ni muunganishaji na mtia moyo anayefurahia akiwaona wengine wakistawi na kujifunza nini maana ya kupendwa na Yesu.

*Kipindi cha 11*



**Debs Marks** aliayaishi maisha yake kule Manchesta, Uingereza. Aliolewa na Colin na binti yake Lizzy hicvi karibuni aliendа chuo kikuu. Debs anapenda kuwezesha kanisa kuwasaidia wakimbizi kumjua Yesu na kufanya kazi ya kujitolea akiwapa wakimbizi malazi.

*Kipindi cha 10*



**Gwen Mason** ameoa na anao wasichana 2. Gwen ametokea Sierra Leone mahali ambapo amewasaidia wanawake kuanzisha biashara. Kwa sasa anaishi Manchester na amewasaidia wakimbizi kura na makazi, kuwasaidia wanafunzi kuwa na makao kwa vijana kufanya kazi kama wanatheolojia kwenye makazi ya Wakristo. Anapenda kuandika kwa Bwana na kuwafikia watu.

*Kipindi cha 2*



**Alan Pugmire** amekuwa mtu wa Kanisa Uingereza kasisi kwa zaidi ya miaka 50. Kwa miaka 40 aliishi Manchester na ni Mzinga wa Manchester Cathedro. Alistaafu mwaka 2002 ila aliendelea na huduma akihubiri. Amekuwa mjane kuanzia mwaka 1999 na ana watoto watatu walioolewa na wajukuu 8. Kwa muda wake alipenda kutembea na kutunza bustani yake.

*Kipindi cha 7*



**Sarah Small** alilelewa na kukua Yorkshire halafu akasomea Dini na Theologia kule Manchester. Miaka 10 iliyofuata alifanya kazi kwenye kitengo cha kujitolea Uingereza na Afrika, sasa anajihusisha na umisheni maeneo ya vijijini kule Uingereza. Anashiriki uongozi wa kanisa, kazi ya kujitolea na ana familia ya watoto 2 na hivi karibuni amemaliza elimu ya MA kwenye Theologia ya Kingdom.

*Kipindi cha 4 na 13*



**Bernard Witika** ni kiongozi wa kikundi na muunganishaji. Alijifunza na kuwa kiongozi wa kanisa na kuanzisha makanisa Lusaka kabla Bwana hajamwita kurudi mijini mahali alipokuwa na kukutana na Yesu. Bernard hamu yake ni kuona watu wengine wakija kwa Yesu.

*Kipindi cha 12*



**Jon Paul Witt** ni mwanzilishi wa Dignity na amefanya kazi na makanisa ndani ya nchi nyingi. Ni mtu mwenye kufikiri, mwanzilishi, mwinjilisti na misionari. Jon amemuoa Judith na wanao watoto 3. Wanaishi kati ya Zambia na Uingereza. Hisia za Jon ni kuwaona watu kufikia kumjua Yesu na kwa hisia kali kuweza kubadilisha jumuia zao.

*Kipindi cha 8*

# Yaliyomo

Namna ya kutumia kitabu hiki ....................................................................... 10
Kuhakikisha usalama wa watoto pale kwenye Vikundi vya Uzima ............................ 15
1: Roho Mtakatifu ni nani? ............................................................................... 16
2: Ujazwe na Roho Mtakatifu............................................................................. 28
3: Tumeumbwa kwa Sura ya Mungu ..................................................................... 38
4: Tabia ya Mungu ni Upendo ............................................................................. 48
5: Tunda la Roho – Tabia .................................................................................. 56
6: Wabariki hao Wanaotuzunguka........................................................................ 66
7: Ugonjwa Unaoua – Dhambi ............................................................................. 76
8: Nini Maana ya Kusamehe - Neema ................................................................... 86
9: Sisi ni wa Mungu - Ukombozi .......................................................................... 96
10: Tu Wasafi Mbele za Mungu – Uthibitisho ....................................................... 106
11: Kuchukuliwa kwenye Familia ya Mungu ........................................................... 118
13: Ufupisho wa Kipindi ..................................................................................... 138

# Namna ya kutumia kitabu hiki

Kitabu hiki kimeandaliwa kutumika kwa mafundisho ya kikundi. Ni kiongozi anayeongoza kikao ndiye anahitajika kuwa na nakala ya kitabu hiki. Unapaswa kujaribu kukamilisha kila kikao kwa muda wa saa 1.5 – 2. Kama utaona unahitaji muda mrefu, siku zote utamaliza kikao 1 kwa muda muda wa wiki 2.

Inafikirika kuwa watu wanaojifunza kitabu hiki tayari wameshasoma ***Misingi 1: Maisha Yameanza***. Hii ina maana kuwa mawazo mengine hayajaelezwa kwenye kitabu hiki. Kama watu wengine wanajiunga na kikundi chako ambao ni Wakristo wapya unatakiwa kukamilisha mawazo mengine toka ***Misingi 1: Maisha Yameanza*** pamoja nao. Namna moja ya kufanya hivyo ni kuanzisha kikundi kingine. Kitabu cha ***Panda*** cha Dignity itakusaidia na haya.

**Namna ya kuongoza kikao**
Ni muhimu kumhusisha kila mtu kwenye kikao. Siyo tu kwa wepesi kusoma kikao na kuwaambia watu jambo wanalopaswa kufanya. Tunaamini kuwa kila mtu anacho kitu cha kipekee cha kuchangia na Mungu hutufundisha kupitia hao wanaotuzunguka. Kwa ajili hiyo, vikao vimeandaliwa kwa namna ambayo kila mtu anapaswa kuhusika. Kuna vifungu vya kukumbuka, maswali, maigizo, hadithi na majadiliano yanayomhitaji kila mtu kuhusika.

Kama kiongozi wa Kikundi unapaswa kuhamasisha majadiliano na kusaidia yaendelee kwa njia iliyo sahihihi, lakini hupaswa kufanya kila jambo mwenyewe.

Unapaswa kuwatia moyo watu wenye aibu na wakimya kujaribu na kuongea wanapoweza. Unapaswa kuwatia watu moyo wenye kelele na wazungumzaji sana kuwapa wengine nafasi kushirikisha mawazo yao pia.

**Unachohitaji kwa kila kikao**

Vikao vimeandaliwa kuwa vyepesi na aihitaji vyanzo vingi. Utahitaji:

- Nakala ya kitabu hiki kwa mtu anayeongoza kikao
- Biblia (itasaidia ikiwa watu wachache kwenye kikundi kuleta Biblia pia, lakini siyo lazima)
- Kalamu na karatasi, ambavyo mara zote hutumika kwenye shughuli. Unapaswa kuwatia watu moyo kuleta vitu hivyo toka nyumbani.

Ikiwa kuna kitu kingine kitahitajika, hii inatakiwa kujulikana kikao kinapoanza na inahitajika kwa ajili gani. Unapaswa kuandaa vitu hivi mapema.

**Ishara za kukusaidia wewe**

Kukusaidia wewe kuongoza kikao tumejumlisha ishara kukjulisha wewe kila sehemu ni nini. Ishara zimeonyeshwa hapo chini na maana yake. Chukua muda kujua kila ishara ina maana gani na kutazazama baadhi ya vikao na kujua jinsi kila ishara inavyotumika. Hii itakurahisishia wewe wakati unaongoza kikao.



**Maandalizi**

Kuhakikisha kuwa kila kikao kinafanyika kwa urahisi hapa kuna vitu vyepesi unavyopaswa kufanya ili kuandaa. Hii inajumlisha wewe kuwa na uhakika kuwa na vitu vyote unavyovihitaji kwa ajili ya kikao tayari na kuandaa watu wa kujitolea kabla ya kukutana. Unapaswa kuangalia mambo haya siku chache kabla hujafanya kikao hivyo utakuwa na muda wa kufanya yale yanayopaswa kufanyika.



**Lengo**

Kila kikao huanza na lengo. Hii itakuongoza wewe kwa yale unayoyafundisha kikundi na kile ambacho kila mtu anapaswa kukielewa anapomaliza kikao. Unapaswa siku zote kutunza malengo haya kwenye fikira zako na kujiuliza kama unawasaidia watu kuyafikia. Ni wazo jema kuanza kushirikisha haya kwenye kikundi.

**Kifungu cha Kukumbuka**

Kila mmoja anapaswa kujifunza kifungu cha kukumbuka na kuweza kukariri mwisho wa kikao. Unapaswa kuwafundisha kwa kusoma kifungu cha kukumbuka na marejeo ya Biblia kwa sauti kwa kikundi. Soma tena lakini kwa wakati huu soma hatua kwa hatua, kwa sehemu ndogo, waambie kikundi kurudia kila sehemu baada yako. Rudia utaratibu huu, pole pole soma sehemu ndefu pamoja na kikundi ukirudia kila sehemu mpaka kila mtu aweze kukariri kifungu chote bila msaada wako. Watie moyo watu wengine wajaribu na kurudia wao wenyewe.

**Hadithi**

Hadithi ni njia nzuri sana ya kutambulisha somo na kujifunza kutoka kitu kinachojulikana. Kila mtu hufurahia hadithi na ni rahisi kukumbuka! Unapo hadithia kikundi, unapaswa kuwaleta kwenye maisha halisi kwa kutumia maigizo. Ikiwa kama kuna mtu kwenye kikundi chako ambaye ni mzuri kwenye kuhadithia itakuwa ni vizuri kuwaambaia wahadithie. Unapaswa kuwaambia mapema kabla ya kikao na kuwapa nafasi ya kujiandaa.

**Kujifunza Biblia**

Kila kikao walao inayo ukrasa 1 wa Biblia wa kusoma, na zingine inayo zaidi. Ikiwa kama kuna watu kwenye kikundi chako wasomaji wazuri unaweza kuwaambia kusoma hayo kwa niaba yako. Unapaswa kuwaambia mapema ili waweze kufanya mazoezi au wakuambie kuwa hawawezi kusoma. Kumbuka kuwa watu wengine hawajui kusoma hivyo unapowaambia kusoma mbele za watu wakati hawawezi kusema hapana ni kama kuwadhalilisha.

**Kuongea**

Hizi ni sehemu zinazopaswa kusomwa kwa sauti toka kwenye kitabu. Unapoyapitia haya unapaswa kuweka kituo mara kwa mara, hasa kwenye pointi za muhimu, na waulize watu kama wameelewa yale unayoyasema. Kama hawajakuelewa, unaweza kurudia sehemu au kujadili jambo kuwasaidia kuelewa.

**Maswali na Kujadili**
Kujibu maswali na kujadili mambo huwasaidia watu kujifunza na kuanzisha kitu wao wenyewe. Hii itawasaidia kukumbuka. Unapoona ishara ya swali ni muhimu kuuliza kikundi swali na kuwatia moyo baadhi ya watu tofauti kutoa majibu. Wakati mwingine maswali ni ya majadiliano kwenye vikundi vidogo. Kama kikao kikikuonyesha hivyo, unapaswa kugawanya watu kwenye vikundi vya 3 au 4 na kuwapa muda wa kujadili maswali. Kama kikundi chote wakija kwa pamoja unapaswa kutoa muda kwa kila kikundi kushirikisha moja au mbili ya pointi walizojadili.
Ikiwa kama kuna maswali mengi ama marejeo ya Biblia ambayo watu watakutaka wewe unaweza kumtia mtu moyo toka kila kikundi kupiga picha swali kutumia simu zao ama kuandaa kabla kwa kuandika nakala ya ziada ya maswali.

**Shughuli**
Watu hujifunza wakati wanapokuwa na vitu vya kuwafurahisha na kwa kufanya jambo fulani. Shughuli husaidia jambo hili kutokea. Unapaswa kumhusisha kila mtu kwenye shughuli na kuwatia moyo wawe na vitu vya kufurahisha wakati wanapofanya hivyo!

**Maombi**
Yale ambayo Mungu anasema moja kwa moja ni ya muhimu sana. Tunataka kutia moyo kikundi chako kuomba na kuombeana pale inapowezekana. Unapoona ishara hii unapaswa kuwaambia watu kuomba. Kuna namna tofauti ya kuomba ambayo imetumika kwenye kitabu hiki chote. Wakati mwingine kikundi inaweza kuambiwa kwa pamoja, wakati mwingine kwenye vikundi vidogo na wakati mwingine wawili wawili. Wakati mwingine watu wanaambiwa wapige kelele kwa Mungu na kwa wakati mwingine watu wanaambiwa kuomba kimya kimya. Ni muhimu kuwa unaacha muda wa kutosha kwa maombi na kuwatia watu moyo kusikiliza yale anayoyasema Mungu.

**Kufanya wiki hii**
Kila wiki kuna kazi ya nyumbani ya watu kufanya. Unapaswa kueleza kwa uangalifu kuwafanya watu kuelewa na uwatie watu moyo

kufanya haya wakati wa wiki. Mwanzoni mwa kikao, unapaswa kuwaruhusu watu wakati mwingine kutoa mrejeo kama wamefanya kazi hiyo waliyopewa.



**Shahidi**

Ni muhimu kuwa tunaonyesha upendo wa Yesu kwa hao wanaotuzunguka. Tunaweza kufanya hivyo kwa njia nyingi tofauti. Kila kikao hutupatia wazo namna ya kufanya jambo lenyewe. Unapaswa kulieleza kwa uangalifu jambo hili kwenye kikundi na kumtia moyo kila mmoja kufanya shughuli hizi wakati wa wiki. Tunapoonyesha upendo wa Yesu kwa hao wanaotuzunguka tunaamini Yesu atabadilisha maisha ya hao wanaotuzunguka na kuleta uhuru. Itakuwa ni vizuri kuwatia moyo wanakikundi kutunza kumbukumbu ya watu waliyozungumza nao kama sehemu ya shughuli hizi na kuwatia moyo kuendelea kuwaombea watu hao.

5 Dakika

**Kuweka muda**

Kwenye maeneo mengine tumeweka pendekezo la urefu wa muda ambao shughuli ama majadiliano utachukua. Hii itakusaidia wewe kutunza muda uliyokubalika kwenye kikao.

**Kurasa sa Biblia na marejeo**

Unapoona jina na namba imepigwa mstari namna hii Zaburi 1:4-6 inakurejesha wewe kwenye ukrsa kwenye Biblia. Maana yah ii hasa unatakiwa kusoma kutoka kwenye kitabu cha Zaburi, mlango wa 1 mstari wa 4 na 6.

# Kuhakikisha usalama wa watoto pale kwenye Vikundi vya Uzima

Kwa pamoja tunaweza kuja na sheria nyepesi ili kuhakikisha watoto wetu wako salama ikiwa wapo nyumbani au pamoja nasi kwenye Kikundi cha Uzima. Sheria hizi ni vema kuzitumia kwenye maeneo ya maisha yetu pia. Ikiwa tunafanya kazi mashambani, kanisani au pamoja na marafiki, Mungu anataka sisi kuhakikisha kuwa watoto wetu wako salama.

Kila mmoja anayehudhuria kwenye kikundi ni lazima kuhakikisha kuwa watoto wao wako salama nyumbani na wanaangaliwa na mtu anayehusika au waje na watoto wao.

Viongozi wa vikundi wanapaswa kuwakumbusha wanakikundi kuhakikisha kuwa watoto wao wako salama nyumbani na wanaangaliwa na mtu anayehusika na pia kuwakaribisha watoto kwenye kikundi.

Mtu yeyote aliyeko kwenye kikundi na anashughulika na watoto ni lazima asifanye kazi mwenyewe afanye na mtu mmoja ama wawili zaidi. Ikiwa ni watu wawili, wasitoke familia moja. (Lazima wawe wa familia tofauti.)

Hao wanaoshughulika na watoto kwenye kikundi wawe ni watu ambao wamehudhuria kwenye kikundi kwa walao miezi mitatu bila kukosa.

Viongozi wa vikundi na wanachama ni lazima wasipige picha za watoto wakatiijihusisha na shughuli za Vikundi vya Uzima.

Ikiwa watoto watashiriki chakula kwenye mikutano ya vikundi, hakikisha ni salama wao kula.

Wanachama wa Vikundi wakati wana tembelea watu kwenye jumuia ni lazima watembee wawili, kwa mfano wanaume 2

1

# Roho Mtakatifu ni nani?



'Kama mnanipenda, mtazishika amri zangu. Nami nitamwomba Baba, naye atawapa Msaidizi mwingine akae nanyi milele. Huyo ndiye Roho wa kweli ambaye ulimwengu hauwezi kumpokea, kwa sababu haumwoni wala haumjui. Ninyi mnamjua kwa kuwa yuko pamoja nanyi naye anakaa ndani yenu.'

Yohana 14:15-17

**Maandalizi**

Unachohitaji kwa kipindi hiki:

- Kuchagua Shughuli 1: Utahitaji kitu kizito, kwa mfano mbao, jabali ama gunia Ła mahindi.
- Kuchagua Shughuli 2: Utahitaji kitu kizito, kwa mfano mbao, jabali ama gunia la mahindi.

Uwe na:

- Mwambie mtu kwenye kikundi kusoma hadithi?
- Mwambie mtu kwenye kikundi asome kifungu cha Biblia?

5 Dakika

Mkaribishe kila mtu kwenye kikundi na kuwashukuru kwa kuja. Kama kutakuwepo na watu wageni waliojiunga na kikundi utaanza kwa kuwaeleza jina lako na kuwaambia wanakikundi kusema majina yao.

Unapaswa kuwaeleza kitakachotokea kwenye kikundi. Omba mambo mafupi, ya shukrani.

**Lengo**

Lengo la kipindi wiki hii ni kufahamu yale ambayo Biblia inasema juu ya Roho Mtakatifu, na hii ina maana gani kwetu kwa maisha mapya yanayokuwa kwetu.

**Kifungu cha Kukumbuka**

5 Dakika

Soma kifungu cha kukumbuka na mistari ya Biblia kwa sauti kwa kikundi. Rudia kusoma tena kwa vifungu vidogo, uwaambie kikundi kurudia kila kifungu baada yaka. Baadaye soma kwa vifungu virefu wakati kikundi kikirudia kwa kila sehemu hadi kila mtu aweze kukariri kifungu chote. Watie moyo baadhi ya watu kujaribu kurudia wenyewe.

> *[15]Kama mnanipenda, mtazishika amri zangu. [16]Nami nitamwomba Baba, naye atawapa Msaidizi mwingine akae nanyi milele. [17]Huyo ndiye Roho wa kweli ambaye ulimwengu hauwezi kumpokea, kwa sababu haumwoni wala*

*haumjui. Ninyi mnamjua kwa kuwa yuko pamoja nanyi naye anakaa ndani yenu.*

*Yohana 14:15-17*

**Hadithi**

Soma Hadith inayofuata inayoitwa 'Bosi wa Makazi' kwa kikundi:

Mlinzi Nee alikuwa Mkristo wa Kichina aliyeishi toka maka 1903 hadi 1972. Alitokea kuwa kiongozi nje ya makanisa yaliyojengwa, akiwatia moyo Wakristo kukutana pamoja kwenye vikundi vidogo. Alijihusisha na uongozi wa mtandao mkubwa kwa makanisa ya nyumbani kwa zaidi ya maka 30. Mwaka wa 1949 kulikuwepo na Mapinduzi kule China na kenye Ukristo, na dini zote zikahirimishwa.

Nee akakaa gerezani kwa miaka ishirini ya maisha yake yaliyobaki. Aliandika vitabu vingi, na labda kinachojulikana sana 'Maisha ya Kawaida ya Mkristo'. Katika hicho alisisitiza juu ya umuhimu kwa wale waliyompokea Yesu kusikiliza na kutenda mwongozo wa Roho Mtakatifu, anayeishi sasa ndani yao.

Kufafanua jambo hilo aliwaambia mtu na mkewe ambao wamekuwa Wakristo kuendelea kutembelea kijiji kule milimani.

*Nilienda, kwa kuchelewa wakati moja wa kiangazi, kwa muda mrefu kwa mapumziko milimani mahali ambapo malazi yalikuwa magumu kupatikana, nikiwa huko ilikuwa ni lazima kwangu kulala nyumba moja na kula sehemu nyingine, badade ikawa nyumba ya makenika na mkewe. Kwa muda wa wiki mbili za mwanzo za kutembea kwangu, zaidi ya kubariki chakula, sikumwambia lolote mwenyeji wangu juu ya Injili; na siku moja nafasi ikapatikana ya kuwaeleza habari za Bwana Yesu. Walikuwa tayari kusikiliza na wakaja kwake kwa imani ndogo tu kwa msamaha wa dhambi zao. Walizaliwa mara ya pili, na nuru mapya na feraha imaja kwenye maisha yao, maana kulikuwepo na majadiliano hasa. Nilikuwa mwangalifu kuwaeleza hasa*

*kilchotokea, na baadaye, hali ya hewa ikawa baridi, ikafikia wakati kuagana nao na kurudi Shanghai.*

*Wakati wa mwezi wa baridi mtu alikuwa na tabia ya kunywa divai na chakula chake, na aliweza kuzidisha. Baada ya mimi kuondoka, na kurudi kwa baridi divai ilionekana mezani tena, na siku hiyo, baada ya mazoeya ya kumanya hivyo mumewe akainamisha kichwa kurudisha shukrani kwa ajili ya chakula lakini hakuna neno lililoweza kutoka kinywani mwake. Baada ya kujaribu mara moja au mbili kwa uchungu alimrudia mke wake. 'Kuna shida gani?' aliuliza. 'Kwa nini tusiombe leo? Lete Biblia uone kile ambacho kitasema kuhusu kunywa divai.' Niliacha nakala ya Maandiko kwao, ingawa mke wake angeweza kusoma lakini alikuwa haelewi Maandiko, na alitafuta yale maandiko mepesi kwenye somo. Hawakujua namna ya kukabiliana na Kitabu cha Mungu na haikuwezekana kukabiliana na ujumbe wa Mungu, maana nilikuwa maili nyingi na ingekuwa kama mwezi kabla hawajaniona. 'Basi kunywa mvinjo wako', mke wake alimwambia. 'Tutapeleka suluhisho kwa ndugu Nee kama nafasi ya kwanza.' Lakini bado mwanaume akajikuta hakuweza kurudisha shukrani kwa Bwana kwa ajili ya hiyo mvinyo. 'Hebu ichukue!' alisema kwa kirefu; nz baada ya kufanya hivyo, kwa pamoja waliomba baraka kwa mlo wao.*

*Wakati kwa kweli mtu aliweza kutembelea Shanghai alinieleza hadithi hii. Kutumia uwelewa wa Kichina: 'Ndugu Nee', alisema, 'Bosi aliyekuwepo asingeniruhusu kunywa mvinyo huu!' 'Vizuri sana, ndugu', Nimesema. 'Mara zote unamsikiliza Bosi mwenyeji!' Wengi wetu tunafahamu kuwa Yesu ni maisha yetu. Tunafahamu kuwa Roho wa Mungu anakaa ndani yetu, lakini ukweli huu una madhara kidogo kwenye tabia yetu. Swali ni kwamba, tunamjua Yeye kama mtua anayeishi, na tunamjua Yeye kama 'Bosi'?*[2]

[2] Nee, Watchman, (1961) *The Normal Christian Life* Eastbourne: Kingsway Publications, page 77

**Kujifunza Biblia**

Soma Yohana 14:15-21 kwenye kikundi:

> *15 "Kama mnanipenda, mtazishika amri zangu. 16Nami*
> *nitamwomba Baba, naye atawapa Msaidizi mwingine akae*
> *nanyi milele. 17Huyo ndiye Roho wa kweli ambaye*
> *ulimwengu hauwezi kumpokea, kwa sababu haumwoni wala*
> *haumjui. Ninyi mnamjua kwa kuwa yuko pamoja nanyi naye*
> *anakaa ndani yenu. 18Sitawaacha ninyi yatima, naja kwenu.*
> *19Bado kitambo kidogo ulimwengu hautaniona tena, ila ninyi*
> *mtaniona, kwa kuwa mimi ni hai, ninyi nanyi mtakuwa hai.*
> *20Wakati huo mtajua ya kuwa mimi niko ndani ya Baba na*
> *ninyi mko ndani yangu na mimi niko ndani yenu. 21Yeyote*
> *mwenye amri zangu na kuzishika ndiye anipendaye, naye*
> *anipendaye atapendwa na Baba yangu, nami nitampenda*
> *na kujidhihirisha kwake."*

Hadithi yetu na kifungu cha Biblia inatuonyesha kuwa tunapopokea zawadi ya maisha mapya kutoka kwa Mungu, anatupa zawadi yake mwenyewe kwa namna ya Roho Mtakatifu. Anakuja kuishi ndani yetu na kutuongoza na kutusaidia kuishi kwenye imani yetu mpya. Mkristo wa Kichina kwenye hadithi yetu inayomtaja Roho Mtakatifu kama 'Bosi Mwenyeji': anayeishi ndani na kumwelekeza kitu cha kufanya, akimsaidia kuishi tofauti. Kama Wakristo tunafahamu kuwa Mungu ni mmoja wa nafsi tatu: Mungu Baba, Yesu mwanaye na Roho Mtakatifu. Tutajifunza zaidi juu ya hayo kwenye kitabu 3 ya ***Misingi***.

**Mafundisho ya Yesu juu ya Roho Mtakatifu**

Kifungu chetu cha Biblia inatoka kwenye kitabu cha Injili ya Yohana, mahali ambapo kuna mafundisho mengi ya Yesu juu ya Roho Mtakatifu. Kabla Yesu alizungumzia juu ya 'kuzaliwa kwa Roho Mtakatifu' na 'Roho Mtakatifu kutoa maisha'. Alimtaja Roho Mtakatifu kuwa maji yaliyo hai ambayo 'yatabubujika kutoka ndani yao.'

Ilipofika wakati wa kufa kwa Yesu, haishangazi kuwad alichukua nafasi kuwafundisha wanafunzi wake naffs ambayo Roho Mtakatifu angetumika kwenye maisha yao. Yesu aliwahakikishia wao, kuwa atawaombea na kwamba Roho Mtakatifu atatumwa kwao akiondoka. Kwenye vifungu vyetu vya Biblia Yesu alimtaja Roho Mtakatifu kama wakili mwingine (angalia vifungu vya 16-17).

Neno ‘wakili’ imetafsiriwa kwa namna nyingi, akijulikana kama msaidizi, lakini pia rafiki na mfariji. Ina maana kuwa ‘moja wa kuwa naye’ au rafiki wa ‘kutembea naye’. Fikiri kama ungetaka kwenda sehemu fulani ya hatari mahali ambapo hujawahi kwenda huko nyuma. Ni vema kuwa na kiongozi anayefahamu maeneo na kilichoko mbele. Siyo tu kwamba kiongozi atakuonyesha njia ya kuiendea, lakini bado atakulinda na hatari zilizoko mbele zilizojificha, na kuandaa chakula chako na mahali pa kulala. Huyo ndiyo msaidizi ambaye Yesu alizungumzia habari zake kwa wanafunzi wake na angemtuma badala yake.

Kama jinsi Yesu alivyokuwa msaada kwa wanafunzi wake, sasa Roho Mtakatifu amechukua nafasi yake. Uwepo wa Mungu hautapungua tena kwenye uhalisi wa Yesu; kwenye uwepo wa Roho Mtakatifu unaoishi ndani moyo wa yeyote mwenye kumpokea. Roho Mtakatifu atawafundisha waamini wapya juu yake, na kuwaongoza kweny kweli. Roho Mtakatifu ni Mungu anayeishi ndani yetu kiła siku.

**Shughuli**

Unaweza kutumia moja ama shughuli zote mbili.

15 Dakika

**Chaguzi 1**

Utahitaji kitu kizito mfano kipande cha mbao, jabali ama gunia Ła mahindi.

- Muulize mtu mwenye nguvu wa kujitolea toka kwenye kikundi.

- Mwambie huyo mwenye kujitolea kile ambacho ungependa kufanya ni kubeba kitu kizito ulichokileta kwa ajili yao sehemu ya karibu.
- Mtu huyo atakapojaribu hilo mwombe mtu mwingine wa kujitolea.
- Kwa wakati huu waambie hao wenye kujitolea wote wabebe kitu hicho kizito kwa pamoja.
- Mwambie huyo mwenye kujitolea wa kwanza nini tofauti ya kubeba mwenyewe na kubeba kwa pamoja. Naamini jibu lao litakuwa ni bora kubeba hicho kitu kwa pamoja.

Waeleze kuwa Roho Mtakatifu ni msaada wetu; siku zote yuko pamoja na sisi kubeba mizigo yetu na kutusaidia kiła siku ya maisha yetu.

**Chaguzi 2**
Namna nyingine ya kufanya jambo hili ni kuonyesha kikundi situ isiyokuwa na moto.

- Waulize simu hiyo inaweza kufanya nini bila moto.
- Sasa unganisha Sims hiyo pate moto na uwashe. Waulize kikundi sasa situ inaweza kufanya nini?
- Tofauti ni moto kuwashwa sasa inaweza kufanya kazi nyingi ambayo imetengenezwa kufanya. Bila moto hatuwezi kutumia kwa lolote kabisa!

Waeleze kuwa Roho Mtakatifu ni nguvu ya Mungu ndani yetu, ambayo inaweza kupungua hivyo tunapaswa kuhakikisha mara zote 'tumechajiwa' na kujawa na nguvu za Roho Mtakatifu.

**Roho Mtakatifu kwenye Agano la Kale**
Roho Mtakatifu hapatikani tu kwenye mafundisho ya Yesu; ukweli ni kwamba yupo kwenye Biblia yote. Tunamsoma kwenye kwenye kitabu cha kwanza cha Biblia Mwanzo 1:2. Alikuwepo hapo mwanzoni mwa uumbaji wa dunia 'akitulia juu ya uso wa vilindi vya maji' wakati Mungu akiumba dunia. Tunamsoma akishukia watu binafsi, manabii na wafalme kwa kazi maalum, ila siyo kwa

kila mwamini kwenye nyakati za Agano la Kale. Manabii wawili pekee namna Roho Mtakatifu angefanya kazi baadaye. Ezekieli alimzungumzia akiwafanya watu wa Mungu kuwa watakatifu, akiwafanya kumtii yeye na Mungu akiweka Roho wake ndani ya watu. (Unaweza kusoma mambo haya kwenye kitabu cha Ezekieli 36:25-30). Nabii mwingine aliyeitwa Yoeli alizungumzia juu Mungu kumimina Roho wake baadaye kwa waamini wote. (Unaweza kusoma haya kwenye kitabu cha Yoeli 2:28-29).

**The Holy Spirit in the New Testament**

Tunasoma zaidi juu ya Roho Mtakatifu kwenye Agano Jipya. Yohana Mbatizaji alikuja akitangaza kuwa Yesu ndiye atakayeitimiza unabii huo akiwabatiza kwa Roho Mtakatifu. Maneno ya Yohana yalirekodiwa kwenye Injili zote nne, ambayo yaliwapa maana kubwa. Baada ya kufufuka, Yesu aliwaambia wanafunzi wake kusubiri Yerusalemu maana alikuwa karibu kutuma 'zawadi aliyoahidi Baba' juu yao (Luka 24:49 na Matendo 1:4) – kudhibitisha wazi kutimiza unabii wa Yoeli, Ezekieli na Yohana Mbatizaji.

Siku ile Roho Mtakatifu alipowashukia waamini wote inaitwa siku ya Pentekoste. Siku ile mkutano wa watu walikusanyika na Petro, mmoja wa wanafunzi wa Yesu akawaambia mkutano:

> 38 *Petro akawajibu, "Tubuni, mkabatizwe kila mmoja wenu kwa jina la Yesu Kristo, ili mpate kusamehewa dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.* 39 *Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu na watoto wenu, na kwa wote walio mbali, na kila mtu ambaye Bwana Mungu wetu atamwita amjie."*
>
> *Matendo 2:38-39*

Ufahamu kuwa kila Mkristo anaweza sasa kupokea ahadi ya Roho Mtakatifu; pia ambayo Mungu aliahidi kuwafikia zaidi ya wale waliokuwepo hapo siku zile (pamoja na wale ambao hawakuwa Wayahudi) wale ambao Mungu amewaita kwa sasa, na kwa baadaye. Hii inatuhusu nyakati hizi. Roho Mtakatifu ni zawadi

toka kwa Mungu kwa Wakristo, zawadi ambayo anaendelea kutoa kwetu tena na tena kwa vile anaishi ndani yetu na kutusaidia kukua.

10 Dakika

**Maswali**

Kwenye kikundi cha 3 au 4 mchukue dakika 10 mkijadili maswali yafuatayo:

- Uliwahi kuwa na ujuzi wa kuongozwa na Roho Mtakatifu? Maswali yafuatayo itawasaidia watu kufikiri juu ya haya zaidi. Wameweza:
- Kufanya jambo lorote na sauti ikakuambia usifanye?
- Kusikia kukiri jambo lorote kwa Mungu?
- Uliwahi kujisikia kufanya jambo lolote kwa nguvu ambalo kwa kawaida hufanyi?
- Uliwahi kutiwa moyo wakati unasoma Biblia au kwenye maombi?
- Uliwahi kujisikia kubadilisha mwenendo wa tabia zako?
- Uliwahi kuwa na ujuzi wa kuongozwa na Roho Mtakatifu?
- Umetiwaje moyo kwa yale ambayo umejifunza kuhusu Roho Mtakatifu leo?

5 Dakika

**Maombi**

Kama kikundi, ombeni kwa pamoja ili kila mtu akut kwenye uelewa juu ya kazi ya Roho Mtakatifu na kazi zake kwenye maisha yako.

Sasa mgawanyike wawili. Waambie watu washuhudiane na watu wengine wa wawili kama wanafikiri wamempokea Roho Mtakatifu bado. Watie moyo waombeane moja kwa mwingine.

- Kama kuna mtu hana uhakika wa kumpokea Roho Mtakatifu waulize kamą wanataka kumpokea wawekee mikono na uwaombee Roho Mtakatifu kuwajaza. Waambie waombe pamoja na wewe.

- Kama kuna mtu amempokea Roho Mtakatifu, waombee wajazwe tena pamoja na waweze kusikiliza sauti wazi na watendee kazi yale waliyosikia.

**Kufanya Wiki Hii**

Kila wiki kuna kazi ya nyumbani ya kufanya. Wiki hii uwe na muda wa kutosha ukimwomba Roho Mtakatifu kukuongoza, na uwe na muda kiasi wa kusikiliza nanachosema. Mwombe akusaidie kwa mambo anayokuongoza. Kuna pia mafundisho ya kuendelea ambayo unaweza kufanya ikiwa unamiliki Biblia.

**Shahidi**

Unapochukua muda kuomba na kumsikiliza Roho Mtakatifu wiki hii, hakikisha uwepo wake unapokuwa karibu na watu wengine. Mwombe akusaidie uwaeleze wengine kuwa umekuwa naye wiki hii, na usikilize namna anavyokuongoza kuyafanya haya. Unaweza pia kuwaambia Wakristo wengine ni ujuzi gani waliyonayo wakati Roho Mtakatifu anapowaongoza wao.

**Uchaguzi wa Kuendeleza Masomo**

Kama watu wanao muda na kumiliki Biblia (au rafiki mwenye Biblia) basi kuna zaidi ya kusma kutusu Roho Mtakatifu. Watie moyo wapige na picha ya ukrasa huu kwenye simu zao au kunakili kielelezo chini kwenye vitabu vyao vya kumbukumbu ili waweze kujifunza haya nyumbani. Vifungu vinavyofuata pia vinatufundisha zaidi juu ya Roho Mtakatifu:

Yohana 7:37-39 Inafundisha kuwa Roho Mtakatifu ni maji yaliyo hai.
Yohana 13:31-16:33 Yesu anazungumza juu ya Roho Mtakatifu na ahead aliyotoa ya kazi ya Roho Mtakatifu kwenye maisha ya waamini baada ya kurudi kwa Baba yake. Ikijumlisha:

- Yohana 14:26 - Roho Mtakatifu ni mwalimu
- Yohana 15:26 - Roho Mtakatifu hushuhudia habari za Mungu
- Yohana 16:13 - Roho Mtakatifu ni kiongozi

Warumi 8:14 Roho Mtakatifu hutuongoza kama watoto wa Mungu
Waefeso 4:29-32 Onyo tusiruhusu tabia zetu kumhuzunisha Roho Mtakatifu ndani yetu
1 Wathesalonike 5:19 Onyo msimzimishe Roho Mtakatifu

# Kumbukumbu

2

# Ujazwe na Roho Mtakatifu



'Kwa hiyo msiwe wajinga, bali mpate kujua nini mapenzi ya Bwana... bali mjazwe Roho.'
Waefeso 5:17-18

**Maandalizi**

Unachohitaji kwa kipindi hiki:

- Urefu wa kamba inayoweza kuvutwa kwa nguvu ya vita, labda mita 3 urefu.

Uwe na:

- Mwambie mtu kwenye kikundi kusoma hadithi?
- Mwambie mtu kwenye kikundi asome kifungu cha Biblia?
- Chagua watu wa kujitolea 6 kwa ajili ya shughuli na waeleze kitu cha kufanya?

**Karibu na Marejesho**

5 Dakika

- Mshukuru kila moja kwa kuja kwenye kwenye kikundi.
- Anza na maombi mafupi.
- Waulize kikundi kama wamefanya 'Kufanya wiki hii' na 'Shahidi' kazi ya wiki iliyopita.
- Waalike watu washuhudie kitu chochote walichojifunza au kuwa na ujuzi kwa kufanya kazi hizi.

**Lengo**

Lengo la kipindi wiki hii ni kufahamu kuwa tunapojazwa na Roho Mtakatifu tunapokubali zawadi ya Mungu ya maisha mapya, tunahitaji pia upya wa kila siku wa Roho Mtakatifu ili maisha mapya yaweze kukua. Kama tusipojazwa na Roho Mtakatifu, jinsi tulivyo, au kujaribu kufanya, ni kwa nguvu etu wenyewe, ambayo haitakuwa ni kitu.

**Kifungu cha Kukumbuka**

5 Dakika

Soma kifungu cha kukumbuka na nukuu za Biblia kwa sauti kwenye kikundi. Rudia kusoma tena kwa vifungu vidogo, waachie kikundi kurudia kila sehemu baada yako. Polepole soma tena kwa sehemu ndefu huku kikundi kikirudia kiła neno mpaka kiła moja atakapoweza kukariri kifungu chote. Watie baadhi watu moyo kujaribu na kurudia wao wenyewe.

*Kwa hiyo msiwe wajinga, bali mpate kujua nini mapenzi ya Bwana… bali mjazwe Roho.*

*Waefeso 5:17-18*

**Hadithi**

Wasomee kikundi hadithi inayofuata:

Kijana mdogo alikuwa na ndoto ya kumiliki gari lake siku moja kwa muda mrefu. Baadaye alifaulu kutunza fedha za kutosha, akapata moja aliyoiona kuwa ni mpango mzuri. Alichukua muda mrefu akilichunguza gari, akichunguza injini na hata alipata nafasi ya kuliendesha kulijaribu.

Baadaye mpango ulikamilika; alitoa fedha na akakabidhiwa ufunguo wa Toyota yake mpya. Kuna vitu vingi alivyovifikiria kufanya kwa vile sasa analo gari lake jipya. Anaweza sasa kuliendesha kazini badala ya kupanda basi, na hata aliweza kuwapa marafiki zake lifti. Sasa aliwezi hata kwenda mjini na kuwaona marafiki na familia yake, kwenda kwenye michezo na kutazama filamu ilio bora. Nafasi hazikuwa na mwisho.

Kitu cha kwanza alichoamua kufanya ni kutembelea mjini na marafiki wachache mwishoni mwa wiki moja. Waliondoka mapema vizuri na jinsi ilivyokuwa ni asubuhi maana ilikuwa ni safari ndefu, na ilikuwa imepoa kusafiri asubuhi. Walifika mjini na wakawa na wakati mzuri; pekee walipoamua kurudi nyumbani hapo ndipo walipokutana na tatizo. Gari liliondoka vizuri, akaliendesha kwa muda, na kwenye viunga vya mji ghafla gari lilianza kushtuka na kutetemeka na likasimama kabisa. Huyo kijana mdogo alichanganyikiwa kabisa. Gari hili jipya linawezaje kuharibika mikononi mwake mapema hivyo baada ya kulinunua?

Alimwita yule mtu aliyemuuzia kumuuliza kama yeye aliwahi kuwa na tatizo kama hilo, makati huo huo marafiki zake wakaanza kuulizia kama kuna mtu angeweza kuwasaidia kuliwasha hilo gari tena. Bahati nasibu makenika alipatikana aliyekuja kuliangalia gari. Alizungumza na kijana mdogo,  akimuuliza yote kuhusu gari.

Baadaye makenika alianza jukechea: akasema gari hilo lisingeweza kwenda popote alimwambia, kwa sababu liliishiwa mafuta!

Kijana aliona aibu; hakuwaza juu ya kuongeza gari lake mafuta, ni kwenye vitu vya anasa tu ndiyo angeweza kuzifanya. Kwa haraka mafuta kiasi yalipatikana, na gari likawashwa na marafiki wakawa tena safarini wakirudi nyumbani tena.

Hili lilikuwa ni fundisho tosha kwa huyo kijana mdogo: hata ingawa gari alilolinunua lilikuwa jipya na kufanya kazi vizuri, ingeendelea tu kufanya hivyo kamą angeliweka mafuta na kulitunza. Hivyo ndivyo ilivyo kwa maisha yetu mapya kwa Mungu – itaendelea tu kukua ikiwa sisi tutabaki tumejazwa nguvu za Roho Mtakatifu.

**Kujifunza Biblia**

Soma Waefeso 5:8-20 kwenye kikundi:

> [8]*Kwa maana zamani ninyi mlikuwa giza, lakini sasa ninyi ni*
> *nuru katika Bwana. Enendeni kama watoto wa nuru* [9]*(kwa*
> *kuwa tunda la nuru hupatikana katika wema wote, haki na*
> *kweli),* [10]*nanyi tafuteni yale yanayompendeza Bwana.*
> [11]*Msishiriki matendo ya giza yasiyofaa, bali yafichueni.*
> [12]*Kwa maana ni aibu hata kutaja mambo yale ambayo*
> *wasiotii wanayafanya sirini.* [13]*Lakini kila kitu kilichowekwa*
> *nuruni, huonekana,* [14]*kwa kuwa nuru ndiyo hufanya kila kitu*
> *kionekane. Hii ndiyo sababu imesemekana:*
> *"Amka, wewe uliyelala,*
> *ufufuke kutoka kwa wafu,*
> *naye Kristo atakuangazia."*
> [15]*Kwa hiyo angalieni sana jinsi mnavyoenenda, si kama watu*
> *wasio na hekima, bali kama wenye hekima,* [16]*mkiukomboa*
> *wakati, kwa sababu nyakati hizi ni za uovu.* [17]*Kwa hiyo*
> *msiwe wajinga, bali mpate kujua nini mapenzi ya Bwana.*
> [18]*Pia msilewe kwa mvinyo, ambamo ndani yake mna*
> *upotovu, bali mjazwe Roho.* [19]*Msemezane ninyi kwa ninyi*

*kwa zaburi, nyimbo na tenzi za rohoni, mkimwimbia na kumsifu Bwana mioyoni mwenu, [20]siku zote mkimshukuru Mungu Baba kwa kila jambo katika Jina la Bwana wetu Yesu Kristo.*

Paulo aliwaandikia Waefeso barua. Aliwaandikia kuwasaidia kujenga imani yao na kuwapa mwongozo wa kiroho. Inafikirika kuwa Paulo aliishi Efeso kwa muda wa miaka 3. Katika wakati huo aliwaaeleza watu juu ya zawadi ya Mungu ya maisha mapya kwa nia ya Yesu. Aliwafundisha pia kuwa ujumbe huo ulikuwa ni wa kila mtu, siyo kwa watu wa Kiyahudi tu. Wengi kutoka idadi ya watu wa Kigiriki, ambao kwa wakati huo waliabudu sanamu tofauti tofauti, miungu na miungu ya kike, wakaja kwa imani ya Yesu.

Waefeso, kama sisi, waliacha giza na kuja kwenye nuru. Wamekuja kwenye nyumba ya Mungu wetu siyo kamą watumwa au watumishi ila ni kama watoto wa Mungu. Walijazwa na Roho wake Mtakatifu na hiyo bado haikutosha. Walipaswa kuishi katika Roho. Walitakiwa kujawa kiła mara na Roho Mtakatifu ili wale safi, kuweta kupokea uongozi na kuonyesha uzuri, maisha ya haki na kweli.

Paulo alikubaliana na ukwell kwamba kule mbele Wagiriki walikuwa mbali sana na Mungu moja wa kweli. Kwa kuongezea, staili ya maisha yao yalikuwa yenye kuchukiza. Kabla ya kukutana na Yesu sisi pia tulikuwa mbali na Mungu ila sasa tumeyaacha maisha yetu ya zamani na kuingia kwenye mahusiano na Mungu Baba yetu.

Tumezaliwa mara ya pili na tumempokea Roho Mtakatifu wa Mungu. Sisi sasa tu watoto wa Mungu, lakini tunatakiwa kukua patika Mungu. Tunatakiwa sasa kujazwa na Roho Mtakatifu kiła wakati, ili kuweza kukuza mahusiano yetu na Mungu na kufanana na yeye.

**Maswali**

10
Dakika

Je ulishawahi kuamua kuwa unataka kuwa mtu wa tofauti? Pengine ulitaka kubadilika kitu kuhusiana na mwonekano wako, kujifunza kitu fulani mpya au kfubadilisha kazi yako au tania ebaya.

Ilienda namna gani?

Waambie kikundi kugawanyika kwenye kikundi kidogo cha 3 - 4 na kusoma Waefeso 5:8-20 tena. Waambie kuchukua vitu hivyo ambayo iliyoambatana na maisha yetu ya giza ya zamani na pia zile zilizoambatana na maisha yetu mapya kwenye nuru.

Hebu tutazame namna Roho Mtakatifu alivyobadilisha maisha ya mitume. Soma Matendo 4:31-37 kwenye kikundi:

> [31]*Walipokwisha kuomba, mahali walipokuwa wamekutanika*
> *pakatikiswa, wote wakajazwa na Roho Mtakatifu,*
> *wakanena neno la Mungu kwa ujasiri.*
>
> [32]*Wale walioamini wote walikuwa na moyo mmoja na nia*
> *moja. Wala hakuna hata mmoja aliyesema chochote*
> *alichokuwa nacho ni mali yake mwenyewe, lakini*
> *walishirikiana kila kitu walichokuwa nacho.* [33]*Mitume*
> *wakatoa ushuhuda wa kufufuka kwa Bwana Yesu kwa*
> *nguvu nyingi na neema ya Mungu ilikuwa juu yao wote.*
> [34]*Wala hapakuwepo mtu yeyote miongoni mwao aliyekuwa*
> *mhitaji, kwa sababu mara kwa mara wale waliokuwa na*
> *mashamba na nyumba waliviuza, wakaleta thamani ya vitu*
> *vilivyouzwa,* [35]*wakaiweka miguuni pa mitume, kila mtu*
> *akagawiwa kadiri ya mahitaji yake.*
>
> [36]*Yosefu, Mlawi kutoka Kipro, ambaye mitume walimwita*
> *Barnaba (maana yake Mwana wa Faraja),* [37]*aliuza shamba*
> *alilokuwa nalo, akaleta hizo fedha alizopata na kuziweka*
> *miguuni pa mitume.*

Kifungu kinatueleza kuwa mitume ‘walijazwa na Roho Mtakatifu.’ Hii ilibadilisha maisha yao kabisa. Waliweza sasa ‘kulinena neno la Mungu kwa ujasiri.’ Waliweza kuwa wakarimu wakashirikiana kiła walichokuwa nacho hivyo ‘hakukuwepo na mtu yeyote mwenye mahitaji kati yao.’ Roho Mtakatifu aliwajaza na hii ina maana kuwa waliweza kuvuta uwezo wa Mungu na uongozi kuishi kabila maisha ya tofauti kabisa na yale walyokuwa wanaishi.

Basi sisi turuhusu kujazwa na nguvu za Roho Mtakatifu. Ni Roho Mtakatifu ndiye atakayetuwezesha kumanya yale ambayo hatukuweza kufanya kwa sababu ya udhaifu. Mtu wa tabia yake kwenye Agano na Kale anayeitwa Zerubabeli alikuwa na wasiwasi juu ya kuanza mradi mkubwa wa ujenzi wa nyumba ya Mungu, lakini alipewa ujumbe ufuatao, ‘“Siyo kwa uwezo wala kwa nguvu, bali ni kwa Roho yangu,” aseme Bwana wa Majeshi.’ (Zakaria 4:6). Tunaweza kufanya zaidi kwa Roho wa Mungu zaidi ya vile tungeweza kumanya wenyewe. Kama yule kijana na gari lake, anaweza kufanya zaidi alo kama atalijaza mafuta!

**Shughuli**

(Unahitaji kuwaandaa watu wako wenye kujitolea kabla ya kufanya igizo hili.)

10 Dakika

Tunaenda kufanya mchezo wa kuigiza. Lengo la igizo hili ni kwa ajili yetu kuona kuwa Roho Mtakatifu anatuwezesha kufanya yale ambayo hatuwezi kufanya kwa uwezo wetu wenyewe. Inaumba pia nafasi kwa kikundi kumpa sifa Roho Mtakatifu.

Utahitaji kamba kwa ajili ya kuvuta kwa nguvu ya vita. (Kwenye kuvuta kwa nguvu ya vita timu 2 zitakuwa zikivuta kwa pande tofauti mwishoni mwa kamba)

Chukua watu 6 wenye kujitolea na uwagawanye kwenye timu 2. Unapaswa kuwaeleza kile unachokitaka wafanye kabla ya kuanza shughuli hii. Wenye kujitolea ndiyo kama waigizaji!

Timu ya 1 inaitwa ‘Tuna nguvu’. Waambie waje mbele na wakati wanakuja sifia uwezo wao. Tayari wana uhakika wa ushindi mvuto wa vita ya kamba kwa sababu ya uwezo ultimo ndani yao. Wanaendelea kujiita jina lao wakali.

Timu ya 2 inaitwa ‘Nguvu ya Roho.’ Waambie wake mbele wakionekana hawana uhakika wao wenyewe, wakijua uwezo wa time nyingine na hata ingawa walijua walitumia muda mwingi wakifanya mazoezi. Wanalitaja jina lao lakini siyo kwa ukali.

Timu hizo mbili zinaenda kuvuta kamba ya vita kwa nguvu. Mshindi kamili ataamuliwa baada raundi tatu bora.

**Raundi 1:** Andaa timu kuanza kuvuta kamba kwa haarka sana. Timu 2, ‘Nguvu ya Roho’ ikashindwa. Timu 1, ‘Tuna Nguvu’ wakatamba juu ya uwezo wao na mafanikio yao yote. Walisema maneno kuwa, “Kamwe hamtatushinda. Hata mnapaswa kujisalimisha sasa.”

Kiongozi wa ‘Nguvu ya Roho’ aliwapa timu yake maneno ya kuwahimarisha, akisema maneno kama haya, “Tunapaswa kufanya bora zaidi, hatutakubali kushindwa. Hatufanyi haya kwa nafsi zetu zenyewe. Lazima tuvute kwa nguvu. Mungu atatusaidia.”

**Raundi ya 2:** Wanachama wa ‘Nguvu ya Roho’ wakapata kusudi jipya na ahadi. Waliinamisha vichwa vyao na kufanya maombi ya haraka kabla ya kushika kamba. Wakavuta mara ya pili na kwa mshangao wa kila mtu ‘Nguvu ya Roho’ iikashinda ‘Tuna Nguvu’.

Kiongozi wa ‘Nguvu ya Roho’ akaipa timu yake tena maneno ya kutia moyo. Wanatimu wa timu ya ‘Tuna Nguvu’ wakaonekana kuchanganyikiwa na kuvunjika moyo.

**Raundi ya 3:** Wanatimu wa timu ya ‘Nguvu ya Roho’ waliomba tena na wakati huu pia walishinda mchezo wa kamba haraka sana.

Wale wote waliokuwa wakitazama wakawashangilia sana. Tia moyo kikundi chote kushangilia ‘Nguvu ya Roho.’

**Maombi**

10 Dakika

Waambie kikundi kugawanyika kwenye kikundi watu cha 3 au 4.

Watie moyo kuombeana, wakimwomba Roho Mtakatifu kuwajaza na kuwasaidia waweze kuishi kwa uweza wake.

Funga muda wa maombi kwa kuomba maombi haya kwenye kikundi chote.

> *Bwana wetu,*
> *Tunataka kukutumikia. Tunataka kukupendeza.*
> *Tujaze sisi na Roho wako Mtakatifu. Tujaze kila siku..*
> *Amina.*

**Kufanya Wiki Hii**

Kila wiki kuna kazi ya nyumbani ya kufanya. Uwe na muda kila siku wiki hii kuweto kwenye uweppo wa Mungu. Mwombe akujaze na Roho wake Mtakatifu tena, na kukuongoza na kukoenyesha namna ya kuzidi kufanana naye. Waambie kikundi chako cha Misingi juu ya ujuzi wako wiki ijayo.

**Shahidi**

Mitume walibadilishwa kama matokeo yake kujazwa Roho Mtakatifu. Wakati umejazwa, fikiri juu ya hayo maeneo kwenye maisha yako ambayo inatakiwa mabadiliko na uweke hayo mabadiliko kwenye utendaji. Waonyeshe watu wanaokuzunguka kwa matendo yako na tabia yako namna Roho Mtakatifu anavyokubadilisha.

# Kumbukumbu

3

# Tumeumbwa kwa Sura ya Mungu



'Nasi sote, tukiwa na nyuso zisizotiwa utaji tunadhihirisha utukufu wa Bwana, kama kwenye kioo. Nasi tunabadilishwa ili tufanane naye, toka utukufu hadi utukufu my zaidi, utokao kwa Bwana, ambaye ndiye Roho.'
2 Wakorintho 3:18

**Maandalizi**

Uwe na:

- Mwambie mtu kwenye kikundi kusoma hadithi?
- Mwambie mtu kwenye kikundi asome kifungu cha Biblia?

**Karibu na Marejesho**

5 Dakika

- Mshukuru kila moja kwa kuja kwenye kwenye kikundi.
- Anza na maombi mafupi.
- Waulize kikundi kama wamefanya ‘Kufanya wiki hii’ na ‘Shahidi’ kazi ya wiki iliyopita.
- Waalike watu washuhudie kitu chochote walichojifunza au kuwa na ujuzi kwa kufanya kazi hizi.

**Lengo**

Lengo la kipindi wiki hii ni kufahamu kuwa kila moja wetu ameumbwa kwa sura ya Mungu. Hata hivyo, sura hii emeumbuliwa ndani yetu, na itaweza tu kurejeshwa tunapopokea na kukua ndani ya maisha yetu mapya. Yesu ndiye sura halisi ya Mungu, na Roho hutubadilisha siku kwa siku hadi kwenye sura ya Yesu.

**Kifungu cha Kukumbuka**

5 Dakika

Soma kifungu cha kukumbuka na nukuu za Biblia kwa sauti kwenye kikundi. Rudia kusoma tena kwa vifungu vidogo, waachie kikundi kurudia kila sehemu baada yako. Polepole soma tena kwa sehemu ndefu huku kikundi kikirudia kiła neno mpaka kiła moja atakapoweza kukariri kifungu chote. Watie baadhi watu moyo kujaribu na kurudia wao wenyewe.

> *Nasi sote, tukiwa na nyuso zisizotiwa utaji tunadhihirisha utukufu wa Bwana, kama kwenye kioo. Nasi tunabadilishwa ili tufanane naye, toka utukufu hadi utukufu my zaidi, utokao kwa Bwana, ambaye ndiye Roho.*
>
> *2 Wakorintho 3:18*

**Hadithi**

Wasomee kikundi hadithi inayofuata:

Ilikuwa ni siku ya mng'aro, na bado, ilikuwa ni siku ya joto. Happy alikuwa na furaha kwa vile haikuwa nyakati za mvua alipokuwa akitembea njiani. Alitoka nyumbani siyo muda mrefu baada ya kukucha akijua kuwa mda siyo mrefu kutakuwepo na jua kali kabla ya kufika kule alikokuwa akienda. Ni siku ya joto sana siku ambayo hawezi kusahau, hivyo alibeba chupa kadhaa za maji, na sasa tayari zilikuwa tupu. Alifurahia kuona miti zimezunguka bwawa iliyojulikana kuwa na maji safi ya kunywa. Zaidi ya kutuliza kiu yake hapa, angeweza pia kujaza machupa yake maji na alitegemea kuwa hizo zitamtosha hadi mwisho wa safari yake.

Happy alipofikia mimi, alishukuru kwa kivuli. Mwishoni mwa ukingo wa maji aliinama ili awes kunywa maji. Ghafla aliacha na kuanza kwa kushangazwa, na kustaajabishwa kile alichokiona. Aliiona hakisi ya sura yake huko nyuma, lakini siyo kwa uwazi namna hii. Siyo to kwamba ilikuwa wazi, ilikuwa kali na rangi zilikuwa za mng'ao kwa kweli. Kwa kawaida upepo husababisha mawimbi na kuvuruga maji au watu au wanyama wakitibua uso wa maji, wakichafua uakisi wowote kiasi cha kwamba wachache hawawezi kutambua kile wanachokiona. Kwa leo hakukuwepo na upepo wala wimbi, walą watu au wanyama waliokuwa wakinywa maji kutoka kwenye bwawa. Mwanga kwenye eneo alilokuwepo Happy akiinama kunywa maji ulitoa kivuli halisi ya sura yake. Hajawahi kujiona namna hii kwenye kioo au kwenye chuma kilichong'arishwa sana, alishangazwa kujiona kwa uwazi jinsi ambavyo angeweza kuwaona watu wengine.

Huku akitazama uwakisi wa kivuli ya sura yake halisi Happy hakuweza kujizuiya tabasamu lililotoka kwenye uso wake – na ilivyofanya, uakisi wa kivuli ya sura yake ilimchekea pia. Kilichofuata alikonyeza na uakisi wa kivuli ya sura yake ikanakili hivyo. Happy akapunga mkono, na kivuli yake ikafanya hivyo. Akatazama kushoto, halafu kulia nayo ikarudia. Akapiga makofi, na ingawa kivuli chake kivuli chake kilirudia Happy akatulia,

ingawa kwa muda halafu akapiga tena. Alionekana kuchanganyikiwa. Alipopiga makofi mikono yake ilitoa sauti – lakini wakati akisi ya kivili ya sura yake ilipopiga makofi haikutoa sauti. Kilichofuata Happy alitazama moja kwa moja kwenye kivuli chake na kusema ‘Hallo’. Uakisi wa kivili chake ulimtazama moja kwa moja, mdomo wake ukiwa wazi, midomo yake kama inasema neno, lakini zilibaki kimya.

Happy akakaa na kuwaza kwa muda. Akatambua kuwa ingawa uakisi wa kivuli chake ilimfanana na kunakili mwendo wake, hakuwa kama hicho kivuli. Haikuwa na uwezo wa kutoa sauti. Haikuweza kufanya vitu huru kwa kujitegemea. Alimfanana, lakini kwa namna nyingi alipungua kuliko yeye. Hapo tena akahisi upepo kwenye uso wake na akaona kiwimbi juu ya uso wa maji. Ng’ombe wengi wakaja kuelekea bwawani kunywa maji. Sasa uakisi wa kivuli chake haikuwa kali tena na kung’ara, lakini ikabadilisha umbo na kufifia. Happy alisimama kuendelea na safari yake na swali moja kwenye kichwa chake – je ataweza tena kuona uakisi wa kivuli ya sura yake ang’avu wazi tena?

**Kujifunza Biblia**

Soma 2 Wakorintho 3:12-18 kwenye kikundi:

> [12]*Kwa hiyo, kwa kuwa tunalo tumaini hili, tuna ujasiri sana.*
> [13]*Sisi si kama Mose, ambaye ilimpasa kuweka utaji ili*
> *kufunika uso wake ili Waisraeli wasiuone ule mng’ao*
> *uliokuwa juu yake hadi ulipofifia na hatimaye kutoweka.*
> [14]*Lakini akili zao zilipumbazwa, kwa maana mpaka leo utaji*
> *ule ule hufunika wakati Agano la Kale linasomwa. Huo utaji*
> *haujaondolewa, kwa maana ni katika Kristo peke yake*
> *unaondolewa.* [15]*Hata leo Sheria ya Mose inaposomwa, utaji*
> *hufunika mioyo yao.* [16]*Lakini wakati wowote mtu*
> *anapomgeukia Bwana, utaji unaondolewa.* [17]*Basi Bwana*
> *ndiye Roho. Mahali alipo Roho wa Bwana hapo pana uhuru.*
> [18]*Nasi sote, tukiwa na nyuso zisizotiwa utaji tunadhihirisha*
> *utukufu wa Bwana, kama kwenye kioo. Nasi tunabadilishwa*

*ili tufanane naye, toka utukufu hadi utukufu mkuu zaidi, utokao kwa Bwana, ambaye ndiye Roho.*

Kifungu chetu kinatueleza kuwa tumebadilishwa kuwa na sura ya Mungu. Leo, sura huchukua muundo tofauti. Kwa wakati mwingine zilikuwa labda michoro, picha za rangi, au sanaa ya mbao au sanaa za mawe. Leo hii tunazo picha na aina nyingi za sura zinazotembea. Hivi vyote vilivyonavyo kwa pamoja ni kwamba zinafanana na mtu fulani au kitu fulani, ingawa haina sifa kamili ya mtu huyo au kitu. Kwenye hadithi Happy aligundua kuwa kivuli kilimfanana, lakini siyo kamili kama yeye alivyo. Kutengenezwa kwa sura ya mtu mwingine maana yake ni kufanana naye, lakini tuanapozungumzia kutengenezwa ili kufanana na Mungu ni zaidi ya kutazama tu, ina maana kuwa tulitengenezwa *ili* kufanana naye pia.

5 Dakika

**Shughuli**

Waambie kikundi kujigawanya kuwa wawili pamoja. Wanapaswa kusimama na kutazamana. Mmoja wao awe mwigizaji na mwngine awe ni kioo.

Mwambie mwigizaji aanzishe matendo fulani (hii inaweza kuwa kitu makini au kibaya jinsi unavyopenda) wakati kioo ikinakili akijaribu kuwa kama sura yao. Baada ya muda waambie wabadilishane na kujaribu teana.

Siyo jambo rahisi kuwa sura ya mtu mwingine! Tanapaswa kushiriki hasa kwao na kufuata yale wanayoyafanya.

Kuelewa maana ya kutengenezwa kwa sura ya Mungu, itasaidia tukianza kuanzia mwanzo wa Biblia. Kwenye kitabu cha kwanza cha Biblia, Mwanzo 1:26 tunasoma kuwa siku ya sita ya uumbaji Mungu akasema, “Na tumfanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu.” Mwanzo 1:27 hapa tunasoma pia, ‘kwa mfano wa Mungu alimwumba; mwanamume na mwanamke aliwaumba.’ Tulitengenezwa kufanana na Mungu.

Hivyo Adamu na Eva, mwanamume na mwanamke wa kwanza, waliumbwa kwa sura ya Mungu walikuwa kama Mungu kwa namna nyingi lakini pamoja na hayo yote hawakuwa sawa na yeye. Mfano mmoja ni mapenzi huru, au uchaguzi. Mungu asingelimwonya Adamu kinyume na kula matunda ya mti fulani kama asingempa uhuru wa kuchagua kama atakula au hatakula. Lakini hata ingawa walikuwa na mapenzi huru, uwezo wa kuchagua ulikuwa na kiwango kwa njia nyingi kwa sababu hawakuwa na ufahamu wa matokeo ya uchaguzi wao. Kinyume na haya, Mungu hana kiwango ya mapenzi huru kwa sababu yeye ni mwenye enzi kwa mambo yote.

Ni kwa sababu wlifahamu kuwa walifanana na Mungu lakini wakiwa na upungufu kuliko yeye, kwa Shetani aliweza kumdanganya Eva. Uongo wa Shetani ulikuwa upi (Mwanzo 3:5)? Siyo kwamba kwenye kula kwa ule mti uliyokatazwa watajua mema na mabaya, lakini hiyo faida kama akili ingewafanya wao kuwa ‘kama Mungu’. Baada ya mke wake kula tunda, Adamu alikabiliwa na uchaguzi wa kufanya jambo hilo au kumpoteza mkewe. Baada ya kula, wote wakagundua kuwa wako uchi, lakini angalia – hawakujua la kufanya kwa jambo hilo. Hawakufanana na Mungu. Ingawa walipata ujuzi wa mema na mabaya, hawakuwa na hekima ya kutosha kutumia ujuzi sawasawa. Walibaki kupungukiwa kuwa sawa na Mungu.

Wakichanganyikiwa na kusikia hukumu, wakajificha mbele ya Muumbaji wao. Hata hivyo, Mungu alijiandaa kwa siku hii. Aliwaambia kutokuamini kwao kumeleta shida juu yao, ilivunja ile sura yake mwenyewe aliyoweka ndani yao, kama chombo cha udongo au bakuli iliyovunjwa vunjwa vipande vipande. Hata aliwaambia wao alikuwa na mpango wa kuwaokoa wao kutokana na makosa yao wenyewe, kutengeneza na kurejesha kile kilichvunjwa. Mpango huu ulikuwa ni wa kumtuma Mwanaye, Yesu.

Kwenye barua yake kwa Wakolosai Paulo anasema Yesu ni, ‘sura ya Mungu asiyeonekana’ (Wakolosai 1:15). Ndani ya Yesu, sura

ambayo Mungu ameumba kwa watu imerejeshwa, kupitia Yesu na kazi ya Roho wake Mtakatifu ndani yetu, sura hiyo inaweza kurejeshwa ndani ya kila moja wetu pia. Tunakuwa hai tukimwakilisha Mungu hapa duniani, sehemu ya mwili wake ambao wengine wanaweza kuona na kupata ujuzi.

Kifungu cha kukumbuka kinazungumzia juu ya kazi ya Roho Mtakatifu kuwarejesha watu kwenye sura ya Mungu. Paulo aliandika juu ya Musa uso wake kung'ara kwa mwanga mkali baada ya kukutana na Mungu juu ya Mlima Sinai ambayo watu walimwambia afunike. (Unaweza kusoma jambo hilo kwenye kitabu cha Kutoka 34:28-35.) Paulo alimfananisha Musa kukutana na Mungu na Wakristo kuwa na uhusiano na Mungu wanapoingia kwenye kuamini. Ni kupitia Roho Mtakatifu ndiyo tunatunza uhusiano wetu na Mungu Baba. Paulo anasema kuwa tuko kama kioo inayokusudiwa kuonyesha utukufu wa Mungu. Ni kazi ya Roho Mtakatifu kuturejeza sisi, hatua moja kwa wakati, kwenye sura ya Mungu ambayo haikuaribiwa.

Picha ya Agano la Kale inayofanana ni Mungu kama msafishaji wa dhahabu na fedha; angalia kwa mfano Zaburi 66:10 na Malaki 3:2-3. Kwa wakati huo wasafisha chuma waliweza kukaa wakivumilia wakitazama chungu yenye chuma ya moto sana iliyoyeyushwa wakitazama chembechembe zikielea juu. Wakati haya yanatokea, msafishaji huchota nje na kusubiri zingine zielee juu ya uso wa chungu. Ni mpaka tu pale atakapoona kutobdilika sura yake ikiendelea kwenye chuma iliyoyeyuka atajua kuwa kazi yake imekamilika. Hii inatoa kielelezo ya kazi ya Roho Mtakatifu kwenye maisha yetu. Kazi yake itakamilishwa tu atakapoona ndani yetu sura ya kweli ya Yesu Kristo.

?
5
Dakika

**Maswali**

Kifungu cha leo inatufundisha kuwa tumeumbwa kwa sura ya Mungu, na anafanya kazi kurudisha hiyo sura ndani yetu. Hata hivyo ikiwa tutakuwa kama yeye ni vema kufahamu kwanza kama yeye anafananaje. Kwenye kikundi cha watu 3 au 4, waambie

wanachama wa kikundi kila moja kushirikisha mawazo fulani ya kusema Mungu anafananaje.

Waambie basi wajadiliane yale ambayo Yesu aliwaonyesha kuhusu Mungu ambayo haijajulikana kwetu.

**Maombi**

10 Dakika

Soma maombi yafuatayo toka Zaburi 139:23-24:

> 23 *Ee Mungu, nichunguze, uujue moyo wangu,*
> *nijaribu na ujue mawazo yangu.*
> 24 *Uone kama kuna njia iletayo machukizo ndani yangu,*
> *uniongoze katika njia ya milele.*

Mwambie kila mtu akae kimya kwa dakika kadhaa na kufikiri kuwa hii ina maana gani. Soma Zaburi 139:23 – 24 tena.

Baada ya dakika kadhaa waambie watu waombe kwenye vikundi vidogo wao wenyewe na moja kwa mwingine kwa mstari huo huo. Kama unafahamu kifungu kingine kinachozungumzia juu ya kusafishwa na Roho Mtakatifu, jumlisha haya kwenye maombi yako.

**Kufanya Wiki Hii**

Wiki hii, kutana na mtu mwingine kwenye kikundi na kuzungumza juu ya njia zingine ambayo sura inaweza kuwa ya tofauti toka mtu wa asili au chombo. (Usifikiri tu juu ya uakisi wa kivuli, unaweza kufikiri juu ya picha au michoro kwa mfano.)

Halafu mfikiri njia zingine ambazo Adamu na Eva walikuwa kama Mungu walipoumbwa, lakini wawe wamepungua kuliko yeye. Kupitia dhambi ya Adamu na Eva watu walipambanua ujuzi wa mema na mabaya; hata hivyo wanakuwa wamepungua kuliko Muumbaji wao kwa namna nyingine. Mjadili tofauti hizi 2 au 3 ili muweze kuona madhara yake kwenye maisha yako mwenyewe.

Kwenye majadiliano yenu kumbuka kuwa Mungu hafurahishwi tu na mwonekano wa nje, hufurahia ndani ya mioyo yetu.




**Shahidi**
Kurejeshwa kwenye sura ya Mungu inaweza kuwa hatua yenye maumivu. Kwenye kitabu cha Yakobo 5:16 Biblia inatutia moyo kukiri dhambi zetu moja kwa mwingine na kuombeana. Zungumza na Wakristo wengine juu ya ujuzi wa kurejeshwa hatua kwa hatua kwenye sura ya Mungu. Watie moyo kwa kushirikisha furaha ya kutambua wakati kitu kimeshughulikiwa na Roho Mtakatifu. Waambie wakutie moyo kwa kuomba kuwa utamruhusu Mungu kukufanya kufanana na Yesu kwa namna unavyoishi kila siku.

Wiki hii nenda ufanye jambo fulani unalofikiri litasaidia kukuunda au kukurekebisha zaidi uwe na sura ya Mungu. Tazama hasa maeneo ya tabia ya Mungu au shughuli ambayo utaona ugumu kukabiliana nayo. Omba kwamba Roho Mtakatifu atafanya kazi ndani yako kukufanya ufanane naye.

# Kumbukumbu

# 4

# Tabia ya Mungu ni Upendo



'Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwanawe wa pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.'
Yohana 3:16

**Maandalizi**

Uwe na:

- Mwambie mtu kwenye kikundi kusoma hadithi?
- Mwambie mtu kwenye kikundi asome kifungu cha Biblia?

**Karibu na Marejesho**

5 Dakika

- Mshukuru kila moja kwa kuja kwenye kwenye kikundi.
- Anza na maombi mafupi.
- Waulize kikundi kama wamefanya ‘Kufanya wiki hii’ na ‘Shahidi’ kazi ya wiki iliyopita.
- Waalike watu washuhudie kitu chochote walichojifunza au kuwa na ujuzi kwa kufanya kazi hizi.

**Lengo**

Mungu ni pendo, ni namna ya pekee ya kuweza kumwelezea jinsi alivyo. Tunafahamu upendo wake kwetu wa aina nyingi. Alimtuma mwanaye kufa msalabani kwa ajili yetu. Tulipokuwa watumwa wa dhambi, Yesu alitufia. Alitupenda hata kabla sisi hatukumpenda yeye. Wafuasi wake wanatambuliwa kwa upendo huu pia, na hii ndiyo inakua kwetu kama sehemu ya maisha yetu mapya.

**Kifungu cha Kukumbuka**

5 Dakika

Soma kifungu cha kukumbuka na nukuu za Biblia kwa sauti kwenye kikundi. Rudia kusoma tena kwa vifungu vidogo, waachie kikundi kurudia kila sehemu baada yako. Polepole soma tena kwa sehemu ndefu huku kikundi kikirudia kiła neno mpaka kiła moja atakapoweza kukariri kifungu chote. Watie baadhi watu moyo kujaribu na kurudia wao wenyewe.

> *Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwanawe wa pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.*
>
> *Yohana 3:16*

**Hadithi**

Wasomee kikundi hadithi inayofuata:

Mwaka 1930 kule Amerika aliishi mtu aliyeitwa John Griffith. Alikuwa na mke na kijana mdogo na kazi yake ilikuwa kuongoza daraja ya kusukumaambayo iliruhusu train kuvuka mto Mississipi.

Siku moja John alimchukua kijana wake kufanya kazi pamoja naye kumwonyesha daraja na kumwambia juu ya treni inayosafiri kuvuka daraja hilo. Mtoto wake alipendezwa kuwa na baba yake kwa siku hiyo, akijifunza yote kuhusu kazi yake.

Baada ya kumwonyesha motto wake maeneo yote, John alisikia kama treni inakuja toka mbali na kutambua kuwa treni ya Memphis Express ilikuwa njiani. Alifanya haraka kurudi kwenye chumba cha kuongoza ambapo ndipo palipokuwa na vinyanyuzi vya kuongoza daraja, akimwacha motto wake na maelekezo ya kubaki mahali alipokuwa. Hata hivyo kijana wa John hakusikiliza na akajaribu kumfuata baba yake, akateleza na kuangia chombo ambacho ndicho kilichopaswa kuzunguka ili daraja iweze kufungwa.

John ghafla akagundua kilichotokea na akatazama chini kwa kitisho kumtazama motto wake, akikabiliwa na uamuzi wa kutisha. Hakuwa na muda wa kumwokoa mwanaye na kusukuma wenzo ina maana treni ingevuka salama, alipaswa kuchagua: maisha ya motto wake, au maisha ya wasafiri 400 waliokuwa ndani ya treni.

Kwa siku hiyo alifanya uchaguzi wa uchungu kuwezekana, alimtoa mtoto wake sadaka ili wali wasafiri waweze kuishi. Waliendelea na safari yao kamwe bila kujua yale ambayo John aliyapitia ili waweze kuishi.[3]

---

[3] Christian Research Institute (2010). *John Griffith, the Bridge Operator* [KWENYE MTANDAO] Inapatikana: www.equip.org/hank_speaks_out/john-griffith-the-bridge-operator/ [Imenakiliwa 12 January 2018]

**Kujifunza Biblia**

Soma 1 Yohana 3:16-18 kwa kikundi:

> *[16]Kwa namna hii twaweza kulijua pendo la Mungu: Kwa sababu Yesu Kristo aliutoa uhai wake kwa ajili yetu. Nasi imetupasa kuutoa uhai kwa ajili ya hao ndugu. [17]Ikiwa mtu anavyo vitu vya ulimwengu huu na akamwona ndugu yake ni mhitaji lakini asimhurumie, upendo wa Mungu wakaaje ndani ya mtu huyo? [18]Watoto wapendwa, tusipende kwa maneno au kwa ulimi bali kwa tendo na kweli.*

Upendo ni neno tunalolisikia kila mara. Unaweza kuwa ‘ndani ya upendo’, ukipendwa na familia yako au marafiki, unaweza kupenda timu fulani, aina ya nguo au hata chakula. Neno lina maana nyingi hivyo unapaswa kufahamu kidogo zaidi tuna maana gani tunapozungumzia upendo wa Mungu.

5 Dakika

**Shughuli – Habari Njema**

Kuna namna nyingi ya kuonyesha upendo wetu kwa watu wengine. Gawanya kikundi nusu na uwape changamoto kuonyesha kiasi cha upendo walionao kwa timu nyingine. Fikiri njia ambazo unaweza kuzungumza juu ya upendo na njia ambazo unaweza kudhihirisha upendo. Uwe mbunifu na ufurahie!

10 Dakika

**Maswali – Upendo wa Mungu ni nini?**

Pole pole soma 1 Wakorintho 13:4-7 kwenye kikundi:

> *[4]Upendo huvumilia, upendo hufadhili, upendo hauoni wivu, hauna majivuno, hauna kiburi. [5]Haukosi kuwa na adabu, hautafuti mambo yake, haukasiriki upesi, hauweki kumbukumbu ya mabaya. [6]Upendo haufurahii mabaya bali hufurahi pamoja na kweli. [7]Upendo huvumilia yote, huamini yote, hutumaini yote, hustahimili yote.*

Gawanya kikundi kwenye vikundi vidogo na mjadili maswali yafuatayo:

- Kifungu hiki kinatufundisha nini kuhusu upendo wa Mungu?
- Kuna ufafanuzi wa upendo ulioorodheshwa hapa inayokushangaza?
- Je kuna nyakati imekuwia vigumu kupenda namna hii? Ni zipi zilizo changamoto kwako?
- Unawezaje kupenda zaidi kama upendo wa Mungu?
- Kwenye kikundi chako rudia kusoma kifungu hiki ukifafanua neno upendo kwa jina lako mwenyewe.

**Upendo wa Kweli**

Kifungu hapo juu inazungumzia juu ya kupenda kwa matendo na kwa kweli, lakini upendo wa kweli ni upi? Wiki hii kifungu cha kukumbuka na hadithi vyote vinadhihirisha kuwa upendo wa Mungu kwetu sisi ni wa ndani kiasi cha kwamba alijiandaa kumtoa Mwanaye kuwa sadaka kwa ajili yetu. Hii ilidhihirishwa kwenye hadithi yetu wakati John Griffith alipaswa kupitisha uchaguzi wa kutisha kati ya maisha ya mwanaye aliyempenda sana, na maisha ya mamia ya wasafiri ndani ya treni ile.

Upendo wa Mungu ni wa tofauti na upendo tunaoonyesha kwa wale wanaotuzunguka. Kwa kawaida tunawapenda wale wanaotupenda: marafiki zetu, wanafamilia, mume, mke na watoto. Ni jambo la adimu kwetu kuwapenda wale wasiyojua hata kuwa sisi ni nani au kujali uwepo wetu lakini ukweli ni kwamba haya ndiyo Mungu alifanya kwa ajili yetu.

Wiki iliyopita tulitazama ukweli kuwa tumeumbwa na Mungu kwa sura yake; kila moja wetu ni wa kipekee na kila moja wetu anapendwa na Mungu. Ni kwa sababu ya upendo huu alimtuma mwanaye afe, ili tuweze kuwekwa huru kuwa na maisha mapya. Wengi wenu mmepokea maisha haya mapya na mmenza kugundua mabadiliko ndani yako kwa matokeo ya haya. Moja ya mabadiliko haya ni kwamba utaelewa kwa kina kuwa Mungu anakupenda namna gani, na ni kiasi gani anawapenda watu wengine pia.

**Upendo wa Matendo**

Upendo wa Mungu huzama ndani zaidi ya uelewa tu; ni jambo ambalo analidhihirisha na kulizungumzia pia. Yesu alipoulizwa na mwanafunzi wa sheria kuwa ni amri ipi iliyo kuu alisema:

> [37]*Yesu akamjibu, " 'Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote na kwa roho yako yote na kwa akili zako zote.'*
> [38]*Hii ndiyo amri iliyo kuu, tena ni ya kwanza.* [39]*Nayo ya pili ni kama hiyo, nayo ni hii: 'Mpende jirani yako kama nafsi yako.'*
>
> *Matayo 22:37-39*

Mungu anapenda tunapompenda: tuliumbwa tuwe na ukaribu wa uhusianao na yeye, ndiyo sababu tunapopokea maisha mapya tunapokea ufahamu wa upendo huu, na wakati mwingine tunapopata ujuzi wa hamu kubwa ya kutaka kupendwa kupitia ngavu za Roho Mtakatifu. Hatufanyi kumpenda yeye – tuko huru kuchagua – lakini anatutaka kumpenda yeye kwa moyo, kila sehemu ya uhai wetu, jinsi anavyotupenda sisi.

Lakini haiishii hapo. Namna ya kumpenda Mungu, anatutaka sisi kuendeleza upendo huu kwa hao wanaotuzunguka. Inafuata kama anampenda kila mtu, anawaambia wafuasi wake kumpenda kila mtu pia. Hii aina maana kuwa siku zote utawahitaji, au kile wanachokifanya, lakini hii ina maana kuwa utawatambua kwa dhamani ya upendo kwa hiyo itakufanya wewe kuwaombea na kuwahudumia kwa nidhamu.

Yesu alipata changamoto zaidi ya hii. Kwa wakati mwingine aliwaambia wafuasi wake:

> [43]*"Mmesikia kwamba ilinenwa, 'Mpende jirani yako na umchukie adui yako.'* [44]*Lakini ninawaambia: Wapendeni adui zenu na waombeeni wanaowatesa ninyi,*
>
> *Matayo 5:43-44*

Mungu anatutaka sisi kufuata mfano wake kutoka nje kuwapenda wale ambao wanapitia wakati mgumu na changamoto. Hii inahusiana na kuwaombea, na kutafuta njia ya kuonyesha upendo wa Mungu kwao. Hii haionekani kama kupenda kama ulimwengu unavyopenda lakini upendo wa Mungu ni wa matendo na wa kweli.

15 Dakika

## Maombi

Kuomba kwa neno la Mungu tukijiombea inakuwa na nguvu. 1 Wakorintho 13:4-7 tena kama maombi:

> **4** *Upendo huvumilia, upendo hufadhili, upendo hauoni wivu,*
> *hauna majivuno, hauna kiburi.* 5 *Haukosi kuwa na adabu,*
> *hautafuti mambo yake, haukasiriki upesi, hauweki*
> *kumbukumbu ya mabaya.* 6 *Upendo haufurahii mabaya bali*
> *hufurahi pamoja na kweli.* 7 *Upendo huvumilia yote, huamini*
> *yote, hutumaini yote, hustahimili yote.*

Mpatie kila mtu dakika kidogo kuomba kwa maneno yake mwenyewe, au wawili kama watataka hivyo.

Malizia kwa maombi yafutayo, ukimwacha kila moja arudie mstari baada yako.

> *Bwana, wiki hii nisaidie kupenda kama unavyopenda.*
> *Naomba kuwa utanisaidia kuwa mvumilivu na mkarimu,*
> *siyo kwa wivu, kujiinua au kujisifu.*
> *Nisaidie niwaheshimu wengine zaidi yangu, nisiwe mwenye*
> *hasira nisiwe na kumbukumbu ya makosa.*
> *Nisaidie nisitake mambo ya shetani lakini nifurahi na kweli.*
> *Nisaidie kulinda, kuamini, tumaini na uvumilivu.*
> *Amina.*

## Kufanya Wiki Hii

Yesu ametuambia tuwapende maadui na kuwaombea wale wanaotutesa. Huyu ni nani unayejiweka sawa na adui,

anayekutesa au kuyafanya maisha yako kuwa magumu? Hii inaweza kuwa ni watu unaowajua au watu wanaowakilisha utaratibu au mazingira inayofanya maisha yako kuwa magumu. Wiki uwe na muda wa kuwaombea kila siku. Mwombe Mungu ajifunue kwao. Mwombe akupe upendo zaidi kwa wale walio wagumu.

Wiki ijayo uwe na dakika chache kushuhudia kikundi jinsi unavyoendelea.



**Shahidi**

Jibidiishe kuonyesha upendo hasa kwa mtu ambaye kwa kawaida haumjali; hii inaweza kuwa na maana kuwaalika kujiunga nawe kwenye chakula, kuonyesha chochote cha huruma kwao, kuwachukua sehemu fulani au kuwasaidia kwenye kazi fulani. Unapoonyesha upendo wa Mungu kwa matendo na kuomba nafasi ya kuzungumza pia juu ya upendo wa kweli wa Mungu na namna unavyopatikana kwao kama watapokea zawadi yake ya maisha mapya.

5

# Tunda la Roho – Tabia



'Lakini tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole na kiasi. Katika mambo kama haya hakuna sheria.'

Wagalatia 5:22-23

**Maandalizi**

Uwe na:

- Mwambie mtu kwenye kikundi kusoma hadithi?
- Mwambie mtu kwenye kikundi asome kifungu cha Biblia?

**Karibu na Marejesho**

5 Dakika

- Mshukuru kila moja kwa kuja kwenye kwenye kikundi.
- Anza na maombi mafupi.
- Waulize kikundi kama wamefanya ‘Kufanya wiki hii’ na ‘Shahidi’ kazi ya wiki iliyopita.
- Waalike watu washuhudie kitu chochote walichojifunza au kuwa na ujuzi kwa kufanya kazi hizi.

**Lengo**

Lengo wiki hii ni kuelewa kwamba tunapojazwa na Roho Mtakatifu, anafanya kazi kuleta matunda kwenye maisha yetu. Kuna matunda ya kiroho, kama ukarimu, furaha na uaminifu na wanawakilisha tabia ya Yesu inayokua ndani yetu.

**Kifungu cha Kukumbuka**

5 Dakika

Soma kifungu cha kukumbuka na nukuu za Biblia kwa sauti kwenye kikundi. Rudia kusoma tena kwa vifungu vidogo, waachie kikundi kurudia kila sehemu baada yako. Polepole soma tena kwa sehemu ndefu huku kikundi kikirudia kiła neno mpaka kiła moja atakapoweza kukariri kifungu chote. Watie baadhi watu moyo kujaribu na kurudia wao wenyewe.

> *22 Lakini tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, 23 upole na kiasi. Katika mambo kama haya hakuna sheria.*
>
> *Wagalatia 5:22-23*

**Hadithi**

Wasomee kikundi hadithi inayofuata:

Tawi juu ya mti kwa wazi ulitaka kutoa matunda. Tawi lilijaribu kwa nguvu kutoa matunda, lakini haijalishi ni kwa kiasi gani ulijaribu, hakuna kilichotokea. Ilijaribu kwa nguvu. Ilijaribu kwa nguvu zaidi, lakini hakuna matunda yaliyokua.

Tawi lilikaribia kukata tamaa wakati iliposikia sauti ya mti ukimnong'oneza, 'Ngoja mimi nifanye.' Tawi liliacha kung'ang'ana, kusukuma na kuvuta ukamwamini mti kuzalisha matunda badala yake. Kwa mshangao, matunda yakaanza kujitokeza. Siyo kidogo tu bali ni mengi.[4]

Niliposikia hadithi hii ikanifanya kufikiri juu ya maisha yangu. Kama tawi kwenye hadithi, nimekuwa nikijaribu kukuza matunda ya Roho Mtakatifu mwenyewe, nilidhani ilikuwa ni kufanya tabia yangu na mwonekano badala ya kufanya na mwenye kutoa.

Mara nyingi nilifikiri, 'Ikiwa nitajaribu kwa nguvu.' Nilijaribu kwa nguvu sana. Mimi ni mtu ninayesukumwa na asili yangu. Nilitaka hasa kusema, 'Matunda ndiyo haya; angalia, nafanya haya sawa!' Lakini kuna vitu ambavyo hatuwezi kufanya wenyewe, haijalishi tutajaribu kwa kiasi gani.

Ikiwa niko kama tawi, Yesu ndiyo kama mti. Anatunong'oneza, 'Ngoja mimi nifanye. Mwache Roho Mtakatifu afanye kazi ndani yako.' Matunda yanayokuwa haituhusu sisi, ni Roho Mtakatifu ndiye afanyae kazi ndani yetu kutufanya kufanana na Yesu, tabia yake na asili yake.

Kitu cha ajabu ni kuwa pamoja na upungufu wetu, tukiweka imani yetu katika Yesu na kutambua uhitaji wa kumwitaji yeye, buni nini kitatokea? Tunaenda kuanza kuelewa nini maana ya kuunganishwa na mti. Tunajikuta wenyewe tukivuta maisha toka

---

[4] Lost Sheep (undated). *Basil the Branch* [KWENYE MTANDAO] Inapatikana: www.lostsheep.com.au/stories/basil-the-branch/ [Imenakiliwa 12 January 2018]

kwenye mti na mahali ambapo hakukua na kitu, ghafla matunda yanatokea ambayo itampa Yesu utukufu.

**Kujifunza Biblia**

Kwenye kitabu cha Yohana 15, Yesu alitumia mfano kama huo wa tawi na mti. Alitumia mfano wa mzabibu na matawi iliyounganishwa nayo. Alieleza kuwa yeye ni mzabibu na sisi ni matawi. Aliweka wazi kuwa sisi wenyewe hatuwezi kufanya jambo lolote, lakini tukibaki ndani yake tutazaa matunda. Tunapojazwa na Roho Mtakatifu tunaunganishwa na mzabibu, na ushahidi wa muunganiko huu ni matunda yanayoanza kuzalishwa ndani ya maisha yetu. Tulivyoona hapo juu, matunda haya yanajumlisha utu wema, upole na furaha. Ni tabia ambazo haziji kwetu kwa njia ya asili, lakini Mungu anataka kukuza ndani yetu hata hivyo.

Mungu anataka kuonyesha maisha yake kupitia sisi kwa matunda tunayozaa. Tunapotambua mahitaji yetu ya kuunganishwa na Yesu, Roho Mtakatifu anakuwa na uhuru kudhihirisha maisha haya ndani yetu kwa njia ya matunda ambayo yanakuwa dhahiri kwa wote kuona kwenye maisha yetu.

**Maswali**

Kwenye kikundi cha 3 au 4 jadili maswali yafuatayo:

10 Dakika

- Tutasaidiaje miti au mazao kuzaa matunda?
  Jibu linaweza kuwa wapatie chakula/maji, wapunguze, walinde na wadudu au wanyama wengine, hakikisha wana mwanga/joto la kutosha.
- Nini itatuzuiya kuzaa matunda?
  Jibu litajumlisha dhambi ndani ya maisha yetu, kukataa kubadilika, kukosa chakula cha kiroho/maji, kukosa kuwa na adabu.
- Tutafanya nini tuweze kuwa na ushirika na Roho Mtakatifu ili kuweza kuzaa matunda?

Jibu linaweza kujumlisha maombi, kufaidi chakula cha kiroho kupitia kusoma Biblia, na kuwa na muda na waamini wenzako.

Soma Wagalatia 5:16-26 kwenye kikundi:

*[16]Kwa hiyo nasema, enendeni kwa Roho, wala hamtazitimiza*
*kamwe tamaa za mwili. [17]Kwa maana mwili hutamani yale*
*yaliyo kinyume na Roho, naye Roho hutamani yale yaliyo*
*kinyume na mwili. Roho na mwili hupingana na kwa sababu*
*hiyo hamwezi kufanya mnayotaka. [18]Lakini kama*
*mkiongozwa na Roho, hamko chini ya sheria.*

*[19]Basi matendo ya mwili ni dhahiri nayo ni haya: Uasherati,*
*uchafu, ufisadi, [20]kuabudu sanamu, uchawi, uadui, ugomvi,*
*wivu, hasira, fitina, faraka, uzushi, [21]husuda, ulevi, ulafi na*
*mambo mengine yanayofanana na hayo. Nawaonya, kama*
*nilivyokwisha kuwaonya kabla, kwamba watu watendao*
*mambo kama hayo, hawataurithi Ufalme wa Mungu.*

*[22]Lakini tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu,*
*utu wema, fadhili, uaminifu, [23]upole na kiasi. Katika mambo*
*kama haya hakuna sheria. [24]Wote walio wa Kristo Yesu*
*wameusulubisha mwili na shauku zake pamoja na tamaa*
*zake.*

*[25]Kwa kuwa tunaishi kwa Roho, basi, tuenende kwa Roho.*
*[26]Tusijisifu bure, tukichokozana na kuoneana wivu.*

*Wagalatia 5:16-26*

Kwenye kifungu chetu cha kukumbuka toka barua ya Paulo kwa Wagalatia, Paulo alisisitiza juu ya matunda tutakayozaa; ‘upendo usiyokuwa wa sababu, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole na kiasi.’ Ni kweli kusema kila moja anaweza kuonyesha baadhi ya matunda au yote ndiyo sababu kama wanamjua Yesu au hapana kwa sababu wote tuliumbwa kwa sura ya Mungu. Lakini, ikiwa tumeunganishwa kamili kwenye

mzabibu – Yesu – inawezekana kwa Mungu kudhihirisha matunda kwa uwingi na kwa kina kupitia sisi kwa nguvu ya Roho Mtakatifu. Tunakuwaje wakati Yesu hayuko na sisi tunafifia kwenye kivuli ya ulinganishi. Hata kama tutatunza kila sheria na amri hatutaweza kuzalisha matunnda mengi bora ambayo Roho Mtakatifu anaweza kuzalisha kupitia sisi.

Kama tumeunganishwa na Yesu, mzabibu, na maisha yake inabubujika kupitia sisi, inafanya maana kamili kufikiri kuwa tabia hizi ambazo Yesu amedhihirisha kama ametembea kati yetu itakuwa ni ushahidi kupitia maisha yetu.

Kawaida ya tabia hizi siyo kwa ajili ya faida yetu wenyewe; Mungu huzitumia kwa kusudi lake. Yohana 15:16 Yesu alisema:

> *Si ninyi mlionichagua, bali mimi ndiye niliyewachagua ninyi na kuwaweka mwende mkazae matunda, na matunda yenu yapate kudumu. Ili nalo lolote mtakalomwomba Baba katika Jina langu, awape ninyi.*

Hapa Yesu hazungumzi moja kwa moja juu ya matunda ya Roho lakini anachokizungumzia ni matokeo ya wazi ya matunda kuwa ushahidi kwa wote kuona.

Uliwahi kusikia ikisemwa, ama kusema mwenyewe, “Nini imenivuta kwa mtu huyu binafsi ama kikundi hiki ilikuwa ni upendo ama furaha ama amani iliyodhihirishwa?” Au uliwahi kumfahamu mtu aliyempenda Yesu, anaeonekana kuendelea kutembea wakati watu wengine wamesema ni ngumu sana ama siyo rahisi? Au uliwahi kukutana na mtu, pamoja na kuonekana siyo rahisi kwao, wameweza kudhihirisha utu wema kwa wengine? Au unamfahamu mtu fulani ambaye hatingishiki mbele ya uso wa upinzani? Tunachozungumzia ni kitu kinachobubujika kupitia kwa Yesu kuja kwetu na kupitia kwetu na kuleta uvuvio kwa watu wanaotuzunguka.

Tazama nyuma kwenye kifungu cha Wagalatia. Mstari 24 inatusaidia kuelewa jambo hili zaidi. Kwetu sisi kuzaa matunda ya Roho Mtakatifu ni lazima tuwe wa Yesu. Hii ina maana kuwa sisi siyo mali yetu tena wenyewe, hatuishi tena kwa nafsi yetu wenyewe na matamanio yetu yanayoitwa 'mwili' kwenye mstari. Huu umesulubishwa (kuingizwa kwenye kifo) pamoja na Yesu na Yesu aliyefufuka sasa anaishi ndani yetu. Kwa maneno mengine, kuzaa matunda, tayari tumetambua na kuruhusu hisia kali na matamanio kuangikwa msalabani.

Tunaishi maisha haya mapya kwa imani ndani ya Yesu. Matunda hukua tunaporuhusu kukabidhi mapenzi yetu kwake.

Kwenye kitabu cha Luka 22:42, kabla hajaenda kufa, Yesu aliomba:

> *"Baba, kama ni mapenzi yako, niondolee kikombe hiki. Lakini si kama nipendavyo, bali mapenzi yako yatendeke."*

Yesu alidhirisha uvumilivu wake maana ya kujitoa na kujikabidhi. Uliwahi kusema nimekuwa na nguvu ya kufanya hili? Nguvu zetu wenyewe haziwezi kutosha; tutafikia mwisho wake. Lakini tunajua kuwa tunaweza kufanya mambo yote tunapotegemea nguvu za Yesu. Kama Paulo alivyoandika kwenye barua yake kwa Wafilipi. Kwenye Wafilipi 4:13 alisema:

> *Naweza kuyafanya mambo yote katika yeye anitiaye nguvu.*

Kwenye mstari wa 25 na 26 Paulo anachora mstari kwa kile kilicho cha muhimu hapa. Kama tutaenda kuzaa matunda ya Roho tusisahau chanzo. Ni vema kuwa karibu na Roho na kulea uhusiano wetu na yeye.

**Shughuli**
Waulize kikundi kama wanakumbuka kifungu cha kukumbuka wiki hii? Waambie wakariri tena.

3 Dakika

Waeleze kuwa tunda hili ni bora na inamwezesha mwamini kumpenda na kumtumikia mwingine na kufikia nje na kuwagusa wale wanaowazunguka ambao bado hawajafikia ujuzi wa zawadi ya maisha mapya.

10 Dakika

**Maswali**

Kwenye kikundi cha 3 au 4 waambie kikundi kuangalia Wagalatia 5:19-21. Kifungu hiki kinataja matunda ya mwili (matamanio yetu). Kiambie kikundi:

- Wamegundua tofauti gani juu ya aina ya matunda?
- Matokeo ya matunda ni yapi?

Kiambie kikundi kukariri kifungu cha kukumbuka tena. Kifungu hiki kinataja matunda ya Roho.

- Nini matokeo ya matunda ya Roho?
- Je matokeo ni sawa au tofauti?

Unatafuta majibu zitakazoonyesha matunda ya mwili zinaongoza kwenye huzuni na kupoteza. Matunda ya Roho yanazaa na kuongoza kwenye matokeo chanya.

Uchaguzi ni wetu, kutiwa moyo iko wazi. Kifungu ambacho tumekuwa tukijifunza kuanza kwa Paulo akisema, 'Haya ni maelekezo yangu: tembea katika Roho, na kuongozwa na Roho italeta utaratibu kwenye maisha.' Kila moja wetu achague kuishi kwa ukali akiunganishwa kwenye mzabibu, Yesu.

10 Dakika

**Shughuli**

Wakati mwingine ni vigumu kwetu kuona matunda kwenye maisha yetu.

Waambie kikundi kujigawanya kwenye kikundi cha 2 au 3. Watu ni lazima wawe na wengine wanaowafahamu au wamewajua kwa muda.

Waambie kila moja kushuhudia mifano ya ni lini wameona matunda ya Roho kwa maisha ya wengine. Ni muhimu kuwa tutakuwa wakarimu na wakweli tunapoyafanya haya. Ni nafasi nzuri kuwatia moyo wengine na kuwasaidia kumwona Yesu ndani yetu.

Waruhusu watu kufanya haya kwa dakika 5 au 10.

15 Dakika

**Maombi**

Kufuatilia shughuli, waulize watu kumshukuru Mungu kwa kila mfano iliyoshuhudia kwenye kikundi. Halafu waulize kuombeana kwenye kikundi kwa majina yabaki kwa Yesu, wamejazwa Roho Mtakatifu na matunda zaidi yakue.

**Kufanya Wiki Hii**

Kila siku wiki hii rudia kifungu cha kukumbuka kitu cha kwanza asubuhi na jambo la mwisho jioni. Unaporudia jioni kwa yale ya asubuhi, mwombe Roho Mtakatifu kukuonyesha ni matunda gani unayo (au haijaonyweshwa) siku hiyo.

Omba tena siku ya pili asubuhi kwamba Mungu akuze kila tunda ndani yako ili uweze kuwa nafasi kushuhudia njia ambazo unakua ndani ya maisha yako mapya ndani yake.

**Shahidi**

Chukua moja ya matunda ya Roho wiki hii; tazama moja kwamba uweze kuwa na ujanja wa asili (inaweza kuwa kiasi, utu wema, uaminifu?). Nenda njia yako kutafuta nafasi mahali ambapo unaweza kufanya mazoezi ukitumia na kukua katika zawadi.

Labda unaweza kuwa mkarimu kwa mtu fulani kwenye jumuiya yako ambaye ni vigumu kumpenda. Labda unaweza ukatoa kitu ambacho unakipenda mwenyewe kwa yule ambaye amepungukiwa zaidi yako.

Omba kwamba kupitia matendo haya utakuwa na nafasi kushuhudia kwa yule mtu ambaye umemchagua kumbariki kwa nini unafanya hivyo, na namna nao wanaweza kupokea maisha mapya ambayo unayo ujuzi nayo.

6

# Wabariki hao Wanaotuzunguka



'Bwana akubariki
    na kukulinda;
Bwana akuangazie nuru ya uso wake
    na kukufadhili;
Bwana akugeuzie uso wake
    na kukupa amani.'
Hesabu 6:24-26

**Maandalizi**

Uwe na:

- Mwambie mtu kwenye kikundi kusoma hadithi?
- Mwambie mtu kwenye kikundi asome kifungu cha Biblia?

**Karibu na Marejesho**

5 Dakika

- Mshukuru kila moja kwa kuja kwenye kwenye kikundi.
- Anza na maombi mafupi.
- Waulize kikundi kama wamefanya 'Kufanya wiki hii' na 'Shahidi' kazi ya wiki iliyopita.
- Waalike watu washuhudie kitu chochote walichojifunza au kuwa na ujuzi kwa kufanya kazi hizi.

**Lengo**

Lengo la kipindi hiki wiki hii ni kufahamu kuwa matunda ya Roho Mtakatifu siyo kwa faida yetu sisi wenyewe. Kwa njia hiyo ambayo Yesu alishirikisha maisha yake na tabia yake kwetu sisi, hivyo tunashiriki maisha yake na tabia kwa wale wanaotuzunguka.

**Kifungu cha Kukumbuka**

5 Dakika

Soma kifungu cha kukumbuka na nukuu za Biblia kwa sauti kwenye kikundi. Rudia kusoma tena kwa vifungu vidogo, waachie kikundi kurudia kila sehemu baada yako. Polepole soma tena kwa sehemu ndefu huku kikundi kikirudia kiła neno mpaka kiła moja atakapoweza kukariri kifungu chote. Watie baadhi watu moyo kujaribu na kurudia wao wenyewe.

> *24 Bwana akubariki*
> *na kukulinda;*
> *25 Bwana akuangazie nuru ya uso wake*
> *na kukufadhili;*
> *26 Bwana akugeuzie uso wake*
> *na kukupa amani.*

*Hesabu 6:24-26*

**Hadithi**

Wasomee kikundi hadithi inayofuata:

Mwaka 2005 Anthony Walker, kijana mwenye akili wa miaka 18 mwanafunzi wa zamani wa Merseyside kule Uingereza, aliuwawa na kikosi cha vijana kwenye ubishi wa mashambulizi ya kuropoka. Baadaye wawili wa hao waliohusika kwenye shambulizi walikamatwa na kushtakiwa kwa kuua. Familia yake ilikuwa mahakamani kupata undani wa shambulizi, na kusikiliza ushahidi wote ambao utatolewa. Mwisho wa kesi wale watu wawili walihukumia kifo na kupelekwa gerezani.

Kufuatilia kesi mama yake Anthony, Gee Walker, Mkristo mwaminifu, aliulizwa yeye anafikiri nini juu ya hao waliomuua mtoto wake. Alisema, ‘Ninapaswa kuwasamehe. Bado nawasamehe. Familia yangu na mimi bado tunasimama kwa kile tunachokiamini: msamaha.’

Kwenye mahojiano mengine dada yake Anthony akasema, ‘…ni lazima kusamehe, hicho ndicho tulichofundishwa, na hicho ndicho Biblia inachosema, na hicho ndicho tunachopaswa kufanya. Ni kitu cha kila siku. Ni ngumu, ni ngumu sana lakini tunapaswa kupitia. Inarahisha uchungu na hasira kama utaamka asubuhi na kufikiri “kusamehe, kusamehe, kusamehe.”

Familia ya Anthony walikuwa wametenga fungu la fedha kuwasaidia vijana weusi toka Merseyside kwenda kwenye shule ya sheria kama Anthony alivyopanga kufanya.[5]

[5] Evangelical Alliance (2005). *Mrs Walker has drawn on her Christian faith to find forgiveness for the two young men who murdered her son Anthony* [KWENYE MTANDAO] Inapatikana: www.eauk.org/current-affairs/news/mrs-walker-has-drawn-on-her-christian-faith-to-find-forgiveness-for-the-two-young-men-who-murdered-her-son-anthony.cfm [Imenakiliwa 12 January 2018]

5 Dakika

**Maswali**

Kwenye historia ya leo tunasoma juu ya familia inayojulikana, ingawa waliteseka hasa na kupata hasara bado waliweza kuonyesha msamaha na utu wema kwa hao waliowakosea.

Waulize watu wamepokeaje hadithi na uwaalike watu kushuhudia yale wanayoyafikiri.

Ruhusu dakika chache watu washuhudie kile wanachokifikiri na usikilize kwa makini kwa majibu mahali pale mtu anaposema juu ya kufanya mazoezi juu ya msamaha kama familia ya Walker walivyofanya. Kama mtu anasema hili, uwe na uhakika wa kusisitiza pointi hiyo.

**Kujifunza Biblia**

Soma Wafilipi 2:1-11 kwenye kikundi:

> 1 *Kama kukiwa na jambo lolote la kutia moyo katika*
> *kuunganishwa na Kristo, kukiwa faraja yoyote katika*
> *upendo wake, kukiwa na ushirika wowote na Roho, kukiwa*
> *na wema wowote na huruma,* 2 *basi ikamilisheni furaha*
> *yangu kwa kuwa na nia moja, mkiwa na upendo huo moja,*
> *mkiwa wa roho na kusudi moja.* 3 *Msitende jambo lolote kwa*
> *nia ya kujitukuza wala kujivuna, bali kwa unyenyekevu kila*
> *mtu amhesabu mwingine bora kuliko nafsi yake.* 4 *Kila*
> *mmoja wenu asiangalie faida yake mwenyewe tu, bali pia*
> *ajishughulishe kwa faida ya wengine.*
>
> 5 *Kuweni na nia ile ile aliyokuwa nayo Kristo Yesu:*
> 6 *Yeye, ingawa alikuwa na asili ya Mungu hasa,*
> *hakuona kule kuwa sawa na Mungu*
> *kuwa kitu cha kushikilia,*
> 7 *bali alijifanya si kitu,*
> *akachukua hali hasa na mtumwa,*
> *naye akazaliwa katika umbo la mwanadamu.*
> 8 *Naye akiwa na umbo la mwanadamu,*

*alijinyenyekeza, akatii hata mauti:*
*naam, mauti ya msalaba!*
[9]*Kwa hiyo, Mungu alimtukuza juu sana,*
*na kumpa Jina lililo kuu kuliko kila jina,*
[10]*ili kwa Jina la Yesu, kila goti lipigwe,*
*la vitu vya mbinguni, na vya duniani,*
*na vya chini ya nchi,*
[11]*na kila ulimi ukiri ya kwamba*
*Yesu Kristo ni Bwana,*
*kwa utukufu wa Mungu Baba.*

Kila mtu anataka kuwa na furaha. Kuwa na furaha au kubarikiwa ni tabia ya asili ya binadamu. Kila siku tunatamani kuwa na furaha na kupata kutoshelezwa. Hata hivyo, neno barikiwa lina maana zaidi ya furaha, kwa sababu kufurahi ni jambo la hisia na kwa kawaida inategemea mazingira ya nje. Kubarikiwa inahusu kufanikiwa na furaha yenye kuendelea kwa hao wanaoshuhudia wokovu wa ufalme wa Mungu.

Historia ya Yesu kwenye Injili na kifungu chetu cha leo inaonyesha kuwa Yesu alikuwa alama ya kukumbukwa ya baraka kwa watu wengine. Kusudi lake la kuja ni ili kufanyika baraka. Leo Yesu aliyefufuka matamanio yake ni kutubariki. Hata hivyo, usishangae kubarikiwa mbele ya macho ya Yesu haionekani wazi kama tunaweza kufikiri.

15 Dakika

**Maswali**

Kwenye kikundi cha 3 au 4 angalia Matayo 5:3-12, kifungu kinachojulikana kama ‘Hotuba ya mlimani.’ Mwache mtu moja asome kifungu kwa sauti kwa muda kadhaa ili wote waweze kusikia. Waambie kikundi kujadili maswali yafuatayo:

- Mjadili kwenye kikundi chenu ni namna gani kwa kawaida mnaelewa maana ya mtu kubarikiwa (mfano kuwa na afya nzuri, elimu, familia kazi, uwezo kiuchumi n.k.).
- Ni watu wa aina gani kifungu hiki kinasema wamebarikwa?

- Yesu anaelewaje changamoto ya baraka wazo tulilokuwa nalo mwanzo?
- Hii inakufanya ujisikieje?

Ruhusu hadi dakika 10 kwa majadiliano halafu urudishe kikundi pamoja tena na uruhusu muda kwa kila kikundi kushuhudia jambo moja au mawili kwa yale waliojadili.

Kwenye Wafilipi 2:1-11 Paulo anaeleza tena na tena kwamba mtazamo ni lazima uwe kama ule wa Kristo ambaye alifikiri juu ya wengine kwanza. Kama tu tutatazama na kuwatumikia na kuwabariki wengine kwanza tutakuwa tunajibariki wenyewe.

Wiki iliyopita tulitazama juu ya matunda ya Roho Mtakatifu. Tutawabariki watu ikiwa tutakuwa wavumilivu kwao, hata kama watachosha na wagumu. Tutawabariki watu ikiwa tutakuwa wema kwao wakati wengine hawako hivyo. Tutawabariki watu ikiwa tutawaletea furaha wakati wako na huzuni au wapweke. Inawezekana hata tumekuwa na ujuzi na baraka hizi wenyewe wakati wengine wametupenda, kuwa wema kwetu, na kuwa pamoja nasi wakati mambo magumu?

Tunaposikia jambo fulani kama tendo la kuelewa ukarimu tunaweza kuwa na wivu au chuki kwa mtu aliyepokea zawadi. Hata hivyo, tunapoona roho ya ukarimu ndani ya mtu mwingine tunapaswa kutamani kuwa na roho hiyo ya ukarimu ndani yetu. Hilo ni tunda ambalo Roho Mtakatifu anaweza kukua na kuendelea ndani yetu wakati maisha yetu mapya ndani yake kukua.

Tunazo baraka tofauti ndani ya maisha yetu. Tunaweza kuwa na upendo kwa marafiki na familia, tunaweza kuwa na nyumbani, chakula na maji na mavazi. Kupitia kwa Yesu pia tunazo baraka za msamaha, amani, maisha mapya, uzima wa milele, kusudi na uhakika kuwa tunafanya tofauti. Tumebarikiwa. Tusidhalilishe

baraka tulizonazo kwa kutunza wenyewe, lakini washirikishe wengine.

Kuwa kama Mungu iko ndani ya ujumbe wa moyo wa Yesu. Anatuambia kuwa na ‘rehema’ kama Mungu alivyo (Luka 6:36) na hata kuwa wakamilifu kama Mungu (Matayo 5:48). Ni kazi ya Roho Mtakatifu ndani yetu kutufanya sisi kuwa zaidi na zaidi kama Mungu. Anakuza matunda ndani yetu.

Njia moja ya namna ya kukua ni kuweka matunda yafanye kazi kwa kufanyika baraka kwa wengine. Yesu alikuwa hasa mtendaji wakati wote. Roho Mtakatifu ataonyeha kila moja wetu namna ya kuonyesha upendo wa utendaji na matendo kwa wengine. Ni muhimu pia kukumbuka kuomba kwamba wengine waweze kubarikiwa na Yesu.

Kifungu chetu cha kukumbuka leo ni ombi Mungu aliyomwabia Musa kuomba kama baraka juu ya Waisraeli. Tunaweza pia kuleta baraka toka kwa Mungu wakati tunaomba maombi haya kwa wengine. Tunaweza tena kufanyia kazi namna ya kuingiza maombi yetu kwenye matendo; zote mbili ni lazima ziende mkono kwa mkono.

10 Dakika

**Shughuli**
Kwenye kikundi cha 3 au 4, omba kwamba Roho Mtakatifu amlete mtu fulani kwenye fikira yako sasa mtu anayepambana au anayeteseka na anamwitaji baraka za Yesu kwenye maisha yao. Washirikishe wengine juu ya mtu huyo ambaye Roho Mtakatifu amemleta ndani ya maisha yako.

Kuwa makini usizungumze vitu ambavyo ni vya binafsi; labda unaweza tu kuwashirikisha juu ya jina la mtu huyo ama mambo machache kadhaa za changamoto wanazokabiliana nazo. Hiyo ni sawa. Jambo la muhimu ni kufikiri kwa uangalifu mtu unayemjua anayepambana.

5 Dakika

**Maombi**

Kwenye kikundi chako rudia kifungu cha kukumbuka ukitaja majina ya watu ambao umekuwa ukiwafikiria. Kwa kufanya hivyo unamwomba Yesu kumbariki mtu huyo.

Kwa mfano, unaweza kuomba:

> *Bwana mbariki Ruti na umtunze;*
> *Bwana fanya sura yake ing'are kwa Ruti na uwe na hisani kwake;*
> *Bwana geuza uso wake kwake Ruti na umpe amani.*

Omba maombi haya kwa kila moja uliyemfikiria kwenye kikundi chako.

**Kufanya Wiki Hii**

Kumbuka kuwa sisi ni, kama Yesu, tuwe baraka kwa wengine. Unaweza kuwa jibu kwa maombi na kuwa baraka kwa watu uliowaombea. Kila moja wenu afikiri namna ya kumbariki mtu uliyomwembea. Hapa kuna mawazo mengi mepesi:

- Onyesha upendo kwa mtu ambaye ni mpweke kwa kumtembelea na kuwa na wakati naye.
- Onyesha uwema kwa kuwatembelea na usile chakula ikiletwa na ule nyumbani kwako.
- Onyesha amani kwa mtu ukimsaidia kurejesha uhusiano uliovunjika.


Waambie watu wengine kwenye shughuli yako ndogo ya kikundi utakachoenda kufanya ambayo mnaweza kutiana moyo wiki hii. Halafu ombeni kwa pamoja mpate nafasi kufanya yale mliyoamua kufanya.

**Shahidi**

Kabla ya kuchukua hatua ya matendo uliyoamua kufanya, mwombe Mungu akupe nafasi na maneno ya kumweleza mtu yule uliyemfikiria na kuomba namna Yesu alivyokubariki na kwa nini sasa unataka kuwabariki wao.

Wakati ukiwa nao, tafuta nafasi ambayo Mungu atakupa na kuchukua muda kueleza kuwa Yesu amewaleta ndani ya moyo wako na kwamba unataka kushuhudia baraka ambazo Yesu amekupa wewe na wao pia.

# Kumbukumbu



7

# Ugonjwa Unaoua – Dhambi

'Kwa kuwa wote wametenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu.'

Warumi 3:23

**Maandalizi**
Unachohitaji kwa kipindi hiki:

- Karatasi ndogo kwa kila moja kwenye kikundi.
- Moto mdogo sehemu salama nje na maji ya kuzima ukimaliza.

Uwe na:

- Mwambie mtu kwenye kikundi kusoma hadithi?
- Mwambie mtu kwenye kikundi asome kifungu cha Biblia?

**Karibu na Marejesho**

5
Dakika

- Mshukuru kila moja kwa kuja kwenye kwenye kikundi.
- Anza na maombi mafupi.
- Waulize kikundi kama wamefanya 'Kufanya wiki hii' na 'Shahidi' kazi ya wiki iliyopita.
- Waalike watu washuhudie kitu chochote walichojifunza au kuwa na ujuzi kwa kufanya kazi hizi.

**Lengo**
Lengo la kipindi wiki hii ni kuelewa kuwa kitu chochote inachotuweka matakwa yetu wenyewe juu ya mapenzi ya Mungu inaitwa 'dhambi' ndani ya Biblia. Kama jinsi sura ya asili ya Mungu ndani yetu iliharibiwa na 'dhambi', kwa hiyo maisha yetu mapya yanaweza kuharibiwa na hata kuharibika kwa ajili ya dhambi. Lakini kuna uponyaji – ukikiri, tubu (badilisha namna yetu ya kufikiri) na kupokea msamaha.

**Kifungu cha Kukumbuka**

5
Dakika

Soma kifungu cha kukumbuka na marejeo ya Biblia kwa sauti kwenye kikundi. Rudia kusoma tena ukiacha kikundi kurudia baada yako mpaka kila mtu aweze kukariri kifungu chote. Watie baadhi ya watu moyo kujaribu kurudia wao wenyewe.

*Kwa kuwa wote wametenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu.*

*Warumi 3:23*

**Hadithi**

Wasomee kikundi hadithi inayofuata:

Kulikuwepo na watu wawili kwenye mji, moja tajiri na moja ni maskini. Mtu tajiri alikuwa na kondoo na mifugo mingi. Yule mskini alikuwa na mwakondoo. Alishikama naye, akakajali na kukilisha. Alikuwa kama binti kwake. Msafiri alifika kwa yule tajiri na huyo tajiri akataka kumtengenezea chakula. Alikuwa na kondoo na mifugo nyingi mali yake. Angeweza kumchinja moja katika hao kumtengenezea msafiri chakula. Lakini hakufanya hivyo. Badala yake, alichukua mwanakondoo wa yule maskini, akamuua na kumtengenezea msafiri chakula.

Mtu aliyesikia hadithi hii alikasirika. Akasema, ‘Mtu aliyefanya hivyo alistahili kufa!’ Akaongeza, ‘Lazima amlipe huyo mwanakondoo mara nne zaidi, kwa sababu amefanya jambo hilo na hakuwa na huruma.’

Alikuwa nabii, Nathan aliyesema hadithi hii kwa Mfalme Daudi. Iko kwenye Biblia (2 Samueli 12:1-6). Lakini Nathan akaongeza, ‘Wewe ndiye mtu huyo.’

Mungu alimchagua Daudi kuwa mfalme katika Israel. Alikuwa jasiri, mwenye hekima na zaidi ya yote alimpenda Mungu. Lakini pia alifanya kosa kubwa.  Daudi hakumwiba mwanakondoo. Alimwiba mke wa mtu mwingine, ingawa alikuwa na wake zake mwenyewe. Alivutiwa na Bathsheba. Alimwona alipokuwa akioga. Mumewe Uria alikua askari. Alikuwa mbali akipigana vita kwenye majeshi ya mfalme Daudi. Baada ya kugundua huyu mwanamke aliyemvutia ni nani, Daudi alifanya mapenzi naye. Baadaye akagundua kuwa ana mimba yake. Akapanga mpango wa Uria kurudi nyumbani toka vitani ili kwamba Uria baadaye afikiri mtoto ni wake. Hata alimwalika Uria kunywa mvinyo pamoja naye akamfanya kulewa. Lakini Uria alikuwa askari mtiifu asingeweza kwenda nyumbani na kulala na mke wake. Mpango wa mfalme Daudi uliposhindwa, akapanga na viongozi jeshi Uria apangwe mstari wa mbele wa vita ili aweze kuuwawa.

Uria aliuwawa vitani na Daudi akamchukua Bethsheba kuwa mkewe. Mungu hakufurahia tabia ya Daudi hivyo yule mtoto ambaye alimpa mimba akafa akiwa bado mchanga. Baada ya kutembelewa na nabii Nathan, Daudi alitambua alichokifanya na akasikitika.

**Kujifunza Biblia**
Soma Zaburi 51:1-12 kwenye kikundi:

1 *Ee Mungu, unihurumie,*
*kwa kadiri ya upendo wako usiokoma,*
*kwa kadiri ya huruma yako kuu,*
*uyafute makosa yangu.*
2 *Unioshe na uovu wangu wote*
*na unitakase dhambi yangu.*
3 *Kwa maana ninajua makosa yangu,*
*na dhambi yangu iko mbele yangu daima.*
4 *Dhidi yako, wewe peke yako, nimetenda dhambi*
*na kufanya yaliyo mabaya machoni pako,*
*ili uthibitike kuwa wa kweli unenapo,*
*na kuwa na haki utoapo hukumu.*
5 *Hakika mimi nilizaliwa mwenye dhambi,*
*mwenye dhambi tangu nilipotungwa mimba kwa mama yangu.*

6 *Hakika wewe wapendezwa na kweli itokayo moyoni,*
*ndani sana ya moyo wangu wanifundisha hekima.*
7 *Nioshe kwa hisopo, nami nitakuwa safi,*
*unisafishe, nami nitakuwa mweupe kuliko theluji.*
8 *Unipe kusikia furaha na shangwe,*
*mifupa uliyoiponda na ifurahi.*
9 *Ufiche uso wako usizitazame dhambi zangu,*
*na uufute uovu wangu wote.*
10 *Ee Mungu, uniumbie moyo safi,*
*uifanye upya roho ya uthabiti ndani yangu.*
11 *Usinitupe kutoka mbele zako*
*wala kuniondolea Roho wako Mtakatifu.*

*[12]Unirudishie tena furaha ya wokovu wako,*
*unipe roho ya utii, ili initegemeze.*

Zaburi hii ni maombi ya Mfalme Daudi baada ya kusikia hadithi. Ndani yake alikuwa anasema anaomba msamaha kwa ajili ya dhambi zake. Alitusaidia kufahamu dhambi ni nini na namna inavyokuwa kama ugonjwa.

**Ugonjwa ni nini**

Inaweza kuwa ni vigumu kuelewa kamili maana ya dhambi hivyo Mfalme Daudi alitumia maneno tofauti kueleza dalili tofauti za dhambi. Tutaenda kutazama maana ya maneno hayo ili itusaidie kushika tusiingie dhambini, la kwanza na bora zaidi, ni kuweka matakwa na matamanio yetu mbele za Mungu.

<u>Kosa</u> (kifungu 1 na 3)

Daudi alivunja mtiririko wa amri ya Mungu alipomwona mke wa Uria na kumchukua kuwa mke wake. Mungu alitoa amri hizo kwa watu wake kuwaonyesha namna ya kuishi maisha mazuri na kumpendeza yeye (kwa kusoma zaidi <u>Kutoka 20:1-17</u>). Mtiririko wa Daudi wa matendo ilivunja nyingi ya amri hizi. Kwa kumwona na kumtamani Bethsheba hii ikampelekea kumfanya mkewe, kufanya mapenzi naye, akafanya hila mumewe kurudi ili aweze kumpasia mtoto kuwa wake na mwishowe kupanga mumewe kuuwawa.

Tunapovunja amri za Mungu, tunafanya dhambi. Hii ndiyo maana ya kosa. Tunapovunja amri tuliyopewa na Mungu tunamkataa yeye na njia zake. Historia ya Daudi inatuonyesha kuwa dhambi moja inaongoza kwenye dhambi nyingine kwa haraka, kama ugonjwa wenye kuadhiri, kabisa inatukamata.

<u>Uovu</u> (kifungu cha 2 na 9)

Uovu maana yake ni kushindwa kuishi jinsi Mungu anavyotaka. Kifungu chetu cha kukumbuka inazungumzia jambo hili inaposema sisi sote ‘tumepungukiwa.’ Ni kama mwindaji na upinde na mishale au bunduki inayopiga risasi, lakini ikakosa

shabaha. Hata kama mwindaji amekosa shabaha kwa sentimeta kidogo sana au kwa mita kadhaa haijalishi; amekosa tu. Hii ni namna nyingine ya kuelewa maana ya dhambi: ni kukosa shabaha na inatuweka kwenye hatari kubwa. Hatari ni kutengana na Mungu.

Wakati mwingine tunawataza watu wanaotuzunguka halafu tunajiona kuwa wazuri kuliko wao tukijilinganisha nao. Pengine hatujawahi kuiba, kuua au kuzini. Pengine hatujawahi kuwajeruhi hao wanaotuzunguka na tumeishi maisha mazuri nay a utu wema. Hata hivyo Biblia haina shabaha ya maisha mazuri hiyo inawezekana kwa kila moja wetu, hata bora kwetu, kupata kwa nguvu zetu wenyewe.

Hatuwezi kujilinganisha sisi wenyewe na watu wengine lakini na Mungu, ni mtakatifu sana kamwe hatuwezi kuwa kama yeye, labda atusaidie, na hivyo ndivyo anavyofanya tunapokua katika maisha yetu mapya.

**Namna ya kutibu ugonjwa**

Kwenye Zaburi hii Daudi pia anatusaidia njia tofauti ambazo Mungu anaweza kusaidia sisi kushinda dhambi zetu na kukua na kufanana naye zaidi.

<u>Huruma</u> (kifungu cha 1)
Alipoonyeshwa dhambi zake, Daudi hakujaribu tena kuzificha. Aliomba huruma. Kuomba huruma ni kukubaliana na dhambi zetu. Tunapoelewa hayo kwamba tumefanya makosa tuanaweza kukiri kwa kutamka, kusema nisamehe na kuomba msamaha toka kwa mtu tuliyemkosea. Daudi alikiri kwa Mungu kwa sababu alitambua kuwa dhambi yake haikua kwa Uria tu bali kwa Mungu. Tunapaswa kuona kuwa dhambi ni kinyume na Mungu na kuomba huruma zake kwa sababu tunataka kweli kubadilika.

Wakati mwingine mtoto aliyekosea anaweza kuambiwa na wazazi wake au mwalimu kuomba msamaha wataondoa kisasi, ‘Nisamehe’, lakini kijana au binti ambaye ameomba msamaha

kinafiki. Kijana au binti anaweza kusema ‘nisamehe’ kujaribu kukwepa adhabu. Tunaposema ‘samahani’ na kuomba huruma za Mungu tunakwepa adhabu ambayo tulistahili. Hatupaswi kuishia hapo pia; tunapaswa kwa uhalisi kutafuta kufanya mabadiliko kwa tabia zetu na kumweka Mungu na mapenzi yake juu yetu sisi wenyewe.

Kuosha (kifungu 2 na 7)
Nguo zinapochafuka tunaziosha. Daudi alitambua kuwa dhambi zake zilimfanya kuwa mchafu na njia pekee ya kuwa msafi ni kusafishwa na Mungu. Hii ni sawa pia kwetu. Sisi sote tulifanywa ‘wachafu’ na dhambi na tunatakiwa kuoshwa na Mungu kuwa safi tena. Yesu aliendа zaidi kwa kuwaosha mitume wake miguu michafu kama tendo la unyenyekevu.

Alifundisha wanafunzi wake ingawa tayari walikuwa wamekwisha kuoga na walikuwa wasafi (kama jinsi tulivyokuwa tulipokubali zawadi za maisha mapya) walikuwa wanatakiwa kuendelea kuosha miguu inavyo endelea kupata uchafu. Hii ina tuonesha sisi kwamba tunapo kubali maisha mapya tunakuwa wasafi na tunakuwa huru na dhambi, lakini wakati huo ili kubaki kuwa safi kuna sehemu ndani yetu zinazotakiwa kuoshwa kila siku (angalia Yohana 13:1-11).

Uufute (kifungu 9)
Namna nyingine ya kuelewa kuwa safi ni picha ya kufuta. Fikiria vitu vibaya ulivyofanya viandikwe kwenye karatasi. Kisha vifutwe, au vichomwe. Hicho ndicho kinachotokea tunapo mwambia Mungu tusamehe dhambi zetu. Zimefutwa kabisa na haziko tena mahali pale.

Hivi ndivyo inavyotokea mara ya kwanza tunasema samahani Mungu na kukubali zawadi ya maisha mapya, tunapokuwa Wakristo. Lakini kama jinsi tulivyokwisha sema, Wakristo bado wanatenda dhambi mara kwa mara na wanataka kuendelea kuja kwa Mungu wakiomba huruma zake na msamaha.

10 Dakika

**Maswali**

Kwenye kikundi cha 3 au 4, jadili maswali yafuatayo:

- Unajisikiaje kuhusu kweli Mungu kusema sisi wote ni wenye dhambi na kupungukiwa? Je hii inaonekana kuwa sawa au kweli kwako? Kwa nini au kwa nini siyo?
- Utamwambia nini mtu ambaye anafanya kitu ambacho unajua Biblia inasema ni dhambi, anayejibu kuwa vyote vitakuwa sawa kwa sababu wameomba juu yake na wanajisikia sawa kufanya hivyo?
- Unapovutiwa kufanya vitu katika maisha yako unavyo vijua ni dhambi, utashindaje majaribu?

15 Dakika

**Shughuli**

Utahitaji kuwa na kipande cha karatasi, kitu cha kuandikia na uwe na moto/mshumaa kwa shughuli hii. Unapaswa kufanya shughuli hii nje sehemu na wazi. Kama kuna mtoto anapata nafasi ya kushiriki, mtu mzima ni vema kuwasaidia kwenye shughuli hii.

Chukua muda kufikiri juu ya maisha yako wakati hujamweka Mungu kuwa wa kwanza kwenye maisha yako. Orodhesha dhambi tofauti ndani ya maisha yako.

Mtie moyo kila mmoja wawe pea na washiriki jambo 1 au 2 ya orodha pamoja nao kama tendo la kutubu. Watu wengine wanaweza wasipende kushirikisha yale waliyoandika chini. Kama ni hivyo, usiwalazimishe kufanya hivyo. Waambie watu kuombeana kumwomba Mungu kwa huruma zake leo.

Sasa chukua orodha kwenye moto na uweke kwenye moto kwa uangalifu. Angalia ikiungua.

Mara orodha itakapokuwa imeungua yote, chukua muda kidogo kumsifu Mungu na kumshukuru kwamba amechukua dhambi zako zote na aibu. Omba na kumwomba kubadilisha dhambi zako kwa zaidi kwake ndani ya maisha yako.

Kumbuka kuuzima moto baada ya kumaliza shughuli hii.

**Maombi**

10 Dakika

Waulize kikundi kama kuna mtu yeyote aliyepo ambaye bado hajaomba msamaha kwa Mungu kwa mara ya kwanza na kama angependa kufanya hivyo. Kama kuna mtu basi mwongoze, kupitia maombi haya yafuatayo:

> *Mungu mwema nisamehe kwa dhambi nyingi ndani maisha yangu, lakini zaidi ni kwa sababu sijakuweka wewe wa kwanza na kufuata njia zangu mwenyewe. Leo nataka kugeuka kutoka kwenye njia zangu za zamani, na kukuweka wewe wa kwanza, na kukufuata wewe. Tafadhali nijaze na Roho wako Mtakatifu na unisafishe kabisa. Nisaidie kuishi maisha safi ninapokua ndani yako. Amina.*

Waeleze kikundi tutaenda kuwa na wakati tulivu muda wa maombi pamoja. Waambie wafunge macho yao wakati tunapoomba.

Anza na maombi mepesi ukimwalika Roho Mtakatifu kuongea na kila moja wetu wakati tunapoomba.

Sasa soma Zaburi 51:1-12 tena. Wakati huu soma polepole kwenye kikundi. Simama baada kila pea ya mistari na uruhusu muda kwa watu kutulia kusikiliza Roho Mtakatifu na kuomba ndani ya mioyo yao.

Mwishoni, funga kwa maombi mafupiukimfikiria Mungu kwamba tunapokiri dhambi zetu kama tulivyofanya, yeye ni wa huruma, anatusafisha kuwa safi na kufuta dhambi zetu.

**Kufanya Wiki Hii**

Kila wiki kuna kazi ya nyumbani ya kufanya. Wakati unapo jaribiwa kujilinganisha na watu wengine wiki hii kujisikia kuwa dhambi zao labda ni mbaya sana zaidi ya za kwako, halafu rudia kifungu cha kukumbuka peke yako.

*Kwa kuwa wote wametenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu.*

*Warumi 3:23*

Omba kwamba Mungu akusaidie ili usijilinganishe na wengine lakini tafuta kufananya naye kwa kumweka yeye mbele kwenye maisha yako.


**Shahidi**

Mara nyingine ni rahisi kusema ‘nisamehe’ Mungu kwa dhambi zetu zaidi ya yule mtu uliyemfanyia dhambi. Je kuna mtu ambaye tumemkosea ambaye tunapaswa kumwambia ‘nisamehe’ na kupokea msamaha? Ikiwa yupo, mwombe Mungu akupe maneno sahihi na nafasi sawa na ujikubali mwenyewe kusema nisamehe kwa mtu huyo wiki hii.

Omba kwa ajili ya nafasi kujieleza kwao kwa nini unaomba msamaha kuwa matokeo ya maisha mapya uliyopokea kwa Mungu.

8

# Nini Maana ya Kusamehe – Neema



'Kuweni na huruma, kama Baba yenu alivyo na huruma. "Msihukumu, nanyi hamtahukumiwa. Msilaumu, nanyi hamtalaumiwa. Sameheni, nanyi mtasamehewa.'

Luka 6:36-37

**Maandalizi**

Uwe na:

- Mwambie mtu kwenye kikundi kusoma hadithi?
- Mwambie mtu kwenye kikundi asome kifungu cha Biblia?
- Waambie watu 3 au 4 kuleta Biblia kama wanyo moja?

**Karibu na Marejesho**

5 Dakika

- Mshukuru kila moja kwa kuja kwenye kwenye kikundi.
- Anza na maombi mafupi.
- Waulize kikundi kama wamefanya ‘Kufanya wiki hii’ na ‘Shahidi’ kazi ya wiki iliyopita.
- Waalike watu washuhudie kitu chochote walichojifunza au kuwa na ujuzi kwa kufanya kazi hizi.

**Lengo**

Lengo la kipindi wiki hii ni kuelewa kuwa dhambi zetu zinasamehewa siyo kwa sababu tunastahili lakini ni kwa yale ambayo Mungu amefanya kwa ajili yetu. Kwa sababu tumesamehewa, sasa tunaweza kutoa msamaha kwa hao waliotukosea.

**Kifungu cha Kukumbuka**

5 Dakika

Soma kifungu cha kukumbuka na nukuu za Biblia kwa sauti kwenye kikundi. Rudia kusoma tena kwa vifungu vidogo, waachie kikundi kurudia kila sehemu baada yako. Polepole soma tena kwa sehemu ndefu huku kikundi kikirudia kiła neno mpaka kiła moja atakapoweza kukariri kifungu chote. Watie baadhi watu moyo kujaribu na kurudia wao wenyewe.

> 36 *Kuweni na huruma, kama Baba yenu alivyo na huruma.*
> 37 *“Msihukumu, nanyi hamtahukumiwa. Msilaumu, nanyi hamtalaumiwa. Sameheni, nanyi mtasamehewa.*
>
> *Luka 6:36-37*

**Hadithi**

Wasomee kikundi hadithi inayofuata:

Hapo mwanzo kulikuwepo na mtu aliyekuwa na wana wawili. Mdogo akamwambia baba yake, ‘Baba, nataka kile kinachoniangukia’.

Hivyo baba akagawanya mali kati yao. Haikuchukua muda kabla yule kijana mdogo hajapakia mabegi yake na kwenda kwenye nchi ya mbali. Huko hakuwa na nidhamu na akatapanya, na kupoteza kila kitu alichokuwa nacho. Baada ya kumaliza fedha zake zote, njaa ikatokea katika nchi ile yote na akaanza kuumia. Aliajiriwa na mwenyeji wan chi ile akampeleka mashambani kutunza nguruwe. Alikuwa na njaa kali kiasi cha kutamani kula chakula cha nguruwe, na hakuna mtu aliyampa kitu chochote.

Hii ikamrudisha kwenye fahamu zake. Akasema, ‘Hao wanyakazi wa mashamba wa baba yangu hula milo mitatu kwa siku, na hapa nateseka kufa. Narudi kwa baba yangu. Nitamwambia, Baba, nimekosa mbela za Mungu, na nimekosa mbele zako; sistahili kuitwa mwanao. Nichukue kama mwajiriwa tu.’ Alinyanyuka akarudi kwa Baba yake.

Alipokua angali mbali, baba yake alimwona. Moyo wake ukagonga, akamkimbilia, na kumkumbatia, akambusu. Mtoto wake akaanza maelezo yake: ‘Baba, nimekosa mbele za Mungu, na nimekosa mbele zako; sistahili kuitwa mwanao tena.’

Lakini wala baba yake hakuwa anamsikiliza. Yeye alikuwa akiwaita watumishi, ‘Haraka. Leteni mavazi mazuri na mumvike. Mvikeni pete ya familia na viatu kwenye miguu yake. Halafu mleteni kondoo aliyenona akaangwe. Tunaenda kuwa na karamu na wakati mzuri! Mwanangu yuko hapa – alikuwa amekufa na sasa amefufuka! Alikuwa amepotea na sasa amepatikana!’ Wakaanza kuwa na wakati mzuri.

Wakati huu wote kijana wake mkubwa alikuwa mashambani. Baada ya muda wa kazi kuisha alirudi. Alipokaribia nyumbani, akasikia musiki na denci. Akamwita moja wa watumishi nyumbani, akamuuliza nini kinachoendelea. Akamwambia, 'Ndugu yako amerudi nyumbani. Baba yako ameagiza karamu – nyama ya kondoo! – kwa sababu amempata tena nyumbani salama na sauti.'

Kaka mkubwa akaondoka akiwa amekasirika na akakataa kuingia ndani. Baba yake akatoka nje na kujaribu kuzungumza naye, lakini hakutaka kusikiliza. Mwanawe akasema, 'Angalia ni miaka mingapi nimekaa hapa nikikutumikia, bila kukupa wakati wowote wa huzuni, lakini uliwahi kunifanyia pati na marafiki zangu? Halafu huyu mtoto wako ambaye ametapanya fedha zako kwenye ukahaba ametokea halafu unamfanyia tafrija!'

Baba yake akasema, 'Mwanangu, wewe huelewi. Ukuwa name siku hizi zote, na kila nilichokuwa nacho ni chako – lakini huu ni wakati wa ajabu, na tunatakiwa kusherehekea. Huyu ndugu yako alikuwa amekufa, na sasa yu hai! Alikuwa amepotea, na sasa amepatikana!'[6]

Hadithi hii inapatikana kwenye Biblia Luka 15:11-32.



15
Dakika

**Shughuli**

Kuhakikisha kuwa kila moja anaeleawa hadithi ya mwana mpotevu na baba mwenye kusamehe tutaenda kuigiza hadithi hii.

Gawanya kila mjo kwenye kikundi cha 4. Mtu moja atakuwa ana hadithia hadithi, wakati wale watatu watachukua nafasi ya baba, mwana na kaka mkubwa.

[6] Scripture taken from The Message. Copyright © 1993, 1994, 1995, 1996, 2000, 2001, 2002. Used by permission of NavPress Publishing Group.

Kipe kikundi dakika 5 kujiandaa halafu, moja kwa mwingine, kila kikundi wanaweza kuigiza hadithi kwa wengine.

**Kujifunza Biblia**

Hii ni hadithi inayojulikana sana kwenye Biblia. Mwana aliondoka akaenda mbali, akatapanya kila kitu alichopewa na baba yake, halafu alipokuwa hana pa kuishi na fukara, alirudi kwa baba yake. Alijua alimtusi baba yake na kuharibu mali yake, lakini alitegemea baba yake anaweza kuwa mwema na kumfanya kuwa mtumishi. Mara nyingine hadithi inaitwa hadithi ya Mwana Mpotevu; hata hivyo wengine wanaiita hadithi ya Baba mwenye Msamaha, kwa kuwa ndiye ufunguo wa tabia ya kuigwa. Tendo la Baba yake inatuonyesha maana ya neema na msamaha ni nini. Tunaenda kufikiri juu ya familia hii na kile anachotufundisha.

**Kijana mdogo alistahili kukemewa kwa ukali**

Kijana mdogo alifanya vibaya sana. Kitu cha kwanza, alitaka apewe urithi wake wakati baba yake bado alikuwa hai. Ni kama tu anasema, ‘Nahitaji fedha zangu, natamani kama ulikuwa umekufa.’ Jambo la pili, aliondoka akenda kutapanya fedha za baba yake kwa wanawake, akilewa na kucheza pati. Mwishowe fedha zikaisha. Siku moja alikuwa na njaa sana hata akatamani kula chakula walichopewa nguruwe. Kwa mtu wa Kiyahudi jambo hili halikukubalika kabisa kwa sababu walijua nguruwe ni mnyama ambaye alikuwa najisi, lakini alichanganikiwa na kuwa na njaa. Hakuna mashaka kuwa kijana alimtusi baba yake na familia na alitumia vibaya fedha zote alizopewa na baba yake. Alistahili kuadhibiwa; wengine hata wangesema matendo yake hayasameheki.

**Majibu ya Baba yanatuonyesha neema ni nini**

Baba yake, hata hivyo, anatunyesha sisi neema na msamaha ni nini. Hata ingawa mtoto alistahili adhabu, hata ingawa baba alitukanwa, wajibu wake haikuwa kutafuta adhabu hasa kwa alivyopoteza na kosa. Wajibu wake ni haki sawa kwa mwanawe. Baba alikimbia kukutana na mwanawe aliyeonekana akija kutoka mbali. Badala ya kumuhudumia kama matendo yake

yalivyostahili, anamkumbatia na kumrejesha kwenye sehemu yake ndani ya familia. Baba alipuuza ‘kilichomilikiwa’ na yeye kwa ajili ya mwanaye.

**Mungu ni kama Baba, sisi ni kama wana**
Lengo la historia ni kwamba Mungu ni kama Baba. Sisi na watu wengine tunaweza kuwa kama wana.

Tuko kama kijana mdogo tunapomkataa Mungu, kumgeuzia mgongo na njia zake. Mara nyingi tumekiaribu kile alichotupa na tunajiingiza wenyewe kwenye hali ya kuchanganyikiwa. Lakini, Mungu anatusamehe bure na kutukumbatia tunaporudi kwake. Hivyo ndivyo upendo wa Mungu unavyofanania. Imejaa neema. Neema ni uwezo wa kumsamehe mtu mwingine, kumrejesha mtu fulani hata kama hakustahili. Baba hakuwa na ugumu wa kusamehe; hakutaka kushawishiwa. Alikimbia kumlaki mwanawe. Hii ni picha yenye nguvu ya upendo wa Mungu.

Tunaweza pia kuwa kama yule kijana mkubwa na wakati mwingine tuanatambua. Mara nyingi tunasahau kuwa tumesamehewa na kuchukua mahusiano yetu na Mungu kwa idhini. Kama kaka mkubwa tunakuwa na wivu kwa wengine, kuona neema ya Mungu kwao ni ya ukarimu mno na hawakustahili. Ni kweli msamaha wa Mungu na neema hawakustahili lakini hatupaswi kuwa na wivu kuona wengine wanapokea kile ambacho tayari sisi tunacho. Kanisa, watu wa Mungu hawapaswai kuwa na hasira kwa wale ambo Mungu anataka kumsamehe. Hatupaswi kuwaadhibu. Tuwaonyeshe neema na kuwa kama baba na siyo kama kaka mkubwa.

**Kwa nini tunapaswa kuwaonyesha watu neema?**
Baba na kaka mkubwa walikuwa na majibu tofauti baada ya mwana mpotevu kurudi nyumbani. Baba alionyesha neema na msamaha, kaka mkubwa hakufanya hivyo. Nini ilisababisha tofauti? Ni tofauti zao kimtazamo. Kaka mkubwa alikuwa kijana bora kwa baba, akikaa naye na kumtumikia, lakini alimwona mdogo wake tu kama moja aliyefanya makosa na alistahili haki na

adhabu. Baba aliona zaidi ya hilo kwa sababu alikuwa mwenye huruma, kama kifungu chetu cha kukumbuka kinavyotukumbusha sisi. Aliona kuwa mwanaye alikuwa amepotea, alikuwa amekufa kwake na ukweli ni kwamba yu hai. Kaka mkubwa aliona tu adhabu; baba aliona mwanawe akirudi akiwa hai tena.

Neema ilifanya haya kuwezekana. Msamaha wa Baba. Ingawa mwanaye hakustahili hili, akamfanya mwanaye kuwa hai tena.

Wakati Yesu alipowafundisha wanafunzi wake juu ya msamaha aliwapa changamoto kusamehe tena na tena kwa kurudia. Moja wao alimuuliza ni mara ngapi kusamehe, kimisingi akiwaza kama kuna kiwango cha msamaha wa Mungu. Yesu alijibu tunapaswa kusamehe tena na tena, mpaka mara 77, ambayo alimaanisha hakuna kiwango. (Kwa zaidi soma Matayo 18:21-22.)

**Tunaweza kupata msamaha kwa Mungu**
Kila moja wetu amepewa maisha mapya wakati tumepokea zawadi ya Mungu ya neema na msamaha. Hao walioko mbali na Mungu wanaweza kupata msamaha na neema kutoka kwa Mungu. Kila moja wetu kwenye kikundi anaweza kumjua Mungu na msamaha wake kwenye maisha yetu. Wote tunatakiwa kuwa kama mwana anayetambua nafasi yake na kurudi tena kwa baba yake. Mungu ni baba wa neema ambaye atatusamehe sisi.

Kama baba, Mungu anatuita sisi kutoa bure hiyo zawadi ya neema na msamaha kwa wote tulio na uhusianao nao. Kuna watu tunaowafahamu ambao wanaweza kufanywa hai tena kwa tendo la neema kutoka kwetu.

10 Dakika

**Maswali**
Kwenye kikundi cha 3 au 4 mjadili maswali yafuatayo. Baada ya kujadili, weka wakati wa kuleta marejesho kwenye kikundi kikubwa. Ni muhimu kuwa kila moja ajifunz kwa mwingine.

- Tunaweza kufikiri wakati ambazo tumeudhiwa, kudanganywa au kujeruhiwa na tumetaka huyo mtu aliyetukosea kuadhibiwa?
- Ni mara ngapi tunapaswa kumsamehe mtu?
- Kuna mtu amepata mfano wa kuwa inafananaje kusamehe mtu ambaye hakustahili? Hii iliwabadilishaje na mtu aliyepokea msamaha?
- Baba alipaswa kumsamehe mwanaye? Ni sawa kuwa mwana mpotevu aliyerudi nyumbani hapati adhabu kwa tabia yake?
- Neema ya baba ilifanyaje mwanaye kuwa hai kwake tena? Nini kingeweza kutokea kama baba angemwadhibu yeye?
- Je mara nyingi tunatenda kama kaka mkubwa, kuwakataa wale ambao hawako kama sisi wasikuwa na tabia nzuri? Kama ni hivyo, hao ni watu gani na tutawafanyaje tuweze kuwabadilisha?

Hakikisha unachukua muda zaidi kushuhudiana moja kwa mwingine.

10 Dakika

**Maombi**

Gawanya kikundi kwenye pea. Mtie moyo kila mtu kujifikiria wenyewe ukiwauliza maswali mawili:

- Je kuna kitu chochote ambayo wanataka kuomba neema ya Mungu na msamaha kwenye maisha yao wenyewe?
- Kuna mtu yeyote ambaye anataka kuonyesha neema na msamaha pia?

Waambie watu washirikishe majibu yao kwa maswali haya kwenye pea zao halafu kila moja amwombee mwenzake.

**Kufanya Wiki Hii**

Kila wiki kuna kazi ya nyumbani ya kufanya. Wakati wa wiki, mwombe Mungu akuonyeshe mahali unapozuia msamaha kwa watu wengine na mazingira kwenye maisha yako mwenyewe. Kila siku uwe na muda wa kumwomba Mungu akuonyeshe. Fikiri juu ya hadithi ya baba mwenye kusamehe na ni kwa jinsi gani

unaweza kuwa kama yeye. Mwombe Mungu akusaidie uanze kusamehe zaidi.

**Shahidi**

Waeleze kikundi kuwa tunapozuia msamaha kwa watu, itawasababishia shida, lakini pia itatusababishia sisi pia shida. Itasababisha shida kibinafsi pamoja na uchungu na hasira. Inaweza pia ikasababisha shida kwenye jumuia yetu na kugombana na vikundi vya watu. Msamaha huwaachilia watu kwenye maisha.

Kuna mambo mawili ambayo tutafanya wiki hii ili kuwa shahidi. Kama unamzuilia mtu msamaha, ni lazima kuwaonyesha neema, acha haki yetu iondoke ya hasira na uende na kuwasamehe. Ni lazima kupatana nao, hata kama hawstahili. Kwa njia hii tutawapa uzima. Kama hatutaweza kwenda kihalisi na kuzungumza nao kwa sababu yeyote, tunaweza kuwasamehe ndani ya mioyo yetu.

Kama tunawafahamu marafiki wawili ambao wanao hasira na wanazuiya msamaha kwa mtu mwingine, au watu wawili kwenye jumuia, tunaweza kufikiri juu ya kitu cha kufanya kuwapata pamoja na kuzungumza. Labda matendo yetu wenyewe itaishia kwenye neema kati yao na msamaha.

# Kumbukumbu

9

# Sisi ni wa Mungu - Ukombozi



**'Ndani yake tunao ukombozi kwa njia ya damu yake, yaani, msamaha wa dhambi, sawasawa na wingi wa neema yake aliyotumiminia kwa wingi, kwa hekima yote na maarifa yote.'**

Waefeso 1:7-8a

**Maandalizi**

Uwe na:

- Mwambie mtu kwenye kikundi kusoma hadithi?
- Mwambie mtu kwenye kikundi asome kifungu cha Biblia?

**Karibu na Marejesho**

5 Dakika

- Mshukuru kila moja kwa kuja kwenye kwenye kikundi.
- Anza na maombi mafupi.
- Waulize kikundi kama wamefanya 'Kufanya wiki hii' na 'Shahidi' kazi ya wiki iliyopita.
- Waalike watu washuhudie kitu chochote walichojifunza au kuwa na ujuzi kwa kufanya kazi hizi.

**Lengo**

Lengo la kipindi wiki hii ni kufahamu kuwa kupitia neema yake Mungu ametununua sisi kwa gharama. Tulipokuwa watumwa wa dhambi kwenye maisha yetu wenyewe. Biblia inatumia picha ya mtumwa wa sokoni kuonyesha kwamba kupitia kifo Yesu Mungu alituweka huru na kwa sasa sisi ni wakwake.

**Kifungu cha Kukumbuka**

5 Dakika

Soma kifungu cha kukumbuka na nukuu za Biblia kwa sauti kwenye kikundi. Rudia kusoma tena kwa vifungu vidogo, waachie kikundi kurudia kila sehemu baada yako. Polepole soma tena kwa sehemu ndefu huku kikundi kikirudia kiła neno mpaka kiła moja atakapoweza kukariri kifungu chote. Watie baadhi watu moyo kujaribu na kurudia wao wenyewe.

> *7 Ndani yake tunao ukombozi kwa njia ya damu yake, yaani, msamaha wa dhambi, sawasawa na wingi wa neema yake*
> *8 aliyotumiminia kwa wingi, kwa hekima yote na maarifa yote.*
>
> *Waefeso 1:7-8a*

5
Dakika

**Shughuli**

Wapeleke watu wote nje au kwenye chumba chenye nafasi kwa mtu kuweza kukimbia akizunguka kwa mchezo huu. Kama kuna mtu ambaye hataweza au hataki kukimbia, wanaweza kuangalia mchezo na kushangilia kwa kutia moyo.

Mtu moja atakuwa kocha. Changamoto yao ni kujaribu na "kuambatanisha" (mguse poleple kwenye bega au mkono) kila mtu kwenye kikundi.

Tutakapoanza mchezo, kila moja atajaribu kumkimbia mshikaji na wasiruhusu kuambatana na mshikaji. Mshikaji akiambatana nawe, akakugusa basi lazima ukae chini juu ya sakafu na atakuwa ametoka kwenye mchezo. Mshikaji ajaribu kuambatana au kumgusa hadi wote wakae juu ya chini.

Hata hivyo, mtu moja ni mkombozi. Mshikaji hawezi kuambatana au kumgusa mkombozi. Ikiwa mtu yeyote atakuwa ameguswa na mshikaji na amekaa chini wanaweza kuokolewa na kurudishwa kwenye mchezo na mkombozi. Mkombozi ni lazima awafikie na kuambatana nao. Wanaweza basi kusimama tena na kurudi kwenye mchezo, huru kurudia na kukimbia tena mbali na mshikaji!

Mchezo unaweza kuendelea kwa muda mrefu hivyo unapaswa kuufikisha mwisho baada ya dakika 4 au 5 wakati watu wengi watakuwa tayari wameambatanishwa ma mshikaji na mkombozi.

**Hadithi**

Wasomee kikundi hadithi inayofuata:

Nikolas Kristof na mkewe Sheryl WuDunn walipata tuzo la ushindi wa uandishi walioandika kwa gazeti Wakati la New York. Walisafiri mara kadhaa kule Asia, wakitoa taarifa kwa yale waliyoshuhudia huko.

Kwa majibu kwa yale wayoyaona Nikolas na Sheryl waliandika kitabu kilichovuviwa, kilichoitwa ‘Nusu ya Anga’, yenye hadithi nyingi za matumaini toka kwa wanawake waliopona kinyume na ubaguzi na mazingira yenye kutisha. Msichana moja alikuwa Srey Neth. Kwenye umri wa miaka 14 alikuwa kwenye danguro kule Poipet, Cambodia kwa mwezi. Binamu wake alimtoa kijijini kwao na kumuuza kwa ajili ya ukahaba. Bikira yake iliondolewa na meneja wa casino ya Thai ambae baadaye alikufa kwa ugonjwa wa UKIMWI. Sasa aliuzwa kwenye danguro kwa watu wa kawaida kwa gharama kubwa. Kristof alimnunua kwa paundi 150, siyo kwa kumdhalilisha ila kumweka huru. Alimrudisha kijijini kwao na kwa familia yao upande mwingine wa Cambodia na kwa msaada wa shirika la Amerika walijaribu kjumkubalisha tena kwenye jamii.

Srey Neth **alikombolewa**, akitolewa kwenye utumwa na Kristof. Ingawa aliadhirika na VIRUSI vya ukimwi, alikubaliana kamili na matibabu ya hospitali na sasa ameolewa na ana mtoto. Mara ya mwisho Kristof alipokutana naye, alikuwa na mpango wa kufungua saluni ya kutengeneza nywele, akiipa jina la Kristof.[7]

**Kujifunza Biblia**

Historia ya Biblia ni historia ya **ukombozi.** Mungu anawaokoa watu wake mara kwa mara tena. Aliwakomboa Waisreli toka utumwani na kuwaleta kwenye nchi ya Kanaan, urithi wao. Hadithi hii inaitwa ‘Kutoka’ ambayo ina maana njia ya kutokea. Ukombozi kwenye Agano la Kale ilionyesha mbele kwenye ukombozi ikikamilishwa na Yesu kwenye Agano Jipya. Yesu ametupa njia ya kutokea kwenye maisha yetu ya dhambi, kwenye maisha mapya ambayo sisi ni wake.

Hii imeelezwa kwenye kitabu cha Ruti. Mama anayeitwa Naomi aliondoka Bethlehemu na mumewe na vijana wake wawili kwa sababu ya njaa, wakaenda kwenye nchi ya Moabu. Huko vijana wake wakaoa wanawake kwenye maeneo. Baada ya muda, mumewe na vijana wake wawili walikufa. Naomi akaamua kurudi

[7] Kristof, Nicolas D. and WuDunn, Sheryl, (2009) *Half the Sky* New York: Alfred A. Knopf

kwenye nchi yake mwenyewe, na mkwe wake Ruti akachagua kuondoka. Ruti hakupaswa kwenda na Naomi; ukweli ilikuwa ni tendo la kushangaza la ujasiri kuondoka na kwenda kuishi kwenye nchi ya kigeni akiwa mjane. Kwa ukweli ilikuwa ngumu, kuishi bila msaada kwenye nchi ya kigeni. Hata hivyo Ruti na Naomi wakakombolewa na matendo mema ya Boazi, jamaa ya Naomi, aliyemchukua Ruti kuwa mkewe na kuwasaidia wote wawili. (Unaweza kusoma historia ya matendo mema ya Boazi kwenye kitabu cha Walawi 25:25.) Ona jinsi Yesu alivyotimiliza jambo hilo kwetu Waebrania 2:14-18.)

Mwandishi Leon Morris anasema ukombozi maana yake ni kulipa gharama ya kumweka mtu huru.[8] Wakati wa Agano Jipya neno komboa ilitumika kwa:

- kuachiliwa kwa watumwa kwa kulipa gharama.
- kuwanunua tena wafungwa wa kivita kwenye uteka wao.
- kuachiliwa kwa mtu kwenye adhabu ya kifo.

?

5 Dakika

**Maswali – Namna ya kuomba?**

Gawanya kikundi kwenye vikundi 3 vidogo. Waambie kila kikundi kutazama moja ya vifungu hapo chini, mjadili kwa dakika kadhaa halafu mshirikishe kikundi kikubwa namna kazi ya Yesu inavyohusiana na ukombozi. (Majibu unayosikiliza yamo kwenye mabano.)

- Kikundi 1 – Warumi 6:6-7
  (Yesu anamkomboa mwamini toka kwenye utumwa wa dhambi)
- Kikundi 2 – Wakolosai 2:15
  (Yesu ametutoa kwenye utumwa wa nguvu za shetani)
- Kikundi 3 – Waebrania 2:14-15
  (Msalaba wa Yesu umetuachilia sisi toka adhabu ya mauti)

[8] Morris, Leon, (1984) *The Atonement* Westmont:Inter-Varsity Press

Soma Waefeso 1:1-14 kwenye kikundi:

*[1]Paulo, mtume wa Kristo Yesu, kwa mapenzi ya Mungu:
Kwa watakatifu walioko Efeso, walio waaminifu katika
Kristo Yesu:*

*[2]Neema na amani itokayo kwa Mungu Baba yetu na kwa
Bwana wetu Yesu Kristo iwe nanyi.*

*[3]Ahimidiwe Mungu na Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo,
aliyetubariki sisi kwa baraka zote za rohoni, katika
ulimwengu wa roho ndani ya Kristo. [4]Kwa maana
alituchagua katika yeye kabla ya kuumbwa ulimwengu ili
tuwe watakatifu na bila lawama mbele zake. Kwa upendo
[5]alitangulia kutuchagua tuwe wanawe kwa njia ya Yesu
Kristo kwa furaha yake na mapenzi yake mwenyewe. [6]Kwa
hiyo tunamsifu Mungu kwa huruma zake kuu alizotumiminia
sisi katika Mwanawe Mpendwa. [7]Ndani yake tunao
ukombozi kwa njia ya damu yake, yaani, msamaha wa
dhambi, sawasawa na wingi wa neema yake
[8]aliyotumiminia kwa wingi, kwa hekima yote na maarifa
yote. [9]Naye alitujulisha siri ya mapenzi yake sawasawa na
uradhi wa mapenzi yake, ambayo alikusudia katika Kristo,
[10]ili yapate kutimizwa wakati mkamilifu utakapowadia,
yaani, kuvitia vitu vyote vya mbinguni na vya duniani
pamoja, chini ya kiongozi mmoja, ndiye Kristo.*

*[11]Katika Kristo sisi nasi tumepata urithi, tukisha kuchaguliwa
sawasawa na kusudi la Mungu, yeye ambaye hufanya
mambo yote kulingana na kusudi la mapenzi yake, [12]ili
kwamba, sisi tuliokuwa wa kwanza kuweka tumaini katika
Kristo, tupate kuishi kwa sifa ya utukufu wake. [13]Ninyi pia
mliingia ndani ya Kristo mliposikia Neno la kweli, Injili ya
wokovu wenu. Mkiisha kuamini, ndani yake mlitiwa muhuri,
yaani, Roho Mtakatifu mliyeahidiwa, [14]yeye ambaye ni
amana yetu akituhakikishia urithi wetu hadi ukombozi wa
wale walio milki ya Mungu kwa sifa ya utukufu wake.*



Baada ya utambulisho wa vifungu (vifungu 1 – 2) Paulo alianzisha sifa kwa baraka za Mungu ‘ndania ya Kristo’ (kifungu 3). Kwamba waamini ‘ndani ya Kristo’ ina maana kwamba ni wa kwake, ni ufunguo wa kuelewa barua. Paulo alitumia namba ya sitiari inayoonyesha yale ambayo Kristo alifanya kwa ajili yetu:

- Kuchaguliwa na kuwa wanawe katika Kristo (kifungu 3-6) ambayo inauhusiana na kuchaguliwa na Mungu na kuletwa kwenye familia yake.
- Ukombozi na upatanisho katika Kristo (kifungu 7-10) inahusiana na kununuliwa tena au kupewa njia ya kuwa na Mungu.
- Uhakika wa urithi wetu katika Kristo (kifungu 11-14) ambayo ina maana kuwa wana wa kiume na kike tunakuwa na nafasi kwake, na kwa wote walio wake.

Kwenye kipindi hiki tunazingatia hasa juu ya ukombozi, ni kitu ambacho kinatokea sasa, kwa wakati uliopo, lakini pia hiyo hutokea kwa wakati ujao.

Kifungu 7 inasema, ‘tunao ukombozi kwa njia ya damu yake’ na kifungu 14 inasema ahadi ya Roho Mtakatifu ni, ‘kuweka uhakika wa urithi wetu mpaka ukombozi kwa wale ambao ni milki ya Mungu’.

Hii ina maana kuwa kama Wakristo tunapata ujuzi wa ukombozi sasa lakini kuna ya zaidi inakuja! Sisi ni mali ya Mungu mara tu tunapopokea zawadi yake ya maisha mpya, lakini kuna pia hatua inayoendelea ambayo tunafikia kufanana naye zaidi na kuwa wake kabisa.

Barua ya Paulo kwa waefeso inaonekana kuwa ni barua jumla kwa makanisa yote, ikiwatia moyo wao kuwa, kama wafuasi wa Yesu, wao sasa ni viumbe vipya vya Mungu (Sura ya 1-3) na kuwapa changamoto kuishi kama viumbe vipya kwenye dunia hii (Sura 4-

6). Paulo anaanza kwa kuelezea kazi ya Mungu ndani yao ambayo tayari tumeshasoma. Kiini cha mawazo yake ni neno ‘ukombozi’.

Kwenye kifungu cha 7 Paulo anasema, ‘Ndani yake tunao ukombozi kwa njia ya damu yake’. Kutokana na hii tunaweza kuona huo ukombozi unapatikana kwa Yesu Kristo, na siyo kwa mwingine. Damu ya Yesu ilikuwa ndiyo gharama ya ukombozi, malipo ya kukomboa makubwa ililipwa.

Kwenye kifungu hicho Paulo anaeleza kuwa ukombozi wetu inahusisha, ‘msamaha wa dhambi’. Kupitia sadaka ya kifo cha Yesu, dhambi zimeondolewa na kuharibiwa kabisa. Hii ni, ‘kulingana na utajiri wa neema ya Mungu,’ hiyo ni, huruma zake, fadhila ambayo hatujaifanyia kazi. Kama kifungu 4 na 5 inasema, neema hii inatoka kwenye upendo wa Mungu siyo kwa kufanyia kazi.

Kama tulivyosema, kifungu 14 inatuonyesha sisi kuwa iko pia ukombozi kwa siku zijazo: urithi wetu kwenye mbingu mpya na nchi mpya. Roho Mtakatifu, tuliyepewa sasa ni ‘udhibitisho’ wa urithi wetu, na ahadi ya ziada kuja.

10 Dakika

**Maswali**

Kwenye kikundi 3 au 4 jadili maswali yafuatayo:

- Je ‘ukombozi’ maana yake nini?
- Ikiwa Mungu alilipa gharama kwa ajili yako, hiyo inakufanya kujisikiaje?
- 1 Wakorintho 6:19-20: Paulo anasema, ‘Wewe siyo mali yako; ulinunuliwa kwa gharama. Kwa ajili hiyo mheshimu Mungu kwa miili yenu.’ Tunajibuje upendo wa Mungu kwetu?
- Imesemwa kwa hao walio nje na Kristo: “Huyo aliyekupata (Shetani) wewe siyo mali yake, na huyu ambaye wewe ni mali yake (Mungu) hajakupata.” Mtu atahamaje kutoka gizani kuingia nuruni?

10 Dakika

**Maombi**

Ombeni kwa pamoja kwamba Mungu akuwezeshe kuamini juu ya ukombozi wake na kwa wakati ujifunze kuelewa na kuishi nuruni kwa hayo yote aliyofanya kwa ajili yako.

Uwe na muda wa utulivu wa kuomba na mwombe Roho Mtakatifu kukuonyesha maeneo kwenye maisha yako ambayo huamini juu ya ukombozi wa Mungu.

**Kufanya Wiki Hii**

Kila wiki kuna kazi ya nyumbani ya kufanya. Kwa kadri utakavyoweza baada ya kipindi hiki soma Warumi 6:6-7 tena pengine peke yako au na rafiki. Mwombe Mungu alete akili yako rafiki moja au wawili au wana familia ambao kwa sasa ni wafungwa na wanatumikishwa na dhambi. Omba kila siku kwa hao watu 1-2 ili nao wawekwe huru kwa njia ya Yesu Kristo.

**Shahidi**

Je unamfahamu mtu fulani anayepambana na deni au changamoto ambayo hawawezi kukabiliana nayo wenyewe? Kwa nini usitafute namna ya kumsaidia kwa jambo hilo pengine kwa kuwapa fedha kiasi au muda wako kuwasaidia ili kudhihirisha ukombozi wa Mungu kwenye utendaji.

**Kuendelea na Masomo Ambayo siyo Lazima**

Kuna vifungu vingi vya maandiko inayozungumzia juu ya ukombozi wa Mungu. Kama kuna muda au kama kikundi kitapenda kujifunza zaidi nyumbani, hapa kuna mapendekezo zaidi ya kusoma.


Vifungu vya ziada vya kusoma ni:

- Sura iliyopo ya ukombozi: Mako 10:45, Warumi 3:24, 1 Wakorintho 1:30, Wakolosai 1:14, Wagalatia 3:13 na 4:4-5, Waebrania 9:12, 1 Petro 1:18-19.
- Sura ya baadaye ya ukombozi: Waefeso 4:30, Warumi 8:23.

# Kumbukumbu

10

# Tu Wasafi Mbele za Mungu – Uthibitisho



'Kwa hiyo, kwa kuwa tumekwisha kuhesabiwa haki kwa imani, tuna amani na Mungu kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo.'
Warumi 5:1

**Maandalizi**

Unachohitaji kwa kipindi hiki:

- Vipande vichache vya matunda matamu. Ikiwezekana, lete moja kwa kila mtu kwenye kikundi.
- Vyungu vichache vichafu au nguo na baadhi ya vitu ambavyo vitatumika kusafisha kama sabuni na maji.

Uwe na:

- Soma Kipindi cha 5 na 9 tena ili uweze kuwasaidia watu kukumbuka hadithi na kifungu cha kukumbuka?
- Mwambie mtu kwenye kikundi kusoma hadithi?
- Mwambie mtu kwenye kikundi asome kifungu cha Biblia?

**Karibu na Marejesho**

5 Dakika

- Mshukuru kila moja kwa kuja kwenye kwenye kikundi.
- Anza na maombi mafupi.
- Waulize kikundi kama wamefanya ‘Kufanya wiki hii’ na ‘Shahidi’ kazi ya wiki iliyopita.
- Waalike watu washuhudie kitu chochote walichojifunza au kuwa na ujuzi kwa kufanya kazi hizi.

**Lengo**

Lengo la kipindi wiki hii ni kuelewa kuwa tumetakaswa kutoka kwenye dhambi zetu na kufanywa sawa mbele za Mungu (kuthibitishwa) siyo kwa matendo yetu wenyewe lakini ni kwa imani yetu ndania Yesu nay ale aliyofanya kwa ajili yetu pale msalabani. Tunapokuwa wa Mungu, anakuwa na uwezo wa kuendeleza kazi ya kutufanya kufanana zaidi na Yesu.

**Kifungu cha Kukumbuka**

5 Dakika

Soma kifungu cha kukumbuka na nukuu za Biblia kwa sauti kwenye kikundi. Rudia kusoma tena kwa vifungu vidogo, waachie kikundi kurudia kila sehemu baada yako. Polepole soma tena kwa sehemu ndefu huku kikundi kikirudia kiła neno mpaka kiła moja atakapoweza kukariri kifungu chote. Watie baadhi watu moyo kujaribu na kurudia wao wenyewe.

*Kwa hiyo, kwa kuwa tumekwisha kuhesabiwa haki kwa imani, tuna amani na Mungu kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo.*

*Warumi 5:1*

**Hadithi**

Wasomee kikundi hadithi inayofuata:

Hapo mwanzo alikuwepo Mfalme mwenye nguvu aliyempenda Mungu. Aliishi ndani ya ikulu nzuri sana. Kwenye mji wa Mfalme, kulikuwepo na muombaji mchafu aliyeishi mabarabarani. Watu wa mji mara nyingi wamekuwa wakimpigia kelele, wakimwita majina mabaya na kumpiga. Watu walichukia kumwona. Huyu muombaji alichoka kudhalilishwa hivyo akajifikiria mwenyewe, 'Nitaenda kuonana na Mfalme, na kumwomba anihurumie. Nitamwomba Mfalme ruhusa ya kuomba barabarani na pengine watu wataacha kunidhalilisha.'

Muombaji akaenda kwa Mfalme kuomba huruma ili aweze kuruhusiwa kuomba barabarani. Alivaa nguo zilizochafuka, hakuwa na viatu, alifunikwa na uchafu na alinuka vibaya. Muombaji alijua kuwa alinuka vibaya na kwamba Mfalme anaweza kumwangalia akakirihishwa.

Mfalme alikuwa na kijana, ambaye pia alimpenda Mungu. Kijana wa Mfame, mwana wa Mfalme, akamwona huyo muombaji mchafu akikaribia ikulu. Akamuuliza, 'Unafanya nini hapa?'

Muombaji akajieleza kuwa alikuwa akienda kumwona Mfalme kumwomba amhurumie, ili aweze kuomba barabarani bila kudhalilishwa na mtu yeyote. Mwana wa Mfalme akamjibu, 'Wewe hustahili kuonekana mbele ya Mfalme! Wewe ni mchafu na mavazi yako yamechanika!'

Mwana wa Mfalme hakumuuliza kuwa kwa nini alikuwa muombaji. Mwana wa Mfalme akamhurumia. Mwana wa Mfalme akamchukua huyo muombaji ndani ya ikulu, kwenye chumba

chake mwenyewe. Akamwosha huyo muombaji, kuondoa uchafu wote. Alimwosha miguu na kuhudumia majeraha yake. Akanyoa nywele na kumpaka mafuta yenye harufu nzuri. Mwana wa Mfalme, mtoto wa mfalme, akampa muombaji nguo zake mwenyewe. Mwisho wa haya muombaji, alionekana kama mwana wa Mfalme!

Mwana wa Mfalme akampeleka muombaji, ambaye sasa anaonekana kama mwana wa mfalme, kwenye chemba ya Mfalme. Mwana wa mfalme akamkabithi mwombaji kwa baba yake, Mfalme. Mwana wa Mfalme akasema, ‘Mfalme wangu, baba yangu, huyu ni rafiki yangu, ambaye ni kama ndugu yangu. Mhurumie.’

Sasa Mfalme alisikia yale ambayo mwanaye amekuwa akifanya na moyo wake pia ukajaa na huruma na kumpenda muombaji.

Mfalme akasema, ‘Kwa sababu umemleta kwangu kama ndugu yako, mimi pia namwita kaka yako! Mpe chochote kile anachokihitaji.’

Hivyo Mwana wa Mfalme akamfundisha muombaji namna ya kuwa mwana wa mfalme na akamkaribisha kuishi ikulu. Muombaji hakuwahi tena kurudi kuishi mabarabarani.

**Kujifunza Biblia**

Soma Warumi 3:22-26 kwenye kikundi:

> [22]*Haki hii itokayo kwa Mungu hupatikana kwa Yesu Kristo*
> *kwa wote wamwaminio. Kwa maana hapo hakuna tofauti,*
> [23]*kwa kuwa wote wametenda dhambi na kupungukiwa na*
> *utukufu wa Mungu,* [24]*wanahesabiwa haki bure kwa neema*
> *yake kwa njia ya ukombozi ulio katika Kristo Yesu.*
>
> [25]*Yeye ambaye Mungu alimtoa awe dhabihu ya upatanisho*
> *kwa njia ya imani katika damu yake. Alifanya hivi ili*
> *kuonyesha haki yake, kwa sababu kwa ustahimili wake*

*aliziachilia zile dhambi zilizotangulia kufanywa.* [26]*Alifanya hivyo ili kuonyesha haki yake wakati huu, ili yeye awe mwenye haki na mwenye kumhesabia haki yule anayemwamini Yesu.*

Kuna sehemu tatu kwenye kipindi hiki:

1. Tujikumbushe wenyewe kuwa tumepewa haki meble za Mungu, kwa imani.
2. Tujifunze jinsi Yesu alivyotusafisha.
3. Tujifunze jinsi Yesu anavyoendelea kutufanya kuwa safi, na kututengeneza, na kutufanya kufanana naye.

**1. Kwa kujikumbusha wenyewe kuwa tumethibitishwa mbele za Mungu, ni kwa imani tu**

Kwenye Kipindi cha 7 (Ugonjwa unaoua – Dhambi) tunatazama Zaburi 51 na kujifunza kuwa Mungu yuko tayari kusamehe dhambi zetu, hata ingawa hatustahili.

Kwenye Kipindi cha 9 (Sisi ni wa Mungu – Tumekombolewa) tunajifunza kuwa Mungu amelipa gharama ya dhambi zetu kupitia kifo cha Yesu na kufufuka. Tumeokolewa nay eye na kukombolewa.

**Shughuli**

3 Dakika

Waambie kikundi kukariri kifungu cha kukumbuka toka Kipindi 9 (Sisi ni wa Mungu – Ukombozi).

> [7]*Ndani yake tunao ukombozi kwa njia ya damu yake, yaani, msamaha wa dhambi, sawasawa na wingi wa neema yake* [8]*aliyotumiminia kwa wingi, kwa hekima yote na maarifa yote.*
>
> *Waefeso 1:7-8a*

Kifungu hiki kinaonyesha kuwa tuko huru na gharama na matokeo ya dhambi zetu kwa sababu tu ya kifo cha Yesu. Ni kupitia damu yake tumesamehewa dhambi na neema yake ni ya ukarimu sana kwetu; imetolewa bure, imejaa na haibadiliki.

Kazi inayohitajika kutufanya sisi kuwa safi mbele za Mungu na kukubalika kwake, ilifanyika na Yesu msalabani. Yesu kweli alikufa msalabani; ni tukio la kihistoria la kweli. Hakuna kitu kinachoweza kuondoa kazi aliyofanya Yesu siku ile.

Hivyo sehemu yetu, hali yetu, ‘ndani ya Kristo’ ni salama, kwa sababu iliumbwa na Yesu, na siyo sisi.

Hii hali ya kuwa ‘ndani ya Kristo’, imetupa haki na kusafishwa mbele zake ni zawadi kutoka kwa Mungu kwa ajili yetu. Ni zawadi ambayo hatuwezi kuifanyia kazi na hata hatustahili.

Bado Mungu kwenye huruma zake ametupa zawadi hii, kutuwezesha sisi kuwa ‘ndani ya Kristo’. Tunachotakiwa kufanya ni kuikubali. Tunapokea zawadi hii kwa kuamini kuwa ni kweli, na kupokea ndani ya mioyo yetu na fahamu.

Kifungu chetu cha kukumbuka leo, Warumi 5:1, inaeleza hali yetu mpya ‘ndani ya Kristo’.

**Shughuli**
Kama kikundi kurudia leo kifungu cha kukumbuka, Warumi 5:1.

3
Dakika

**2. Kujifunza jinsi Yesu anavyotufanya kuwa safi**
Kuwa mwenye haki mbele za Mungu ina maana kuwa ni kukbaliwa nay eye. Kwa kuwa Mungu ni Mtakatifu (mkamilifu) hawezi kutukubali sisi ndani ya hali ya dhambi. Hata hivyo, anatusafisha kuwa safi kupitia kifo cha Yesu na kufufuka kwake.

Kwa kuweka imani yetu katika Yesu dhambi zetu zinasafishwa na kwa kudhihirisha hili, na kusaidia kuelewa hili, Mungu anatamka kuwa sisi ni wenye haki (kuthibitishwa). Anatupa hali mpya. Anatufanya kuwa safi.

5 Dakika

**Maswali**
Waambie kikundi kwa wote washirikishe yale wanayokumbuka kwenye hadithi ya leo. Mtie moyo kila mtu kushirikisha chochote wanachokumbuka.

Unaweza kuuliza maswali kama:

- Watu waliyokuwa kwenye hadithi ni akina nani?
- Kila mtu alifanya nini au kusema?
- Nini imekustaabisha kwenye hadithi?

Soma kifungu cha Biblia (Warumi 3:22-26) tena.

Kwenye hadithi yetu Mwana wa Mfalme alimsafisha muombaji na kumpeleka kwa baba yake, Mfalme, kama kaka yake. Ingawa Mfalme alifahamu kuwa mtu huyo alikuwa muombaji, alimtazama kama msafi na kama mwana wa mfalme.

Yesu hutufanya sisi kuwa safi ili kwamba tuweze kusimama mbele za Mungu, kama muombaji alivyoweza kusimama mbele ya Mfalme kwenye hadithi. Mungu anatutazama kama wasafi tunapompokea Yesu na Mungu anataka kutusaidia sisi kubaki hivyo.

**3. Kujifunza jinsi Yesu alivyoendelea kutufanya kuwa safi, na kututengeneza, na kutufanya kufanana naye**
Sasa tuko 'ndani ya Kristo' tumefanywa kuwa safi na tunakubalika na Mungu, na bado tuko ni wale watu walioanguka. Bado tunatenda dhambi.

Kwa mfano, 1 Wakorintho 1:26 anatuonya juu ya kutojivuna na hali yetu 'ndani ya Kristo' na kuwadharau wengine kwa sababu ya hayo. Inatukumbusha kuwa na shukrani kwa Mungu kwa yale ambayo amefanya juu yetu:

> *Ndugu zangu, kumbukeni mlivyokuwa mlipoitwa. Kwa kipimo cha kibinadamu, si wengi wenu mliokuwa na hekima.*

> *Si wengi mliokuwa na ushawishi, si wengi mliozaliwa katika jamaa zenye vyeo.*
>
> *1 Wakorintho 1:26*

Habari njema ni kuwa Mungu hatatuacha peke yetu kupambana na dhambi. Mungu yuko kazini ndani yetu kutubadilisha sisi kufanana zaidi na watu wanaostahilihali yetu 'ndani ya Kristo'. Roho Mtakatifu hufanya kazi kutusafisha sisi na kutufanya kufanana na Yesu.

Sasa ni zamu yetu kufanya kuwa hiyo ina maana gani kwetu kwenye maisha yetu ya kila siku. Utaratibu huu wa ku-husiana na Mungu, hutufanya kuwa wapya na wasafi inaitwa utakaso. Ina maana ni ile hali ya kufanya kuwa watakatifu.

Kubaki 'ndani ya Kristo' maana yake ni kuwa na wakati naye kwa maombi na kujifunza, kumsikiliza yeye na kumtii yeye. Ina maana ya kuwa na muda na Wakristo wengine, kuombeana, kujifunza Biblia pamoja na kufanyia upendo mazoezi na kusameheana.

5 Dakika

**Shughuli**

Waulize kikundi kama mtu yeyote anakumbuka hadithi ya tawi ambalo lilikuwa likijaribu kuzaa matunda lenyewe toka Kipindi cha 5 (Matunda ya Roho – Tabia)?

- Wanakumbuka nini kuhusu hadithi?
- Tulijifunza somo gani?

Unasikiliza majibu inayosema kuwa tawi lisingeweza kuzaa matunda lenyewe lakini lilitakiwa kuungamanishwa na mti. Mti uliufanya kuzaa matunda.

Kumbusha kikundi kuwa hadithi hii ni mfano wa picha ya namna Yesu alivyotufanya kuwa safi. Hatuwezi wenyewe kuwa safi; tunapaswa kuwa karibu sana na Yesu, 'ndani ya Kristo' na atafanya kazi ya kutufanya kuwa safi kupitia Roho Mtakatifu anayeishi ndani yetu.

Waambie kikundi kukariri kifungu cha kukumbuka toka Kipindi cha 5.

> *[22]Lakini tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, [23]upole na kiasi. Katika mambo kama haya hakuna sheria.*
>
> *Wagalatia 5:22-23*[9]

Tunapotoa maisha yetu kwa Mungu na kutafuta kuwa karibu na Yesu na kufuata mapenzi yake kwa maisha yetu, basi tutazaa matunda ya ajabu inayozalishwa na Roho Mtakatifu ndani yetu. Watu wengine wataona hayo matunda ndani yetu pia!

10 Dakika

**Shughuli**

Utahitaji kuwa na pipi, vyungu vichafu au nguo chafu, sabuni na maji aliyokuja nayo.

**Shughuli 1 – Tumefanywa kuwa safi mbele za Mungu (kuthibitishwa)**

- Mwambie kila mtu kuwa umewaletea wao pipi au kipande cha tunda.
- Waambie kuwa hawajafanya chochote ili kupata hii, ni zawadi toka kwako.
- Siyo kitu wanachostahili.
- Ni zawadi ya bure uliyotoa wewe.
- Wanachopaswa kufanya ni kunyoosha mikono yao, na kusema aksante na kupokea zawadi inapotoa.
- Sasa mpe kila mtu pipi na uwaeleze kuwa ni mfano wa njia ambayo Mungu anatupa zawadi ya kuwa ‘ndani ya Kristo’.

**Shughuli 2 – Tuko kwenye hatua ku-husiana na Mungu kutufanya kufanana na Yesu zaidi (utakaso)**

Sasa chukua vyungu vichafu au nguo. Chukua sabuni na maji na uwaambie baadhi ya watu wa kujitolea kuja na kuzisafisha.

---

[9] Scripture taken from The Voice™. Copyright © 2008 by Ecclesia Bible Society. Used by permission. All rights reserved.

Baada ya kusafisha hivyo vifaa, waaulize imegharimu nini kuvisafisha.

Unatafuta majibu kama:

- Maji
- Sabuni
- Kitu cha kusugua
- Nguvu
- Muda

Waeleze kuwa hata ingawa tumepewa zawadi bure ya Kristo, na kwamba sasa Mungu anatuona kuwa wasafi, bado anataka kufanya kazi ndani yetu kutufanya watakatifu. Inachukua muda na kazi kwetu sisi ili kuzidi kufanana naye zaidi na Yesu zaidi.

10 Dakika

**Maswali**

Waambie kila mtu kufanya vikundi vidogo 4. Hakikisha kuwa kuna mtu anayefahamu kusoma na Biblia kwenye kila kikundi. Kila kikundi kitazame moja ya vifungu inayofuata na kujibu maswali yaliyotolewa hapa.

- Kikundi 1: Waefeso 4:22-32
  Kifungu hiki kinaonyesha maana ya kutakaswa (kufanywa watakatifu) inavyofanana. Mungu anatuuliza kufanya nini kwenye hiki kifungu?
- Kikundi 2: Waefeso 4:11-16
  Ishara za Mkristo aliyekomaa ni zipi? Mungu anasababishaje kukomaa? Umeonaje kukua ikitokea kwenye maisha yako?
- Kikundi 3: 1 Wakorintho 15:50-55
  Kifungu hiki kinatupa ahadi gani? Tunaweza kuwa na uhakika na nini?
- Kikundi 4: 1 Yohana 3:2
  Kifungu hiki kinatupa ahadi gani? Tunaweza kuwa na uhakika na nini?

Kipatie kikundi dakika 5 kutazama kifungu chao halafu waulize wote kushirikisha kikundi chote walichojifunza kwa dakika 1.

10 Dakika

**Maombi**
Sasa wageukie waoshe kila mtu mikono kama ishara kuwa makosa yote tuliyofanya zimeoshwa na kuwa safi kwa Yesu kufa na kufufuka kutoka kwa wafu kwa ajili yetu. Tamka kweli hii kwa kila moja na kuomba maombi ya baraka kwamba Mungu aendelee kumfanya kila moja kufanana na Yesu.

**Kufanya Wiki Hii**
Kila wiki kuna kazi ya nyumbani ya kufanya.

Unapofua nguo zako na kuwa safi, jikumbushe kuwa hivi ndivyo Mungu anavyokutazama.

Mwombe Mungu akuonyeshe ni nani unatakiwa kumsamehe, na uwasamehe. Sema kwa sauti, ‘Nimewasamehe.’

Mshukuru Mungu kwa kukuosha na kuwa safi kutoka kwenye dhambi zako zote kila mara utaoshwa, oga au ujioshe. Kumbuka kuwa huna alama yeyote mbele za Mungu.

**Shahidi**
Unapozungumza na marafiki au watu unaoonana kwa siku, mwambie mtu moja kuwa kwa nini wewe ni Mkristo na maana ya kuwa Mkristo ni nini sasa umeoshwa na huna alama yeyote mbele za Mungu. Uwe na uhakika kumweleza kuwa siyo kwa sababu wewe ni bora kuliko wengine lakini ni kwa sababu ya yale Yesu alifanya.


Kama umemsamehe mtu fulani mwombe Mungu kama sasa unaweza kwenda na kuzungumza nao. Kama unafikiri anakuagiza hivyo basi, ikiwezekana, nenda ufanye hivyo.

Kama unasikia ujasiri wowote unaweza kujitoa kusafisha nguo au nyumba ya rafiki, au okota takataka kwenye nyumba ya jirani. Ikiwa mtu atakuuliza kwa nini unafanya hivi waambie ni kwa sababu Yesu amekufanya kuwa safi.

# Kumbukumbu

11

# Kuchukuliwa kwenye Familia ya Mungu



'Kwa maana ninyi nyote mmekuwa watoto wa Mungu katika Kristo Yesu kwa njia ya imani.'
Wagalatia 3:26

**Maandalizi**

Uwe na:

- Mwambie mtu kwenye kikundi kusoma hadithi?
- Mwambie mtu kwenye kikundi asome kifungu cha Biblia?
- Ukitazama nyuma kipindi cha 1 – 2 ujikumbushe mwenyewe yale tuliyojifunza juu ya Roho Mtakatifu?

**Karibu na Marejesho**

5 Dakika

- Mshukuru kila moja kwa kuja kwenye kwenye kikundi.
- Anza na maombi mafupi.
- Waulize kikundi kama wamefanya 'Kufanya wiki hii' na 'Shahidi' kazi ya wiki iliyopita.
- Waalike watu washuhudie kitu chochote walichojifunza au kuwa na ujuzi kwa kufanya kazi hizi.

**Lengo**

Lengo la kipindi wiki hii is kuelewa kuwa tumechukuliwa na kuwa familia ya Mungu. Tunamwita yeye Abba, Baba yetu. Sisi ni kaka na dada wa Yesu na kwa wengine. Tuko kwenye biashara ya familia.

**Kifungu cha Kukumbuka**

5 Dakika

Soma kifungu cha kukumbuka na marejeo ya Biblia kwa sauti kwenye kikundi. Rudia kusoma tena ukiacha kikundi kurudia baada yako mpaka kila mtu aweze kukariri kifungu chote. Watie baadhi ya watu moyo kujaribu kurudia wao wenyewe.

> *Kwa maana ninyi nyote mmekuwa watoto wa Mungu katika Kristo Yesu kwa njia ya imani.*
>
> *Wagalatia 3:26*

**Hadithi**

Wasomee kikundi hadithi inayofuata:

Kulikuwa na kijana mdogo aliyeitwa Ben. Mama yake Ben aliondoka wakati alipokuwa mdogo na alipokuwa kijana Ben aligundua kuwa mtu ambaye alidhani ni baba yake alikuwa ni

baba wa kufikia. Kwenye maisha yake yote ya utoto Ben alizungukwa na mambo mabaya mengi. Baba yake wa kufikia alizoeya kunywa sana, akitumia madawa ya kulevya na kucheza kamari. Ben aliondolewa shuleni na kulazimishwa kuwa na kazi ya kupata pesa kwa ajili ya kutunza familia.

Alipokuwa mtu mzima, Ben akaanza kuuliza kuwa kwa namna mambo yalivyotokeaa kwenye familia yake yalikuwa mazuri au hapana. Ben alipofikisha umri wa miaka 16 baba yake wa kufikia alimwambia aondoke nyumbani kama hakupenda hali jinsi ilvyokuwa. Ben aliamua kuondoka.

Ben alifaulu kupata kazi na sehemu ya kuishi. Ilikuwa ni vigumu kwa sababu hakuna mtu aliyemfundisha namna ya kutunza nyumba au kunza fedha zake. Alianza kujenga maisha yake mapya lakini aliona kuna kitu kimepungua.

Ben akakumbuka kuwa kuna mtu alimwalika kanisani miaka 3 iliyopita. Alijiuliza kama alichelewa kuchukua mwaliko, lakini aliamua kwenda kanisani na kuona. Familia kwenye kanisa ilimwalika na kuanza kumfahamu kidogo. Muda ulipoenda waliendela kumfahamu na kujua kuwa yuko mwenyewe na anapambana. Walianza kumkaribisha kwenye nyumba yao na kumhusisha kwenye familia yao.

Baada ya muda, familia ilimuuliza Ben kama angependa kuwa moja wa familia yao, kuhamia kwao na hata kubadilisha ubin kuwa wao. Ben alikubali na sasa ni mwana familia.

Familia yake mpya ilimwonyesha Ben njia tofauti na ile aliyolelewa nayo. Walipendana na kujaliana. Kama hawakubaliani kwa wao kwa wao, watafanya kazi kwa bidii kuelewana na kusameheana.

Mara zote haikuwa rahisi kwa Ben au familia yake mpya. Familia yake ilikuwa na sheria ambayo Ben alitakiwa kujifunza kuishi nayo na alipaswa kukubaliana na mamlaka ya wazaazi wake wapya.

Mara nyingine aliwaumiza kwa matendo au kwa kutowajibika. Wakati mwingine familia yake ilimchanganya. Alijifunza kusema samahani, ili kusamehewa au kusamehe. Muda ulipopita alianza kufahamu kuwa upendo wa familia yake mpya haukuwa wa masharti. Haikujalisha kama alikuwa mzuri au mbaya, zaidi walimpenda kwa sababu alikuwa motto wao.

Ben alitazama namna familia yake hii mpya ilivyofanya vitu na akajifunza kutoka kwao. Leo, Ben amefanana kabisa na familia yake mpya ingawa hakuzaliwa kwenye familia hiyo. Wanashikiana vilivyo vya dhamani, imani na tabia. Ben anao uhakika wa sehemu yake kwenye familia na anajua anapendwa sawa na watoto waliozaliwa kwenye familia hiyo.

**Kujifunza Biblia**
Soma Warumi 8:14-17 kwenye kikundi:

> 14*Kwa kuwa wote wanaoongozwa na Roho wa Mungu, hao*
> *ndio watoto wa Mungu.* 15*Kwa maana hamkupokea roho ya*
> *utumwa iwaleteayo tena hofu, bali mlipokea roho ya*
> *kufanywa wana, ambaye kwa yeye twalia, "Abba, yaani,*
> *Baba,"* 16*Roho mwenyewe hushuhudia pamoja na roho zetu*
> *ya kwamba sisi tu watoto wa Mungu.* 17*Hivyo, ikiwa sisi ni*
> *watoto, basi tu warithi, warithi wa Mungu, warithio pamoja*
> *na Kristo, naam, tukiteswa pamoja naye tupate pia*
> *kutukuzwa pamoja naye.*

Kwenye vipindi viwili vilivyopita tumeelewa kuwa tumekombolewa (kununuliwa upya na Mungu) na kusafishwa kwa yale Yesu alifanya juu yetu. Tunayo mwanzo mpya na maisha mapya.

Haishii hapo pia. Tunayo pia hali mpya. Kifungu chetu leo kinatueleza kuwa, 'Roho mliyompokea imeleta kuchukuliwa kwenu kuwa wana. Na kwa Yeye tunalia, "Abba, yaani Baba."' Kuna maana nyingi iliyowekwa kwenye maneno machache pale, hivyo tunaenda kutazama kwa pamoja kwenye kifungu cha 4.

**‘Roho mliyompokea’**
Tunapofanyika Wakristo, Mungu hutujaza na Roho wake Mtakatifu. Tumejifunza juu ya Roho Mtakatifu kwenye vipindi vilivyopita.

5 Dakika

**Maswali**
Waulize kikundi nini wanachokumbuka juu ya Roho Mtakatifu. Mpe kila mtu nafasi kushirikisha kitu chochote.

(Inaweza kuwa ni wazo zuri kutazama kipindi cha 1 hadi 2 ya kitabu hiki unapojiandaa kwa mafundisho haya ili uweze kuwasaidia watu kama wanapambana kukumbuka.)

**‘kuletwa karibu na kuwa mwana’**
Kifungu hiki kinasema Roho tunayempokea imetuleta karibu na kuwa wana.

Kumchukua mtoto maana yake ni uhalali wa kumwingiza utaratibu wa wazazi kwa huyo mtoto. Mtoto aliyechukuliwa anakuwa na haki sawa kama mtoto aliyezaliwa na wazazi hao. Wazazi wapya hawawezi kubadili mawazo na kusema, “Hatukuhitaji tena.” Hakuna kitu mtoto atafanya au kusema itawafanya wao kupunguza dhamani ya kuwa mwana wa familia yao. Kuchukuliwa kabisa, mabadiliko ya hali halali.

Hivyo ndivyo ilivyo kwetu. Tunapofanyika Wakristo na kupokea maisha yetu mapya tunaingizwa kwenye familia ya Mungu. Tumetakaswa na kuwa safi mbele za Mungu kwa yale ambayo Yesu amefanya kwa ajili yetu. Tumejazwa na Roho Mtakatifu na kufanyika moja wa watoto wa Mungu, sehemu ya familia yake. Mungu hatabadilisha mawazo yake hata kwa chochote tutakachofanya haitatupunguzia kuwa mtoto. Sisi ni sehemu ya familia yake.

Kitu cha muhimu kutambua ni kwamba mtoto aliyechukuliwa alikuwa na maisha mengine kabla na baada ya kuchukuliwa. Unamkumbuka Ben kwenye hadithi yetu? Alikuwa na familia

kabla ya kuridhiwa. Alijifunza njia ya maisha kutoka kwao ingawa ameanza kuuliza kama ni vizuri. Baada ya Ben kuchukuliwa kwenye familia yake mpya maisha yake na vitu alivyovijifunza vilibadilika. Leo Ben ni mtu tofauti na mtu ambaye angekuwa kama asingecchukuliwa.

Hivyo ndivyo inavyokuwa kwetu tunapofanyika Wakristo. Kwa muda tumebeba ndani yetu tabia na muundo kwa maisha yaliyopita, sasa sisi ni sehemu ya familia mpya, familia ya Mungu, tunayo maisha mapya. Kwa nyakati, tumekuwa watu wa tofauti sana kwa watu ambao tungekuwa hivyo kama tusingechukuliwa kwenye familia ya Mungu. Kuna vitu vimebadilika ghafla, vingine vinabadilika polepole namna Roho Mtakatifu anavyofanya kazi ndani yetu kutufanya kubadilika na kufanana na Yesu na tunajifunza toka kwa washirika wengine wa familia yetu mpya.

**Maswali**

5 Dakika

Kwenye kikundi cha 3 au 4 mjadili maswali yafuatayo:

- Kuchukuliwa maana yake nini?
- Kuchukuliwa maana yake nini kwa mtoto aliyechukuliwa?
- Ina maana gani kwetu sisi kuchukuliwa kwenye familia ya Mungu?

**‘kuwa mwana’**

Pointi ya kutusaidia kuelewa ni kwamba wakati Biblia imeandikwa, wana walionekana kuwa bora zaidi ya mabinti. Waliweza kurithi utajiri wa familia na kubeba jina la familia mbele. Kuwa mwana ni kuwa na hali kubwa. Nyakati hizo mabinti hawakuwa na hali sawa na wana.

Wakati kifungu kinasema tumepewa uwana, haina maana kuwa wanaume tu ndiyo wanaopaswa kupokea hii. Haina maana kuwa wanawake hawadhaminiwi. Hii ina maana kuwa watu wote, wanaume na wanawake, wanaweza kupewa hali kubwa inayowezekana kwenye familia ya Mungu ambayo, wakati Biblia ilipoandikwa, alikuwa ni mwana. Hii ina maana kuwa kupitia

kuchukuliwa kwenye familia ya Mungu, tumepewa hali mpya, hali ya juu. Tunafanyika warithi wake. Tunalibeba jina lake.

Hii ni heshima kubwa. Tunapata faida zote kwa kuwepo kwenye familia: Baba anayetupenda anayetuangalia sisi kwa ulinzi wa baba na upendo na upendo na kujaliwa na mama (angalia Matayo 6:26, Isaya 66:13, na Matayo 23:37). Tunawapata pia ndugu wengi wapya wa kiume na wa kike – na hao wote wanaomwamini Yesu na wamempokea Roho Mtakatifu.

Kama tu vile Ben kwenye hadithi yetu, wakati mwingine tunagundua kuwa ni ngumu kuwa sehemu ya familia. Tunaweza kupambana kuishi namna familia mpya inavyotaka; tunaweza kuumizwa na watu wengine ndani ya familia. Kama Ben, tanapaswa kujifunza kusema samahani kwa Mungu na kwa kila moja, kusamehewa na kusamehe.

**‘na kwake yeye tunalia, “Abba, Baba.”’**
Neno ‘Abba’ ni neno la Kiaramaik (hii ni lugha iliyozungumzwa wakati wa Yesu). Mara ya kwanza ilinakiliwa ndani ya Biblia wakati Yesu alipokuwa akiomba, kabla hajasalitiwa na kuuwawa. (Unaweza kusoma maombi yake kwenye kitabu cha Marko 14:32-42.) Yesu alimlilia Mungu kama baba yake, dadi wake. Ilikuwa ni maombi ya ndani sana ya moyo wake.

Neno hilo limerudiwa tena mara mbili ndani ya Biblia, ndani ya kifungu tulichokisoma leo (Warumi 8:15) na pia kwa Wagalatia 4:6. Kwenye sehemu hizi mbili, Biblia inasema kuwa ni Roho Mtakatifu ndani yetu anayetupa uwezo kulia ‘Abba, Baba’ – Dadi. Tunaweza kumlilia Mungu ndai kabisa ya mioyo yetu, tukifahamu kuwa anatujali kwa sababu tuu watoto wake.



10
Dakika

**Shughuli**
Shughuli hii itafunua maana ya kuwa sehemu ya familia.

- Moja baada ya mwingine, mwambie kila mtu kushuhudia njia moja ambayo wako kama mama yao au baba au njia nyingine kwamba mtoto wao ni kama wao.
- Kinachofuata, mwambie kila mtu kushuhudia kitu kimoja ambayo ni cha muhimu sana kwenye familia yao. Hii inaweza kuwa kitu wanachokifanya, mtazamo ama imani wanayoshikilia au utani wote wanaujua!

Mara kila moja atakapokuwa amejibu unapaswa kuonyesha kuwa baadhi ya majibu yanaonyesha namna tulivyozaliwa (labda wote tunafanana) na wengine wafanye yale tuliyojifunza (tabia zetu na dhamani). Unaweza kukumbusha kikundi kuwa tunapofanyika familia ya Mungu Roho Mtakatifu anayeishi ndani yetu atatusaidia kuwa, kutazama, na kuonekana zaidi kuwa wana familia.

Waulize kama kila moja kwenye chumba aliyemchukua mtoto ama alichukuliwa angependa kushuhudia sehemu ya hadithi yao. Ni muhimu kutomfanya mtu yeyote kujisikia vibaya au chini presha, hivyo waambie watu hao ni wale tu wanaopenda kushuhudia kwa hiari.



15
Dakika

**Maombi**
Mkumbushe kila moja kuwa sote tu familia moja, hivyo ni vizuri kuw pamoja na kuzungumza na baba yetu wa mbinguni kwa pamoja.

**Kujiunga na familia**
Kwanza uliza kama kuna moja ambaye hajafanyika sehemu ya familia na angependa kufanya hivyo leo. Kama hakuna mtu anayejibu, unaweza kusonga mbele kwenye maombi mengine (Kusalimia familia). Ikiwa kuna mtu ambaye angependa kujiunga na familia leo, unaweza kuwaongoza kwenye maombi sasa. Waulize watu 2 wanaokaa karibu nao kuwawekea mikono kama ishara kwao kukaribishwa kwenye familia, halafu uwaambie warudie maombi haya, mstari 1 kwa wakati, baada yako.

*Baba, aksante kwa kumtuma mwanao Yesu kufa kwa ajili yangu ili niweze kuingizwa kwenye familia yako.*
*Leo nataka kuwa sehemu ya familia yako.*
*Nageuka kuacha maisha yangu ya zamani na kukuomba umtume Roho Mtakatifu aje kuishi ndani yangu ili nifanyike mwanao, unisaidie mimi kufanana zaidi na wewe.*
*Amina.*

Waambie kila mtu kushangilia baada ya kumaliza maombi kumkaribisha mwanachama mpya kwenye familia!

**Kusalimia familia**
Sasa tutaenda kuwasalimia kaka na dada zetu kwenye familia ya Mungu – kila moja – na mshukuru Mungu kwa kila moja. Eleza kuwa ikiwa mtu alikuwa hana makubaliana na mwenzake kwenye kikundi sasa, ni wakati mzuri kusema nisamehe kwa huyo mtu na kusameana.

Mwambie kila moja wapeane mikono kwa watu wengi kwenye chumba kwa kadri watakavyoweza, na kumshukuru Mungu kwa sauti kwa kila mtu wanapofanya hivyo. Ruhusu kama dakika 5 kwa watu kufanya hivyo halafu warudishe wote wawe pamoja.

**Kuongea na Baba yetu**
Mwambie kila moja kusimama kwenye mduara na kushikana mikono na waeleze kuwa wote waombe kwa sauti kwa wakati moja. Mwambie kila moja atumie maneno yake kumshukuru Mungu kuwachukua kwenye familia yake. Kama kuna kitu chochote wanachohitaji kusema samani kwa Mungu, sasa ni wakati mzuri wa wao kufanya hivyo. Wamwombe Mungu kuendelea kuwafanya wafanane naye kwa njia ya Roho Mtakatifu.

**Kufanya Wiki Hii**
Kila wiki kuna kazi ya nyumbani ya kufanya.

Wiki hii sisi sote tutaenda kuwaalika wengine kwenye nyumba zetu na kushiriki chakula cha pamoja.

Nusu ya kikundi wanapaswa kukaribisha na nusu ya kikundi wanapaswa kutembelea! Hakikisha hakuna mtu anayeachwa nyuma, na kila mtu aidha anakuwa na mgeni anayekuja ama mahali pa kutembelea. Watu wanaweza kuweka mipango wanayokubaliana nayo.

Chakula ni sehemu muhimu kwa familia na nafasi nzuri kufikiri juu ya maana ya kuwa sehemu ya familia. Mtakapokutana tena, Unapaswa kumuuliza kila moja maswali yafuatayo:

- Ina maana gani kuchukuliwa na kuingizwa kwenye familia ya Mungu?
- Tutawakaribishaje watu kwenye familia zetu za nyumbani na kwenye familia ya Mungu?



**Shahidi**

Kwa njia hiyo ambayo Mungu anatuchua kwenye familia yake, tunaweza kuwakaribisha wengine kwenye familia zetu, kama familia ya Ben ilivyofanya. Kuchukuliwa ni ushahidi wa jambo la ajabu hivyo wote wanaochukulia kwenye familia na hao wanaotuzunguka.

Kuchukuliwa kwenye familia nyingine siyo kitu cha kufanyika haraka au kwa wepesi. Wiki hii tumia muda kufanya uchunguzi kumtafuta mtu aliyo chukuliwa kwenye familia nyingine na kuomba kama unaweza kuchukua watoto kwenye familia yako ama usaidie familia wanamchukua mtoto kwenye familia yao.

12

# Uwe Mwenye Huruma kwa Wengine



'Njooni kwangu, ninyi nyote mnaotaabika na kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha. Jifungeni nira yangu, mjifunze kutoka kwangu, kwa maana mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo, nanyi mtapata raha nafsini mwenu. Kwa maana nira yangu ni laini na mzigo wangu ni mwepesi.'

Matayo 3:11

**Maandalizi**

Uwe na:

- Mwambie mtu kwenye kikundi kusoma hadithi?
- Mwambie mtu kwenye kikundi asome kifungu cha Biblia?

**Karibu na Marejesho**

5 Dakika

- Mshukuru kila moja kwa kuja kwenye kwenye kikundi.
- Anza na maombi mafupi.
- Waulize kikundi kama wamefanya ‘Kufanya wiki hii’ na ‘Shahidi’ kazi ya wiki iliyopita.
- Waalike watu washuhudie kitu chochote walichojifunza au kuwa na ujuzi kwa kufanya kazi hizi.

**Lengo**

Lengo la kipindi wiki hii ni kujifunza kuwa msamaha wetu ni matokeo ya huruma na Mungu kwetu. Tunapokuwa kwenye maisha yetu mapya siyo tu kwamba tunajisikia tu kuwa na huruma, lakini ni kudhirisha kwa matendo pia.

**Kifungu cha Kukumbuka**

5 Dakika

Soma kifungu cha kukumbuka na nukuu za Biblia kwa sauti kwenye kikundi. Rudia kusoma tena kwa vifungu vidogo, waachie kikundi kurudia kila sehemu baada yako. Polepole soma tena kwa sehemu ndefu huku kikundi kikirudia kiła neno mpaka kiła moja atakapoweza kukariri kifungu chote. Watie baadhi watu moyo kujaribu na kurudia wao wenyewe.

> *28“Njooni kwangu, ninyi nyote mnaotaabika na kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha. 29Jifungeni nira yangu, mjifunze kutoka kwangu, kwa maana mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo, nanyi mtapata raha nafsini mwenu.*
> *30Kwa maana nira yangu ni laini na mzigo wangu ni mwepesi.”*
>
> *Matayo 11:28-30*

**Hadithi**

Wasomee kikundi hadithi inayofuata:

Kwenye kijiji kinachoitwa Katubu aliishi kijana anayeitwa Jack. Jack aliishi na wazazi wake waliofanya kazi ngumu na wakajitahidi kuhakikisha kuwa siku zote wanayo chakula kwa ajili ya Jack na ndugu zake na dada kwa ajili ya kula.

Jack alikuwa rafiki wa Bright walioishi karibu. Alijua maisha ni magumu kwa Bright kwa sababu mama yake alifariki wakati Bright alikuwa mdogo bado. Baba yake Bright pia alifanya kazi kwa bidii, lakini akipambana kuangalia familia na kuwahudumia. Bright alitumia muda mwingi akichota maji, akiandaa chakula na kuwaangalia mdogo wake na dada yake.

Jioni moja wakati Jack alipokuwa akila chakula chake cha jioni na familia yake, alitambua kuwa Bright alikuwa amekaa juu ya ngazi mbela ya mlango wao akiwatazama.

Jambo hilo likatokea na siku ya pili.

Jack akatambua kuwa hili ni jambo la ajabu kwa sababu Bright kwa kawaida hushughulika kuandaa na kula chakula muda huo ambao nao wanakula.

Jack akaenda kuongea na Bright na kugundua kuwa baba yake Bright alikuwa mgonjwa sana hivyo hakuweza kwenda kazini, apate pesa anunue chakula. Familia iliishiwa chakula na wote walikuwa na njaa.

Jack alijisikia huzuni juu ya jambo hili akamtuliza Bright kwa kadri alivyoweza. Bright alitabasamu na kusema aksante na Jack akaenda nyumbani.

Asubuhi ya pili familia ya Jack walikaa chini ili wanywe kifungua kinywa na Jack akamkumbuka Bright na akawaza jinsi alivyo na njaa asubuhi hii. Alimwomba mama yake na baba kama wangeweza kushirki kifungua kinywa na Bright pamoja na familia yake, akiwaeleza kuwa hawakuwa na chakula wiki hii.

Familia ya Jack ikakubali na kumwalika Bright na ndugu yake na dada kujiunga nao kwenye kifungua kinywa. Walichukua pia bakuli la uji kumpelekea baba yake Bright aliyekuwa bado mgonjwa.

Familia ya Jack waliendelea kushiriki chakula na familia ya akina Bright kwa zaidi ya wiki 2 mpaka baba yake Bright akapona tena na kuweza kurudi kazini.

Familia ya akina Jack walipungukiwa na chakula wiki hiyo na wakaanza kusikia njaa, lakini kwa vile walikuwa na huruma kwa familia ya akina Bright wasingeweza kuwaacha bila chakula.

Kuanzia wakati huo, familia ya Bright na Jack wakawa marafiki wa karibu na kusaidiana kwa njia nyingi.

10 Dakika

**Shughuli**

Gawanya kikundi kwa 2 vikundi vidogo na kukiambia kila kikundi kuandaa mchezo wa kuigiza ambayo itaelezea hadithi ambayo tumesoma.

Mtu anaweza kuigiza kama Jack na mwingine kama Bright. Wengine wanaweza kuwa familia zao.

Ruhusu dakika 5 kwa kila kikundi kujiandaa, ukiwatia moyo kusaidia kuonyesha huruma inaweza kuonekana namna gani.

Baada ya dakika 5, waambie kila kikundi kuigiza sehemu zao kwenye hadithi kwa kikundi kingine.

Mpe kila moja mzunguko wa kupiga makofi.

5 Dakika

**Maswali**

Waambie kikundi nini wanachofikiri hadithi hii inatufundisha nini. Ruhusu muda watu wachangie mawazo yao.

**Kujifunza Biblia**
Soma Marko 6:30-34 kwenye kikundi:

> [30]*Wale mitume wakakusanyika kwa Yesu na kumpa taarifa*
> *ya mambo yote waliyokuwa wamefanya na kufundisha.*
> [31]*Basi kwa kuwa watu wengi mno walikuwa wakija na*
> *kutoka, hata wakawa hawana nafasi ya kula, Yesu*
> *akawaambia wanafunzi wake, "Twendeni peke yetu mahali*
> *pa faragha, mpate kupumzika."*
>
> [32]*Hivyo wakaondoka kwa mashua peke yao, wakaenda*
> *mahali pasipo na watu.* [33]*Lakini watu wengi waliowaona*
> *wakiondoka, wakawatambua, nao wakaenda haraka kwa*
> *miguu kutoka miji yote, nao wakatangulia kufika.* [34]*Yesu*
> *alipofika kando ya bahari, aliona makutano makubwa ya*
> *watu, akawahurumia kwa maana walikuwa kama kondoo*
> *wasiokuwa na mchungaji. Kwa hiyo akaanza kuwafundisha*
> *mambo mengi.*

Kwenye hadithi hii kwenye maisha ya Yesu tunasikia kuwa yeye na mitume wake walitafuta sehemu tulivu pa kupumzika. Pamoja na hayo Yesu alipoona kikundi kikubwa kikimfuata aliwahurumia na kuanza kuwafundisha. Angaliweza kuchagua kupuuza mahitaji ya makutano lakini badala yake alichagua kuweka mahitaji yao mbele ya za kwake.

Msikio huu wa huruma Yesu aliyokuwa nayo ikamsukuma kufanya kitofauti. Ikampa kuona kitu ambacho hakuwa anakiona kabla; alianza kuwaelewa watu kwa ubora zaidi. Kifungu kinaelekeza mkutano wa watu kama kondoo na kwa Yesu kuwa mchungaji. Kama mchungaji, Yesu angewafundisha watu walichohitaji kujua na kuwaweka wasikaye mbali na Mungu. Aliwasaidia kukwepa hatari na kuwafundisha juu ya Ufalme wa Mungu, na maisha mapya ambaye alikuwa anawapa.

Ingawa huruma huanza kama kujisikia, Yesu anaeleza namna hiyo ya kujisikia inavyogeuka na kuwa kwenye hali ya matendo. Wakati

anawaona watu wakipambana, kuteseka au kuwa kwenye shida huruma anayosikia kwa ajili yao itamwongoza yeye kuwasaidia wao. Katika kila hali msaada ni tofauti na inahusiana na mahitaji yanayotambulikana.

Hapa kuna hadithi nyingine tatu inayoonyesha huruma za Yesu:

- Yesu aliona mkutano mkubwa ukimngoja yeye na kwa matokeo ya huruma aliyokuwa nayo juu yao aliwaponya hao waliokuwa wagonjwa kati yao (Matayo 14:14).
- Yesu amekuwa akifundisha mkutano mwingine kwa siku tatu akatambua kuwa walikuwa na njaa, hivyo akawahurumia akawaagiza mitume kutafuta chakula kwa ajili yao. Kwa muujiza aliongeza kile chakula hivyo hakuna mtu aliyerudi nyumbani akiwa na njaa (Matayo 15:32).
- Yesu alikuwa akisafiri wakati vipofu wawili walipompigia kelele. Akawauliza walikuwa wanataka nini wakamjibu tunataka kuona. Kwa sababu aliwahurumia aliwaponya wakaona (Matayo 20:34).

Kwenye hadithi yetu leo, Jack aliona kuwa familia ya akina Bright hawakuwa na chakula akawahurumia. Huruma hii ikamfikisha sehemu ya kuchukua hatua, akiwatia moyo familia yao kushiriki chakula walichokuwa nacho na familia ya akina Bright na akawa na muda nao wote. Kwa kuwapatia chakula na kuwa na muda nao Jack na familia yao pia walipokea vingi zaidi toka kwa familia ya akina Bright kuwa sehemu ya urafiki. Jack hakumpuuza Bright, wala kumlaumu au kutazama chini kwa sababu ya mapambano. Badala yake alimpa kile alichoweza na kushiriki alichonacho, hata ingawa ina maana kuwa Jack na familia yao walikuwa na njaa wenyewe!

**Huruma ni nini?**

Huruma ni hisia inayoinuka unapoanza kugundua kuwa wako watu wanaoteseka, wenye uchungu na wanapambana. Ni hisia inayoleta motisha uchukue sehemu ya kupunguza yale mateso. Inakubadilisha wewe kama mtu kwa kukusaidia wewe kufahamu wengine jinsi wanvyojisikia; hii inaweza kukumiza unapoingia

kwenye uchungu wao na changamoto. Hata hivyo, pia inatoa mafuta ya kubadilisha ulimwengu unaokuzunguka kwa kufanya kitu kusaidia kupunguza uchungu au changamotoambayo tayari umeshaanza kugundua.

Mungu ni mwenye huruma kwa asili; anaelezewa kuwa:

> *Bwana, Bwana, Mungu mwenye huruma na neema, asiye mwepesi wa hasira, mwingi wa upendo na uaminifu.*
>
> *Kutoka 34:6*

Tunapokua kwenye maisha yetu mapya ili kufanana naye, hivyo huruma yetu inaongezeka.

Mungu huleta huruma kwenye mioyo yetu kupitia Roho wake Mtakatifu; hutupa pia mwelekeo na hamu ya kufanya jambo fulani kwa huruma zetu. Kama Jack na familia yake, hatupaswi kuwa matajiri ili tuwe na huruma. Hatupaswi kuwa na maisha ambayo yote yamerekebishwa na tusiwe na changamoto yetu wenyewe kuwa na huruma. Kila mtu anaweza kujisikia kuwa na huruma kwa mwingine na Mungu atawapa wazo la namna ya kufanya kwa huruma hii.

?

5 Dakika

**Maswali**

Kwenye kikundi ya 2 au 3 mwambie kila mtu kujadili maswali yafuatayo. Baada ya muda mpe kila mtu muda ya kutoa marejesho na kushirikisha mawazo yao.

- Ni lini uliwahi kuwa na huruma au lini uliwahi kuhurumiwa?
- Huruma imeleta tofauti gani kwenye mazingira?

**Utaratibu wa kupalilia huruma**

- Kama unataka wengine wawe na furaha, fanyia mazoezi huruma.
- Kama unataka kuwa na furaha, fanyia mazoezi huruma.

Unaweza kusema kujali juu ya furaha ya mtu mwingine kama ingekuwa ni wewe ni huruma. Yesu alionyesha jambo hili

alipoweka mahitaji ya watu wengine juu zaidi ya mahitaji yake. Alipoulizwa ni amri ipi iliyo kuu, Yesu alifundisha:

> [37]*Yesu akamjibu, "'Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote na kwa roho yako yote na kwa akili zako zote.'*
> [38]*Hii ndiyo amri iliyo kuu, tena ni ya kwanza.* [39]*Nayo ya pili ni kama hiyo, nayo ni hii: 'Mpende jirani yako kama nafsi yako."*
>
> *Matayo 22:37-39*

Kama tunampenda Mungu kwanza na kuwa penda majirani kama tunavyojipenda, hatutashindwa kuwa na huruma kwa hao tunaokuta nao.

**Ufunguo wa kukuza huruma**
Kukuza huruma unatakiwa kuwa ni jambo lako la mazoezi ya kila mara. Tafakari juu yake asubuhi. Unaweza kufanya hivyo wakati uko kwenye kazi yako ya kila siku, unapopalilia shamba au kusafisha nyumba yako. Fikiri juu yake wakati unapokutana na wengine. Lirudie juu yake usiku. Hakuna sababu ya kuwa kanisani uweze kutafakari juu ya huruma – Mungu anaweza kuongea na sisi mahali popote tulipo. Hakuna sababu ya kuwa na filosofia isiyowezekana: utu wema ndiyo filosofia.

Tunapojifunza kukuza huruma tunapaswa kuanza kujihusisha na dunia inayotuzunguka. Huruma haifanyi kazi kwa kufikiria juu yake, tuanatakiwa kuwa karibu ya kutosha kwa watu kuona kinachoendelea kwenye maisha yao na kujihusisha kuwasaidia. Hii italeta changamoto na gharama kwetu lakini itakua tu njia ambayo itakuza kweli huruma.

**Nini maana ya kuwa mwenye huruma?**
Tunaweza tusielewe maana ya kuwa mwenye huruma:

- Ni kutoa fedha kwa watu maskini kupitia mashirika yanayosaidia? Hapana!
- Ni kuwa tu mwenye huruma? Hapana!

- Ni kumwambia mtu mwingine juu ya shida yako na kutegemea kukusaidia? Hapana!

Kwenye maisha yetu ya kila siku, huruma ni kuwa na moyo uliofunguka katika maisha yetu ya kila siku. Hii inamaanisha tuwasikilize tuwapendao na watu wanao tuzunguka. Matayo 13:15 Yesu alifundisha kwenye kifungu katika kitabu cha Isaya 6:9-10 kuhusu umuhimu wa kuona, kusikia na kuelewa kipi kinachoendelea ili tumgeukie Mungu atuponye na atusaidie. Huruma inahusu kuelewa vizuri kabisa tufanye nini na kwa kadri tunavyoweza na kufanya kila tunachoweza ili tuweze kusaidia. Ni kuhusu kuona, kusikia na kuelewa, na kuchukua, hizi hisia kwa Mungu na kuhusu kufanya kazi naye na kusaidia watu na kuleta matumaini na kuwaponya.

Hisia yenyewe haitoshi.

**Maswali**

5 Dakika

Kwenye kikundi watu 2 au 3 rudia tena kuwaambia wajadili maswali haya yafuatayo. Baada ya hapo mpe kila mtu wakati kutoa marejesho na kushuhudia mawazo yao.

- Nini imetuzuiya tusiwe na huruma?
- Tunawezaje kuwa na huruma?
- Huruma inatufanyia nini sisi na jumuia zetu?

Huruma haiwezi kupigiwa hesabu. Inatakiwa uisikie na kushirikisha.

**Maombi**

15 Dakika

Tutaenda kumwomba Mungu kutupa moyo wenye huruma. Mwambie kila moja kuomba wakiwa wawili.

- Jambo la kwanza, watu wanapaswa kumshukuru Mungu vile ni mwenye huruma kwa kila moja wetu.
- Jambo la pili, wanapaswa kumwomba Mungu kuleta kwenye mioyo yao kila wakati ambao wamekosa kuwa na huruma kwa mtu mwingine na kumwomba Mungu msamaha kwa

hilo. Wanaweza pia kuomba nafasi ya kusema nisamehe kwa mtu ikwa ni lazima.

- Linalofuata wamwombe Mungu kuwasaidia wao wajisikie kuwa na huruma kama jinsi Yesu alivyokuwa na huruma na sisi.
- Wanapaswa kumwomba Mungu kuwaonyesha ni nani wa kuhuru-miwa na ni tendo gani watachukua kuwajali watu hawa.

**Kufanya Wiki Hii**

Unajisikiaje unapoona mtu anateseka?

Unafikiri nini juu yako unapofikiri maisha ya watu wengine?

Wiki hii, tutaenda kufanya mazoezi juu ya wito wetu na kuchukua hatua kuwasaidia wengine wanaoteseka.

Kama Mungu amemleta mtu kwenye akili yako wakati tulipokuwa tukiomba huko mbele, ni vema kukumbuka huyo mtu ni nani na kuomba tena. Kama hakuna mtu amekuja kenye akili yako, unapaswa kuendelea kumwomba Mungu ni nani anataka umhurumie kwa wiki hii.

**Shahidi**


Nenda umtembelee mtu huyo ambaye Mungu amemleta kwenye akili yako. Tafuta kufahamu mazingira yao na mwombe Mungu ni nini unaweza kufanya kumsaidia atoke kwenye tatizo alilonalo.

Halafu nenda ufanye kitu kwa ajili yao.

Unapowahudumia na mahitaji yao, waambie juu ya huruma za Mungu na jinsi anavyowajali na maisha mapya ambayo angeleta kwenye hali yao.

13

# Ufupisho wa Kipindi



'Hivyo mwenye kupanda na mwenye kutia maji si kitu, bali Mungu peke yake ambaye huifanya ikue.'
1 Wakorintho 3:7

**Maandalizi**

Unachohitaji kwa kipindi hiki:

- Baadhi ya mbegu na udongo na udongo kwenye chombo ya kuotesha mbegu ndani.

Uwe na:

- Mwambie mtu kwenye kikundi kusoma hadithi?
- Mwambie mtu kwenye kikundi asome kifungu cha Biblia?

**Karibu na Marejesho**

5 Dakika

- Mshukuru kila moja kwa kuja kwenye kwenye kikundi.
- Anza na maombi mafupi.
- Waulize kikundi kama wamefanya ‘Kufanya wiki hii’ na ‘Shahidi’ kazi ya wiki iliyopita.
- Waalike watu washuhudie kitu chochote walichojifunza au kuwa na ujuzi kwa kufanya kazi hizi.

**Lengo**

Lengo la kipindi wiki hii ni kujikumbusha wenyewe juu ya wazo kuu ambalo tayari tumekwisha jifunza kwenye ***Misingi 2: Maisha Hukua***. Tutatazama pia mbele juu ya yale yanayokuja kwenye ***Misingi 3: Maisha Huumba***.

**Kifungu cha Kukumbuka**

5 Dakika

Soma kifungu cha kukumbuka na nukuu za Biblia kwa sauti kwenye kikundi. Rudia kusoma tena kwa vifungu vidogo, waachie kikundi kurudia kila sehemu baada yako. Polepole soma tena kwa sehemu ndefu huku kikundi kikirudia kiła neno mpaka kiła moja atakapoweza kukariri kifungu chote. Watie baadhi watu moyo kujaribu na kurudia wao wenyewe.

> *Hivyo mwenye kupanda na mwenye kutia maji si kitu, bali Mungu peke yake ambaye huifanya ikue.*
>
> *1 Wakorintho 3:7*

**Hadithi**

Mfalme Yosia alitawala taifa la Yuda zaidi ya maka 2500 iliyopita. Alitokea kwenye mtiririko mrefu wa wafalme, wengine wao walikuwa wazuri, na wengine hawakua wazuri. Kilichopendeza kuhusu Yosia ni kwamba alifanyika mfalme akiwa na muri wa miaka 8. Alikuwa ni kijana mdogo tu baba yake alipouwawa akaachwa na wajibu wa kuongoza taifa.

Pamoja na umri wake mdogo, uwezo wa Yosia kutawala ulikuwa na kukuzwa. Alipofikisha umri wa miaka 16 alianza kumtafuta Mungu. Kwenye umri wa miaka 20, alianza kufuata seria za Mungu kuondoa ibada ya sanamu kwenye taifa. Akiwa na umri wa miaka 26, alitumia pesa zilizokusanywa kwenye kodi kurekebisha hekalu na kuwatia watu wake moyo kumwabudu Mungu pia. Wakati time yake walipokwenda kurekebisha hekalu wakapata kurasa za nakala za mwanzoni ya vitabu vichache vya Biblia. Yosia alitaka asomewe kitabu hicho ikabadilisha maisha yake. Kwa kweli, alikuwa akimfuata Mungu kufuata na mila na desturi za babu zake, lakini sasa aligundua maandiko kwa binafsi yake akaanza kumfuata Mungu kwa karibu zaidi. Imani yake ikakua na kuongezeka na akapanga kushuhudia imani kwa wale wote aliowaongoza, akiwapa nafasi ya kumjua Mungu na kumwabudu pia.

Yosia alipouwawa kwenye vita taifa lake lilimlilia kwa muda mrefu, na baadaye wakapelekwa utumwani kwa sababu hawakuwa tena na kiongozi mwenye nguvu mcha Mungu.

(Unaweza ukasoma hadithi hii kwenye Biblia kitabu cha mambo ya 2 Nyakati 34-35.)

**Kujifunza Biblia**

Soma kitabu cha Marko 4:26-29 kwenye kikundi:

> 26 *Pia akawaambia, "Ufalme wa Mungu unafanana na mtu apandaye mbegu shambani.*
> 27 *Akiisha kuzipanda, usiku na mchana, akiwa amelala au ameamka, mbegu huota na*

*kukua pasipo yeye kujua ikuavyo.* [28]*Udongo huifanya iote*
*kuwa mche, halafu suke, kisha nafaka kamili kwenye suke.*
[29]*Lakini nafaka inapokuwa imekomaa, mara mkulima*
*huingia shambani na mundu wa kuvunia, maana mavuno*
*yamekuwa tayari."*

Kwenye mtiririko huu tumekuwa tukijifunza juu ya maisha yetu mapya katika Mungu yanavyokuwa. Kwenye ukrasa wetu wa Biblia na kifungu cha kukumbuka inatuambia, siyo sisi ndiyo tunaojikuza, ni Mungu pekee ndiye mwenye kuweza kufanya hivyo. Kama jinsi mimea inavyokua wakati mbegu imewekwa ardhini, nayo maisha yetu katika Mungu yanakuwa. Kama jinsi Mungu anavyowajibika kwenye kukua, nasi tunawajibika kuhakikisha kuwa hali ya kukua ni jambo la kwanza, au hii inaweza kufanya kukua iwe polepole na kuwa ngumu zaidi.

15 Dakika

**Shughuli**
(Kwenye shughuli hii utahitaji mbegu kiasi na udongo kwenye chombo ambacho unaweza kupanda mbegu ndani yake.)

Ili tuweze kujikumbusha kukua yanayokuja baada ya maisha kuanza tunaenda kupanda baadhi ya mbegu na kutazama cinsi inavyokua kwa wiki inayofuata.

Kila mtu anapaswa kuchukua chombo na kujaza udongo/dunia, baadhi ya mbegu na baadaye uweke maji. Wanaweza kuchukua chombo hicho nyumbani na kuangalia kukua kwa mmea.

Wakati unahudumia mbegu, zitazame zikikua hata ifikie sehemu ya kuliwa au ufurahie kuzitazama kile kitakachozaliwa (kutegemea kile ulichochagua kuotesha), kumbuka kuwa Mungu anakuza kitu kipya ndani yako pia.

**Ukitazama nyuma kwenye Kitabu 2: *Maisha Hukua***
Kwenye kitabu hiki cha pili kwenye mtiririko, ***Maisha Hukua,*** tumetambulisha baadhi ya misingi ambapo imani yetu inakua na kupanuka. Tumetambulisha pia mawazo ya maandiko ambayo

inafunua kuelewa matumizi ya Biblia na maombi ambayo imetusaidia kuelewa na kuingiza kwenye mazoezi maisha mapya ambayo tumekubali.

Kwenye kitabu hiki tumechukua muda zaidi tukitazama kuwa Roho Mtakatifu ni nani na namna alivyokuja kuishi ndani yetu tulipokubali zawadi ya Mungu ya maisha mapya. Anapokuja kuishi ndani yetu, tumeona kuwa anatupa zawadi na pia anafanya kazi kuingiza tabia ya Mungu ndani yetu. Roho Mtakatifu anatusaidia kudhibitisha maisha yetu mapya na pia kukuza maisha yetu mapya.

Tunatazama kwa ukaribu zaidi yale ambayo dhambi hufanya ndani yetu, na namna zawadi ya neema kutoka kwa Mungu ambayo inatolewa bure kwitu inavyoweza rkushinda nguvu ya dhambi kwenye maisha yetu. Tumewekwa huru, kununuliwa upya, kusafishwa na kupewa nafasi kwenye familia mpya kama matokeo ya neema ya Mungu. Hii ilitusaidia sisi kutambulisha theologia ya mjadala wa ukombozi, kupewa haki na kuchukuliwa, kila moja ikituonyesha maana ya kupokea maisha mapya na nini hutokea kwetu wakati tunapokea wakati maisha hayo mapya yamepokelewa. Maisha hayo mapya hutubadilisha kabisa, na maisha yetu yaliyobaki yamewekewa alama kukua kukuzwa kufanana na Yesu.

Baadaye, tunaanza kuona namna maisha mapya yalivyo ndani yetu, jinsi inavyokuwa, siyo kwa faida yetu tu, lakini kwa faida kubwa kwa familia zetu na jumuia. Maisha yetu mapya siyo ya kutunza sisi wenyewe lakini, kama kwenye hadithi ya Yosia, yale mabadiliko ndani yetu yanamaanishwa kutuongoza kwenye mabadiliko ya dunia inayotuzunguka pia.

**Kutazama mbele kwenye Misingi 3: *Maisha Huumba***
Kwenye kitabu kinachofuata, ***Maisha Huumba,*** tunatazama kwa undani namna maisha mapya ndani yetu kujiumba yenyewe kwenye dunia inayotuzunguka. Mkristo mwenye afya hujihusisha

na kuleta maisha mapya kwa wale wanaowazunguka na kujipalilia wao wenyewe.

Tutaendeleza kuelewa zawadi ya Roho Mtakatifu kwa undani zaidi na kujadili namna wafuasi wa Yesu wanaweza kujihusisha kuleta haki hapa duniani. Tutaendelea kujifunza namna ya kuombea jumuia zetu, na kujihusisha na njia tofauti kuwafikia wao na kudhihirisha upendo wa Mungu kwa ajili yao kwa matendo na kwa maneno pia.

**Maswali**

20 Dakika

Unapotazama nyuma kwenye vipindi 12 vilivyopita kwenye ***Misingi 2: Maisha Hukua,*** tumia muda kiasi kujadili kwenye vikundi vya 3 au 4 baadhi ya mafundisho mliyojifunza. Washirikishe baadhi yao juu ya ujuzi wako wa kuwashuhudia wengine kwenye jumuia yako ukijumlisha ujuzi ambao ulikuwa na changamoto zaidi.

Hatimaye, kama kikundi kimoja kikubwa, jaribianeni juu ya kifungu cha kukumbuka cha 13 muone kama mnaweza kusaidiana kukumbuka maandiko amabyo tayari mmekwishajifunza.

Kama kuna muda, mjadili ni vifungu gani mmegundua kuwa na msaada zaidi au zimezungumza na wewe kwa nia fulani kwa wiki 12 zilizopita.

**Maombi**

15 Dakika

Tunapokaribia kufunga kipindi hiki uwe na muda wa kutosha kuomba kama kikundi. Hii inaweza kuwa nafasi nzuri kuona kuwa kila moja kwenye kikundi ambaye hajapokea zawadi ya Mungu ya maisha mapya angependa kufanya hivyo, na kama watapenda basi utawaongoza kwa maombi yafuatayo:

> *Mungu mwema,*
> *Aksante kwa yote niliyojifunza kwako wakati wa mafundisho haya ya Misingi. Leo ningependa kupokea zawadi ya maisha mapya ambayo umenipa. Nakubali kwa yale uliyofanya*

*kwangu kupitia kufa na kufufuka kwa mwanao, Yesu, na napenda kuishi maisha mapya, huru kukua na kukuzwa ndani yako. Nisamehe kwa njia ambazo nilijaribu kuishi maisha yangu huko nyuma na kuomba msaada wako kuanza upya leo, na kukua ndani yako maisha yangu yote. Amina.*

Kufuatana na hili, uwe na muda wa kutosha ukiwaambia wanachama wa kikundi chako kama watahitaji maombi halafu muombeane, mkitiana moyo kupitia changamoto, na kuzungumzia upendo wa Mungu kwa moja kwa mwingine.

**Kufanya Wiki Hii**
Geukia mmea wako na ukumbuke baadhi ya njia ambazo unaweza ukasaidia kuunda hali nzuri ili iweze kukua (mfano uipatie maji, uweke kwenye nafasi nzuri, na kuilinda isiharibike). Unapotazama namna ya kulinda mmea wako unaokua, omba na utazame njia za kulinda imani yako inayokuwa na namna ya kuunda hali nzuri ili Mungu akukuze wewe (hii inaweza kujumlisha kuwa na muda wa kutosha kusom Biblia, kuomba na kusikiliza kwa Mungu, kutenda kwa utiifu kwa yale mambo anayokuagiza kutenda.)

**Shahidi**
Tafuta nafasi kuwa na muda kwa mtu 1-2 wanaokufahamu vizuri wiki embat bado hawajamfuata Mungu. Waambie wakwambie ni mabadiliko gani wamegundua kwaku tokea upokee zawadi ya maisha mapya. Kama wewe ni jasiri hasa utawaambia wawe wakweli na wakwambie ni mambo gani ambayo bado hayajabadilika kwao!

Baada ya kuğundua mabadiliko ndani yako, waulize kama watafurahia kumjua Mungu anayetupatia sisi maisha mapya na kutubadilisha kutoka ndani kuja nje.

# Kifungu cha Kukumbukas

‘Kama mnanipenda, mtazishika amri zangu. Nami nitamwomba Baba, naye atawapa Msaidizi mwingine akae nanyi milele. Huyo ndiye Roho wa kweli ambaye ulimwengu hauwezi kumpokea, kwa sababu haumwoni wala haumjui. Ninyi mnamjua kwa kuwa yuko pamoja nanyi naye anakaa ndani yenu.’

*Yohana 14:15-17*

‘Kwa hiyo msiwe wajinga, bali mpate kujua nini mapenzi ya Bwana… bali mjazwe Roho.’

*Waefeso 5:17-18*

‘Nasi sote, tukiwa na nyuso zisizotiwa utaji tunadhihirisha utukufu wa Bwana, kama kwenye kioo. Nasi tunabadilishwa ili tufanane naye, toka utukufu hadi utukufu my zaidi, utokao kwa Bwana, ambaye ndiye Roho.’

*2 Wakorintho 3:18*

‘Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwanawe wa pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.’

*Yohana 3:16*

‘Lakini tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole na kiasi. Katika mambo kama haya hakuna sheria.’

*Wagalatia 5:22-23*

‘Bwana akubariki na kukulinda;
Bwana akuangazie nuru ya uso wake na kukufadhili;
Bwana akugeuzie uso wake na kukupa amani.’

*Hesabu 6:24-26*

‘Kwa kuwa wote wametenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu.’

*Warumi 3:23*

‘Kuweni na huruma, kama Baba yenu alivyo na huruma. Msihukumu, nanyi hamtahukumiwa. Msilaumu, nanyi hamtalaumiwa. Sameheni, nanyi mtasamehewa.’

*Luka 6:36-37*

‘Ndani yake tunao ukombozi kwa njia ya damu yake, yaani, msamaha wa dhambi, sawasawa na wingi wa neema yake aliyotumiminia kwa wingi, kwa hekima yote na maarifa yote.’

*Waefeso 1:7-8a*

‘Kwa hiyo, kwa kuwa tumekwisha kuhesabiwa haki kwa imani, tuna amani na Mungu kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo.

*Warumi 5:1*

‘Kwa maana ninyi nyote mmekuwa watoto wa Mungu katika Kristo Yesu kwa njia ya imani..’

*Wagalatia 3:26*

‘Njooni kwangu, ninyi nyote mnaotaabika na kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha. Jifungeni nira yangu, mjifunze kutoka kwangu, kwa maana mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo, nanyi mtapata raha nafsini mwenu. Kwa maana nira yangu ni laini na mzigo wangu ni mwepesi.’

*Matayo 11:28-30*

‘Hivyo mwenye kupanda na mwenye kutia maji si kitu, bali Mungu peke yake ambaye huifanya ikue.’

*1 Wakorintho 3:7*

# Kumbukumbu

# Mpangilio wa Picha

| Picha | Undani wa Picha |
|---|---|
| Jalada la mbele | Imepigwa picha na Erol Ahmed siku ya Unsplash |
| Kikao cha 1 jina la ukrasa | Imepigwa picha na Ian Dooley siku ya Unsplash |
| Kikao cha 2 jina la ukrasa | Imepigwa picha na Scott Rodgerson siku ya Unsplash |
| Kikao cha 3 jina la ukrasa | Imepigwa picha na Jeremy Pagden siku ya Unsplash |
| Kikao cha 4 jina la ukrasa | Imepigwa picha na Jayakumar Ananthan siku ya Unsplash |
| Kikao cha 5 jina la ukrasa | Imepigwa picha na Samuel Zeller siku ya Unsplash |
| Kikao cha 6 jina la ukrasa | Imepigwa picha na Abigail Keenan siku ya Unsplash |
| Kikao cha 7 jina la ukrasa | Imepigwa picha na Nadia Supertino siku ya Unsplash |
| Kikao cha 8 jina la ukrasa | Imepigwa picha na Beth Tate siku ya Unsplash |
| Kikao cha 9 jina la ukrasa | Imepigwa picha na Aaron Burden siku ya Unsplash |
| Kikao cha 10 jina la ukrasa | Imepigwa picha na Monkgogi Samson siku ya Unsplash |
| Kikao cha 11 jina la ukrasa | Imepigwa picha na Sebastian Leon Prado siku ya Unsplash |
| Kikao cha 12 jina la ukrasa | Imepigwa picha na Wilco van Meppelen siku ya Unsplash |
| Kikao cha 13 jina la ukrasa | Imepigwa picha na Dikshit Mundra siku ya Unsplash |

MISINGI 2:

# Maisha Hukua

***Misingi*** ni mafundisho inayowasaidia watu kugundua na kukua ndani ya mahusiano yao na Mungu na kuwatia moyo kuhudumia jumuiya zao. Iliandikwa ili iweze kutoa vifaa vilivyo bora ambavyo vingeweza kutumika kwenye maeneo mengi ya kijiografia na kwenye vikundi vya kitamaduni duniani pote. Misingi ni mkusanyiko wa seti ya vitabu vine, na kila kimoja kinayo vipindi kumi na vitatu ya mafundisho kwenye vikundi.

***Misingi*** imeandikwa na waandishi wageni waliojitolea toka duniani kote na kukusanywa na kuandaliwa na Dignity.

***Misingi 2: Maisha Hukua*** na kujenga msingi itakayowezesha imani kukua na kutoa ufahamu kwa baadhi ya maandiko yanayotumika ya Biblia na maombi.

**Wasiliana nasi kwa hello@dignityonline.org.uk au +44(0)7340 573 937.** **Kwa majina ya vitabu vyetu vyote na gharama tembelea tovuti yetu: www.dignityonline.org.uk/publications.**

Swahili Toleo la kwanza
Aliyeandaa jalada: The Message Trust
Picha ya jalada: Erol Ahmed/Unsplash

DIGNITY

www.dignityonline.org.uk